**19 APRILI, 2023**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA MOJA**

**Kikao cha Kumi – Tarehe 19 Aprili, 2023**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

**NAIBU SPIKA:** Hati za Kuwasilisha Mezani; Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge, Utawala, Katiba na Sheria. *(Makofi)*

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Tunaanza maswali, Ofisi ya Waziri Mkuu. Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea.

Na. 123

### Mpango maalum wa kuwapatia vijana mafunzo ya ujuzi kupitia VETA nchini

**MHE. BONNAH L. KAMOLI** aliuliza:-

Je, ni Watanzania wangapi wamejitokeza na kupata fursa ya mafunzo maalum ya ujuzi yaliyotangazwa kupitia *VETA* kote nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, Mbunge wa Segerea kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu kuanza kutekeleza Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi mwaka 2016/2017, kupitia Vyuo vya *VETA,* Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi *(FDC)* na Vyuo Binafsi, jumla ya vijana walioomba mafunzo ni 215,233 na waliopatiwa mafunzo ya ujuzi ni 96,894 ambapo kati yao vijana 74,578 wamepatiwa mafunzo kwa njia ya uanagenzi na vijana 22,296 wamepatiwa mafunzo kupitia njia ya urasimishaji ujuzi *(RPL)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bonnah.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali, lakini nilikuwa na maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; je, Serikali imejipangaje kutokana na miradi mikubwa ambayo inaendelea hapa kama Bwawa la Mwalimu Nyerere lakini pia na Miradi ya *SGR;* ili kuhakikisha vijana wetu wa Tanzania wanaenda kusimamia hii miradi pindi itakapokamilika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili: Ili kuendana na Uchumi wa Bluu; je, Serikali imejipangaje kufundisha vijana wetu kwenye mambo ya uvuvi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU (MHE. PASCAL P. KATAMBI):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba kujibu maswali

mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bonnah Ladislaus Kamoli, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Serikali ilimeshaliona hilo na kwa maagizo ya Mheshimiwa Rais na maelekezo mahususi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ile miradi wakati inaanza tayari tulishatambua vijana ambao walipaswa kuchukuliwa na kwenda kupata mafunzo zaidi. Katika Mradi wa Reli ya Kisasa, vijana 3,526 tayari walishaajiriwa. Kati ya hao, tumewatambua vijana 1,916 ambao wataenda kwenye vyuo vyetu mbalimbali na ndio watakaofanya *succession plan* kwenye maeneo hayo kwa ajili ya masuala ya teknolojia na ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, likiwa sambamba na Bwawa la Mwalimu Nyerere ambapo ni zaidi ya vijana wa Kitanzania 10,228 ambao tumewaajiri, kati hao 146 tumeshawatambua na tutawasajili kuweza kuwajazia na kuwajengea ujuzi na *skills* za kuweza kuendelea hata baada ya watalamu wa kigeni wale kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili katika *succession plan;* sheria yetu inaendelea kusimamia *seccession plan* ya *local content* ili ilete faida zaidi kwa Watanzania hasa katika kununua bidhaa za ndani na pia kupata wafanyakazi wa Kitanzania kwenye miradi hii ya maendeleo na kuweza kujeza kujenga uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kuhusiana na *Blue Economy,* tayari kupitia Wizara yetu ya Uvuvi, wapo vijana ambao wanapata mafunzo na ufugaji wa samaki umeshaanza, ufugaji wa vizimba kule Mkoa wa Mwanza, pia tunafanya kwenye maeneo ya bahari ikiwa ni pamoja na Tanzania Zanzibar, tayari programu hii ipo, imeshaanza kufanya kazi na Mheshimiwa Rais ameendelea kutoa fedha kwa ajili ya kuwawezesha vijana hawa kwa kujiandaa na uchumi wa kisasa, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Deus Clement Sangu.

Na.124

**Kituo cha Afya cha Laela kuwa Hospitali ya Wilaya**

**MHE. DEUS C. SANGU** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupanua Kituo cha Afya cha Laela na kuwa katika hadhi ya Hospitali ya Wilaya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kituo cha Afya Laela kinamilikiwa na Kanisa Katoliki ambapo Mwaka 2004 kiliingia mkataba wa kutoa huduma na Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga ili kuhakikisha wananchi wa Kata ya Laela wanapata huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, Serikali itatenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya kipya katika Kata ya Laela ambacho kitakuwa na uwezo wa kutoa huduma za afya pamoja na huduma za upasuaji za dharura.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga imeshajenga Hospitali ya Wilaya,

Kituo cha Afya cha Laela kitatoa huduma kwa ngazi ya kituo cha afya, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sangu.

**MHE. DEUS C. SANGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa ya maswali madogo ya nyongeza. Kwanza, naishukuru Serikali kwa kukubali ombi hili na nimpongeze Mheshimiwa Waziri Mkuu aliahidi, wananchi wa Laela wanamshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza la nyongeza; Kata ya Ilemba ina wakazi wapatao 30,000 na ni miaka kumi sasa wanajenga kituo chao cha afya, hakijakamilika: Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga juhudi za wananchi kukamilisha kituo hiki cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili; Kata ya Msandamuungano kuna kituo cha afya ambacho kinajengo moja tu la *OPD;* Serikali ina mpango gani wa kuongeza majengo ili kiweze kutoa huduma zote zinazohitajika katika kituo cha afya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Deus Clement Sangu, Mbunge wa Jimbo la Kwela, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kata hii ya Ilemba ambayo ameitaja Mheshimiwa Mbunge ambayo wananchi wameanza ujenzi wa kituo cha afya; kwanza nitumie fursa hii kuwapongeza wananchi wa Kata hii kwa kuongeza nguvu zao katika ujenzi wa kituo hiki cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwahakikishie kwamba Serikali imeweka mpango mzuri wa kuunga nguvu za wananchi katika ukamilishaji wa majengo ya vituo vya afya na zahanati na tutaendelea kutenga bajeti na mara tukiwa na fedha hiyo, tutaona uwezekano pia wa kuchangia kukamilisha hicho kituo cha afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na Jengo la *OPD* lililopo katika kituo hicho, ni kweli tuna vituo vingi vya afya vyenye majengo machache na vinahitaji kuongezewa majengo mengine, na mpango wa Serikali ni kuendelea kutafuta fedha na kupeleka kwenye majengo haya kikiwemo kituo hiki ili majengo yakamilike na kutoa huduma bora kwa wananchi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kituo cha Njombe Mjini ni kituo kongwe katikati ya Mji, kimekuwa na ahadi za muda mrefu: Ni lini sasa kituo hiki kitapanuliwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Deo Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kituo cha Afya cha Njombe Mjini ni kikongwe na ni chakavu, na pia kina miundombinu michache na Serikali imeshafanya tathmini ya uhitaji wa majengo ya ziada na kazi inayoendelea sasa ni kutafuta fedha ili fedha ikipatikana tukaongeze majengo yale na kukiwezesha kile kituo cha afya kufanya kazi inayotarajiwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Wananchi wa Kata ya Narumu wameshatenga eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha afya cha Kata ya Narumu; je, ni lini Serikali itatuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa kituo hiki cha Narumu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, Mbunge wa Jimbo la Hai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwapongeze wananchi wa Kata ya Narumu kwa ajili ya kutenga eneo kwa ujenzi wa kituo cha afya. Pia niwatie moyo kwamba waanze kwa nguvu zao kujenga kile kituo cha afya na baadaye Serikali ikipata fedha, basi tutakwenda kuwaunga mkono, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Leah Komanya.

Na. 125

**Kukamilisha maboma ya ofisi – Meatu**

**MHE. LEAH J. KOMANYA** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa maboma ya Ofisi Kata za Nkoma, Mwangudo, Mwamanimba na Imalaseko – Meatu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uwepo wa maboma manne ya Ofisi za Kata ya Nkoma, Mwangudo, Mwamanimba na Imalaseko katika Jimbo la Meatu ambayo yanahitaji kukamilishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Bajeti ya mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Halmashauri ya Meatu imetenga fedha za mapato ya ndani kiasi cha shilingi milioni 60 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya Ofisi za Kata ya Imalaseko na Lingeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwenye vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya ofisi za Kata nchini kote zikiwemo Kata za Nkoma, Mwangudo na Mwamanimba, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Leah.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali kwa kutambua uwepo wa maboma nchini.

Je, Serikali haioni haja ya kutafuata programu nyingine ya kufanya maboresho katika Ofisi za Kata baada ya programu ya Ruzuku ya Uendelezaji Mitaji Serikali za Mitaa kukoma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliridhia watendaji walipwe shilingi 100,000; je, Serikali sasa haioni yale malipo

yao yakakatwa *at source,* yakalipwa na Hazina katika mapato ya Halmashauri kwa sababu yanapitia kwenye mfumo wa *Treasury Single Account* ili kuondokana na usumbufu unaotokana na ucheleweshwaji wa Watendaji wa Kata kupata yale mafao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya, Mbunge wa Jimbo la Meatu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Ofisi za Maafisa Watendaji za Kata, na pia Ofisi za Watendaji wengine wote wa Serikali katika Halmashauri zetu na ndiyo maana imeendelea kutenga fedha kwa awamu, kuhakikisha kwamba tunakamilisha majengo hayo na fedha hizo ni kupitia mapato ya ndani, na pia kupitia fedha za Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nachukua fursa hii kuwakumbusha na kuwasisitiza Wakurugenzi wote wa Mamlaka za Serikali Mitaa kote nchini kuweka kipaumbele katika bajeti za mapato ya ndani kwa ajili ya Ujenzi wa Ofisi za Kata na pia Ofisi za Vijiji na Ofisi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusiana na posho za Maafisa Watendaji wa Kata shilingi 100,000, Serikali ilishatoa maelekezo, na ni wajibu wa Wakurugenzi kuhakikisha fedha za posho za Watendaji wa Kata zinawafikia kwa wakati bila ucheleweshaji wowote. Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutafuatilia kuhakikisha kwamba fedha hizo zinawafikia kwa wakati, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona. Swali langu ni kwamba; je, ni lini Serikali itapeleka fedha Wilayani Kilwa kwa ajili ya ujenzi wa ofisi za Maafisa Watendaji Kata wa Kata za Somanga, Namayuni, Mitole na Njinjo?

**NAIBU SPIKA:** Hebu rudia tena swali lako.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Je, ni lini Serikali itapeleka fedha katika Wilaya ya Kilwa kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi za Maafisa Watendaji Kata za Somanga, Njinjo, Mitole pamoja na Namayuni?

**NAIBU SPIKA.** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaelekeza kutumia fedha za mapato ya ndani kuanza Ujenzi wa Ofisi za Maafisa Watendaji wa Kata. Nitumie fursa hii kusisitiza Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kilwa kutenga fedha kwa ajili ya Kata hizi za Somanga na Kata nyingine ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitaja, ili watendaji wetu wapate maeneo mazuri ya kufanyia kazi, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi.

Na. 126

**Mpango wa kudhibiti mafuriko Mto Mara**

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI** aliuliza:-

Je, kuna mpango gani wa kudhibiti mafuriko katika Mto Mara kwa kuvuna maji kupitia Mabwawa na kujenga Skimu za Umwagiliaji?

**NAIBU WAZIRI:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais, tayari imezindua Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira *(Environmental Master Plan for Strategic Intervention 2022-2032)* ambao umeelekeza mikakati na shughuli endelevu zitakazoweza kufanyika katika maeneo hayo ni kama vile: kuimarisha usimamizi wa vyanzo vya maji na kuhakikisha uwepo wa mtiririko wa uhakika katika mito ikiwemo Mto Mara, Mto Kagera, Mto Ruaha Mto Wami na Ruvuma; kuhamasisha matumizi sanifu kwa watumiaji wote wa Mto Mara, Kagera, Ruaha, Momba na Mto Ruvuma; na kuimarisha viwango vya maji katika vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Mto Mara ni moja ya miongoni ya Mito mikubwa muhimu nchini Tanzania. Hivyo, Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais na Wizara nyingine za

kisekta zitakaa na kuona namna bora ya kuvuna maji ili kudhibiti mafuriko, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Jeremiah.

**MHE. JEREMIAH M. AMSABI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na naishukuru Serikali kwa majibu mazuri. Hata hivyo, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza: Vijiji vya Borenga, Nyiboko, Buchanchali, Nyasulimunti na Gantamome ambavyo vipo kando kando ya Mto Mara kwa muda mrefu sasa vimeendelea kupata adha kubwa na hasara ya mafuriko katika mashamba, na tunaona mpango huu wa Serikali wa miaka kumi: Je, ni lini mpango huu utaanza ili kuondoa hadha hii inayoendelea katika maeneo hayo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Kumekuwepo na mpango mzuri na maarufu kabisa wa Serikali uliojulikana kama *Nile Basin Initiative* ambao unahusisha maeneo haya ya Mto Mara kujengewa mabwawa makubwa, *scheme* za umwagiliaji na kudhibiti mafuriko haya: Je, mpango huu sasa wenyewe umefikia wapi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah Amsabi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika Serikali hasa kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira tunayo nia ya kuhakikisha kwamba tunafanya huo mradi ambao Mheshimiwa ameupendekeza ama ameutaja. Kikubwa nimwambie Mheshimiwa awe na subira kwa sababu miradi hii

kwanza lazima tufanye utafiti, tuone namna itakavyowezekana lakini lazima kuna Wizara tukae, kwa sababu kama tunavyoona hili jambo lina Wizara za kisekta lazima tukae Wizara ya Maji, tukae Wizara ya masuala ya Kilimo pia na sisi tukae pamoja, lakini kubwa zaidi atupe muda kidogo tutafute fedha kwa ajili ya kurekebisha ama kukamilisha mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili nimwambie kwamba Wizara hii ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira tumekuwa tuna utaratibu wa kutembelea miradi takribani yote ambayo inasimamiwa na Ofisi yetu. Kila tunapokwenda tunatoa maelekezo kwamba kwanza miradi ikamilike kwa wakati, pili, miradi iwe ya kiwango, lakini tatu, miradi hii ihakikishe kwamba inanufaisha walengwa. Nimwambie tu kwamba miradi yote iliyo katika eneo lake ama jimbo lake tutaifuatilia na tutatoa maelekezo na itakamilika kwa wakati, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa George Mwenisongole.

Na. 127

**Kuondoa makato kwa wakulima wa kahawa – Mbozi**

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaondoa makato yaliyopo kwenye Vyama vya Msingi kwa Wakulima wa Kahawa Mbozi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa George Ranwell Mwenisongole, Mbunge wa Mbozi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na mapitio ya makato yaliyopo kwenye vyama vya ushirika kwa wakulima katika mazao mbalimbali ikiwemo zao la kahawa. Kufuatia malalamiko tuliyoyapokea kutoka kwa wakulima wa kahawa Mkoani Songwe, Serikali iliunda Timu kwa ajili ya kufuatilia na kufanya tathmini kuhusu masuala mbalimbali yahusuyo zao la kahawa ikiwemo suala la makato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Timu hiyo imekamilisha tathmini na inatarajia kuiwasilisha Wizarani mapema Mwezi ujao. Hivyo, baada ya kupitia taarifa hiyo ya tathmini, Serikali itachukua hatua stahiki.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa George.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; tatizo ni muda, mwezi Juni na mwezi Mei mwishoni wakulima wa kahawa wanaanza kuvuna kahawa yao kupeleka kwenye hivyo Vyama vya Msingi, sasa Waziri anaposema mwezi ujao, kwa nini hili suala lisifanyike mapema kabla ya msimu wa kuuza haujaanza ili hayo makato yaondolewe na wakulima wapate chao?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; niipongeze Serikali kwa uamuzi wa kuwafutia leseni mawakala wa mbolea 700. Kwa kweli hii ni hatua nzuri na naomba wasirudi nyuma wakaze buti, hatuwezi kutishwa na watu wasiokuwa waaminifu, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri wakati naingia hapa Bungeni taarifa imekwishafika Wizarani, kwa hivyo tutaanza kulifanyia kazi mwezi huu ili kuuwahi msimu.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali la nyongeza. Naomba sasa kuiuliza Serikali swali la nyongeza. Je, Wizara ya Kilimo ina mkakati gani wa kuhakikisha wakulima wa kahawa wa Wilaya ya Ngara wanaendelea kuuza kahawa yao kwa bei nzuri kama ilivyokuwa kwenye msimu uliopita? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mbunge kwa kazi nzuri ambayo anaifanya kwenye zao hili la kahawa, nataka tu nimhakikishie kwamba utaratibu ambao tulioanza nao ulimpa mkulima bei nzuri, tutaendelea nao. Vilevile tutahakikisha kwamba tunamsaidia mkulima kupata masoko ya uhakika na azalishe kahawa yenye ubora ili iweze kumpatia bei nzuri sokoni. Kwa hiyo nimwondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba wakulima wa kahawa Mkoa wa Kagera na maeneo mengine wataendelea kunufaika na utaratibu ambao tumeuweka hivi sasa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sophia.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kama ilivyo kwa zao la kahawa kuwa na tozo nyingi; je, ni lini, Serikali itafanya marejeo tena kwa zao la parachichi hasa katika Mikoa ya Njombe na Wilaya ya Rungwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza ambalo tumelifanya kwenye parachichi ni kukaa na wadau na kutengeneza mwongozo wa pamoja wa zao ambao pia ndani yake tutajadili makato yote na namna ya uendeshaji wa zao hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimtoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba na lenyewe pia tumelipa kipaumbele kwa sababu parachichi ndio dhahabu yetu ya kijani, kwa hiyo tunaiangalia katika jicho la kipekee sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cherehani.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wakulima wa tumbaku wamekatwa makato makubwa sana ya upandaji wa miche ya miti ambapo ni zaidi ya shilingi 813 kwa kila mche mmoja.

Sasa kwa nini, Serikali isiondoe kabisa makato haya kwa wakulima wa tumbaku ili waweze kupanda miti kwa hiari yao bila makato yoyote?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge na tuna kikao cha wadau ambacho tutajadili mambo haya na kuweza kukubaliana kwa pamoja. Kwa hiyo tumeuchukua ushauri wa Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara. Mheshimiwa Neema Lugangira.

Na. 128

**Kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji**

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA** aliuliza:-

Je, Serikali imejiandaaje kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba ya Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuna mazingira wezeshi Serikali imeendelea kutekeleza Mpango

wa Kuboresha Mazingira ya kufanya Biashara Nchini (MKUMBI) lakini pia kuboresha sera na sheria mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako tukufu, Serikali ilitunga Sheria mpya ya Uwekezaji Tanzania ya mwaka 2022 ambayo pamoja na masuala mengine imeboresha na kulinda maslahi ya wawekezaji na uwekezaji, kuboresha huduma kwa wawekezaji katika kupata vibali na leseni mbalimbali kupitia mfumo unganishi wa kielektroniki katika kuhudumia wawekezaji, kuboresha utoaji wa vivutio vya kikodi kwa wawekezaji kwa kuongeza muda kutoka miaka mitatu hadi mitano na kutoa vivutio katika miradi ya upanuzi na ukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia inaendelea kuboresha miundombinu wezeshi kama barabara, reli, bandari, viwanja vya ndege na umeme, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Neema.

**MHE. NEEMA K. LUGANGIRA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Serikali ni vyema tutambue kwamba Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, anaweka jitihada kubwa sana kuimarisha mazingira wezeshi na kuvutia wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi na hiyo imeenda sambamba kabisa na Mheshimiwa Rais kuamua kuchukua jukumu la uwekezaji na kuweka chini ya Ofisi ya Rais, pamoja na kuteua Katibu Mkuu wa Uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; *Blueprint* imeelekeza kwamba ili kuimarisha mazingira wezeshi lazima tuwe tuna ardhi inayojulikana kwa ajili ya uwekezaji kwa maana ya kwamba ardhi hiyo ipimwe na iainishe ni uwekezaji gani ambao uatafanyika sasa je, mpaka hivi sasa Serikali

imepima kiwango gani cha ardhi na ramani ya ardhi hiyo kwa ajili ya uwekezaji inapatikana wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; pamoja na kwamba Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 2022 ilipitishwa ndani ya Bunge lako Tukufu kwenye *blueprint* imeelekeza zaidi ya sheria 20 ambazo zinatakiwa zifanyiwe maboresho.

Kwa hiyo ningependa kufahamu kutoka kwa Serikali, je, ni lini Serikali italeta hizo sheria zingine zaidi ya 20 ili zifanyiwe maboresho ili kuhakikisha kwamba tunaimarisha mazingira wezeshi hapa nchini na hivyo kuunga mkono na kutokufifisha jitihada za Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan za kuimarisha na kuleta wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Swali la kwanza Mheshimiwa Waziri linahitaji takwimu tutaliacha. Jibu swali la pili.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Neema Kichiki Lugangira, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la msingi tumeshaanza kutekeleza MKUMBI au *Blueprint* na moja ya utelekezaji huo ni kuhuisha au kutunga Sheria mpya ya Uwekezaji lakini pia ninyi ni mashahidi katika Bunge liliopita tumepitisha maboresho ya sheria mbalimbali zaidi ya 19 ambazo ziligusa sekta tofauti tofauti. Kama nilivyosema utekelezaji wa MKUMBI au *blueprint* sio kitu cha siku moja, kwa hiyo tunaendelea kutekeleza moja ya maeneo ambayo Mbunge ameyasema ni hayo ya kupitia baadhi ya sheria na kanuni lakini pia kuboresha baadhi ya taratibu ambazo zipo na tunazoona ni changamoto au kero kwa ajili ya kuboresha uwekezaji hapa nchini, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chomete.

**MHE. GHATI Z. CHOMETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. Pamoja na uwekezaji mzuri kufanyika wa kujenga Kiwanda cha Nguo cha *MUTEX* Musoma, lakini mpaka sasa kiwanda kile hakifanyi kazi. Je, ni upi mkakati wa Serikali kufufua kiwanda hicho?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli moja ya mikakati tunayoifanya Serikali ni kuona namna gani tunafufua viwanda ambavyo havifanyi kazi na sisi kama Serikali tumeshaanza kuona vile viwanda ambavyo vilikuwa vimepewa watu binafsi na hawaviendelezi kuvirudisha Serikalini na hatua ya pili sasa ni kuvitafutia wawekezaji ili waweze kuwekeza katika viwanda hivyo na kimojawapo ni kiwanda hiki cha *MUTEX* kilichopo kule Musoma, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

Na. 129

**Wananchi wa Nanyumbu waliofidiwa kutokana na uharibifu wa mashamba**

**MHE. YAHYA A. MHATA** aliuliza: -

Je, ni wananchi wangapi wa Jimbo la Nanyumbu wamefidiwa kutokana na uharibifu uliofanywa na tembo katika mashamba yao?

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahya Ally Mhata, Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2022/2023, Wizara ilipokea jumla ya maombi nane kutoka kwa wananchi wa Vijiji vya Mchenjeuka, Lukula, Masuguru, Marumba na Mpombe walioathiriwa na matukio ya wanyamapori wakali na waharibifu katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyumbu. Baada ya taratibu za malipo kukamilika, mnamo tarehe 21 Machi, 2023, Wizara ilifanya malipo ya kifuta jasho ya jumla ya shilingi 5,160,000 kwa wananchi saba wa Vijiji vya Michenjeuka, Lukula, Masuguru na Mpombe waliharibiwa mazao. Aidha, mwezi Machi mwaka huu, Wizara ilipokea maombi mapya 12 ya wananchi wa Vijiji vya Nanyumbu na Marumba ambayo yanaendelea kushughulikiwa kwa ajili ya kuandaa malipo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba niulize maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; takwimu ananzozieleza Naibu Waziri sio sahihi. Takwimu ambazo ninazo za waathirika wa wanyama waharibifu ni zaidi ya watu 200.

Je, Waziri yupo tayari kumwagiza Afisa wake aliyopo pale Masasi aende akafanye mapitio mapya ya waathirika wote walioathirika na Wanyama waharibifu hasa tembo katika Kkata ya Sengenya, Kijiji cha Mkumbaru, Chinyanyera, Igunga; Kata ya Nangomba Kijiji cha Chihuve; Kata ya

Luimesule; na Kata ya Masugulu? Takwimu hizi sio sahihi kwa hiyo namuomba Waziri afanye hayo kama nilivyomwelekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili; fidia wanazolipwa waathirika ni ndogo kuliko hali halisi ilivyo. Waathirika hawa wanaopoteza maisha yao fidia ni ndogo, wanaopata ulemavu fidia ni ndogo na wanaoharibiwa mashamba yao fidia ni ndogo. Je, Waziri yuko tayari kuleta Muswada hapa wa kurekebisha viwango hivi ili wananchi walipwe haki sawa kulingana na hali halisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahya Ally Mhata**,** Mbunge wa Jimbo la Nanyumbu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwenye hili suala la takwimu nitazichukua kutoka kwake, lakini pia tutaenda kuhakiki upya katika maeneo hayo ili wananchi waweze kulipwa stahili yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye upande huu wa fidia sheria ya mwaka 2011 iliyopitisha kifuta machozi na kifuta jasho ilikuwa na madhumuni ya kumshika mkono mwananchi, lakini ukiangalia namna ya kufidia mfano maisha ya mwananchi ambaye amepoteza maisha ni ngumu sana kufidia au mtu ambaye amepata ulemavu, hivyo sheria hii ilipitishwa kwa ajili ya kumshika mkono mwananchi kumwonesha kwamba Serikali iko pamoja naye.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo katika Bunge lako hili mwaka jana tulipewa maelekezo ya kuzipitia upya Kanuni zake zinazohusiana na masuala ya kifuta machozi na jasho na hivi karibuni tutaileta katika Bunge lako hili kwa ajili ya

kuipitia ili tuweze kuongeza kiwango hiki na Kanuni zirekebishwe, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Endapo ikitokea mwananchi ameua tembo au gari limegonga tembo au mnyama yoyote faini anayotozwa ni kubwa sana, lakini ikitokea vinginevyo kwamba mnyama amemuua mwananchi au ameharibu mazao yake, sheria haimpi haki mwananchi. Je, nini kauli ya Serikali ku-*balance* haya mambo ili kuhakikisha kwamba Mtanzania anapata haki yake ndani ya nchi yake? (*Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tutambue kwamba hawa wanyama ambao tunao katika nchi yetu ni rasilimali za Taifa na wanalindwa kisheria kama ambavyo tunawalinda wanadamu na tutambue kwamba changamoto hii ya wanyamapori wakali na waharibifu imeanza hivi karibuni. Miaka ya nyuma wanyama hao walikuwa wanaishi kwa uhuru na salama kabisa na hatukuwahi kuwa na changamoto hizi. Kwa hiyo ukiangalia mahitaji ya ardhi, ongezeko la watu tumeendelea kusogea katika maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukisema leo hii changamoto hii tuielekeze kwenye faini, mzigo ni mkubwa sana kwa Serikali hautaweza kugharamia hasara ambayo itaweza kujitokeza. Kwa hiyo tunaendelea kuhamasisha wananchi kwamba tusiendelee kuyasogelea maeneo haya na ndio maana

kanuni hii ilitungwa kwa wale ambao Wanyama wamewafata basi tunawashika mkono ili kuhakikisha kwamba Serikali inaonesha kwamba iko nao.

**NAIBU SPIKA:** Waziri anasema msijenge nyumba zenu kwenye *corridor* za wanyama.

Mheshimiwa Naibu Waziri kuna kero ya popo Kata ya Kivukoni Jimbo la Ilala. Hawa popo ni waharibifu, wanachafua mazingira na wananchi walishalalamika mpaka leo bado. Hebu tueleze mnachukua hatua gani kwa upande wa popo Kata ya Kivukoni? *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuna changamoto ya popo ambao wamezunguka katika maeneo ya Dar es Salaam hususan maeneo yanayozunguka Ikulu. Serikali imeshaanza kuyafanyia kazi tulishawahi kufanya kazi ya kuwapuliza kwa maana ya kuwapunguza, lakini changamoto tunayoipata ni kwamba tunapowaondoa wanaruka wanaondoka, lakini kuna muda ambao wanarudi. Sasa tumeshaanza utaratibu na Taasisi ya *TAWIRI* kutafuta mbinu mbadala kuhakikisha tunawaondoa kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuahidi kabla ya Bunge lako hili la bajeti kwisha, tutakuwa tayari tumeshakamilisha utaratibu wa kuwaondoa.

**NAIBU SPIKA:** Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Cosato David Chumi.

Na. 130

**Mafinga kunufaika na Mradi wa Umeme *Peri–Urban***

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Je, ni lini Mafinga itanufaika na Mradi wa Umeme wa *Peri-Urban*?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya maeneo na Mitaa ya Mji wa Mafinga yatanufaika na Mradi wa Ujazilizi Awamu ya Pili C *(Densification IIC)* ambao upo katika hatua za ununuzi wa Wakandarasi. Aidha, Serikali imekamilisha uhakiki wa vitongoji visivyo na huduma ya umeme na kuandaa mradi kabambe wa kusambaza umeme katika vitongoji vyote uitwao *Hamlet Electrification Project* ambapo Mafinga Mjini nayo itanufaika na mradi huu. Mradi huu unatarajiwa kutekelezwa kuanzia Mwaka wa fedha wa 2023/2024 kulingana na upatikanaji wa fedha, nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chumi.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; je, Serikali wako tayari kukaa na mimi ili kuweza kufahamu hivyo vitongoji ambavyo vinaweza

kunufaika na ujazilizi wa awamu ya pili unaoitwa IIC ni vitongoji gani na vingapi ili tuondoe mchanganyiko kwa sababu kuna wakati mwingine vitongoji vya Mafinga vinasomeka Mufindi na pale kuna Halmashauri ya Mji Mafinga na Halmashauri ya Mufindi. Kwa hiyo je, wako tayari kukaa na mimi ili tujue hivyo vitongoji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; tunaipongeza Serikali kwamba maeneo ya vijijini bado wananchi wataingiza umeme kwa shilingi 27,000, lakini maeneo kama ya Mafinga yako maeneo pamoja na kuwa ni Mafinga Mji, lakini maisha, mazingira na kipato ni kama maisha ya kijijini.

Je, Serikali iko tayari maeneo kama hayo kama vile Ndolezi, Luganga na Ulole na wenyewe kuwapa bei nafuu katika kuingiza umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Chumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wetu wa *Densification 2C* utakuwa na una takribani vitongoji kama 2,562. Kama alivyoomba, na mimi niko tayari, baada ya hapa nitakaanaye ili nimuoneshe vitongoji ambavyo vitakuwa ni vya eneo lake kwa ajili ya kuhudumia wananchi katika Jimbo lake la Mafinga Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye swali la pili, kama ambavyo tumeeleza siku chache zilizopita, ni kweli Wizara ilituma timu yake kwenda katika majimbo yetu yote Tanzania ili kuhakiki yale maeneo ambayo yapo mijini, lakini yana uso wa vijiji ili kuweza kuwapangia bei ambayo ni stahiki na wanayoweza kulipa. Lakini kwa bahati mbaya taarifa tuliyoipata baada ya kui-*verify* humu Bungeni, tulibaini kuna

Waheshimiwa Wabunge hawakushirikishwa. Kwa hiyo tumeiagiza ile timu irudi tena na kwenda kubaini upya hayo maeneo na ituletee taarifa. Hivyo taarifa hiyo itakapofika tutashirikishana hapa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, tunapanga bei ambayo wananchi wataimudu kwa ajili ya kuweza kuunganisha gharama za umeme.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea Wizara ya Afya. Mheshimiwa Husna Sekiboko.

Na. 131

**Udhibiti wa matumizi holela ya dawa za binadamu**

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kudhibiti matumizi holela ya Dawa za Binadamu nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko, Mbunge, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kudhibiti matumizi holela ya dawa za binadamu nchini Serikali inatekeleza mambo yafuatayo: -

(i) Kutoa elimu juu ya matumizi sahihi ya dawa kwa wananchi kupitia vyombo vya habari ikiwemo vipindi vya elimu kwa umma kwa kutumia wataalamu wa dawa.

(ii) Kusimamia muongozo wa matibabu nchini unaobainisha matibabu kwa kila ugonjwa ikiwemo dawa zinazohitajika kutibu magonjwa hayo.

(iii) Kusimamia weledi wa watoa dawa katika maeneo yote yanayohusika na utoaji wa dawa kama vile maduka ya dawa na vituo vya kutolea huduma za afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Husna.

**MHE. HUSNA J. SEKIBOKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa nafasi hii. Moja ya kisababishi kikubwa cha matumizi holela ya dawa za binadamu ni kukosekana kwa wafamasia kwenye vituo vya ngazi ya chini, kwa maana ya zahanati.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kusambaza wafamasia kwenye vituo vyote vya kutolea huduma za afya nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; matumizi ya dawa holela yanaambatana au yanaenda sambamba na utengenezaji na usambazaji wa dawa holela. Hivi karibuni tumeshuhudia *TMDA* wamekamata watu mbalimbali wakiwa wanafanya shughuli hizo.

Je, Serikali sasa ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba, mambo hayo yanasitishwa na hayatokei tena kwa afya ya binadamu, Mtanzania?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge. Kwanza nimpongeze kwa sababu, swali lake ni muhimu sana na limekuja kwa wakati muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza linasema ni kwa namna gani tunaweza tukahakikisha kwamba, vituo vyetu vya afya na zahanati kuna wafamasia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwahakikishia kwamba, wafamasia, lakini tunaweza tukachukua wale waliosomea dawa, *certificates* na *diploma*. Tutashirikiana na wenzetu wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, ili kuona kila wakati ni namna gani tutapunguza hilo *gape* kwa kuajiri watu wa namna hiyo ili kuweza kusimamia dawa vizuri kule chini.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini swali lake la pili ni kuhusu kwamba, kunakuwepo na utengenezaji holela wa dawa, kwa maana unamaanisha dawa ambazo ni *fake:* -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza moja inaeleweka kabisa kwamba, tunayo taasisi yetu ya *TMDA* na inafanya kazi nzuri ya kuhakikisha hayo mambo hayatokei. Kikubwa tunaendelea, tunapoelimisha yote haya, elimu hiyo kwa jamii kwamba, watoe taarifa, tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha tunadhibiti hawa wahalifu wanaofanya kazi hiyo, na kwamba wakipatikana wanapewa adhabu kubwa ambayo itawafanya wasirudie tena.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zoezi la ukaguzi wa ubora wa dawa linafanyika katika vituo vya wauza dawa nchini, kitendo ambacho kinaleta hasara kubwa kwa wafanyabiashara hawa;

Je, Serikali haioni umuhimu sasa wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa ubora wa dawa katika hatua za mwanzo kwenye viwanda ili wafanyabiashara wasipate hasara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, moja ni kwamba, kwenye kudhibiti suala la dawa na wafanyabiashara ya dawa wenzetu wakati mwingine wanaangalia kutengeneza faida kuliko usalama wetu sisi watumiaji. Kwa hiyo suala la wao kuendelea kusimamiwa kwa nguvu na kuhakikisha kwamba wanafuata taratibu ni lazima tuwasimamie namna hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini tumekuwa na mjadala wa kuhakikisha sasa badala ya kuwepo na wafamasia kwenye maduka ya dawa ambao wanaweka vyeti vyao, tubadilishe hiyo sheria iwe sasa mfamasia anaajiriwa kwenye duka husika na anakuweko pale kuhakikisha usalama unakuweko, na hasa kazi ya ukaguzi inakuwepo kwa mambo ambayo hayaendani na utaratibu yanazuiliwa mapema.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katimba.

**MHE. ZAINAB A. KATIMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna dawa ambazo zinanunuliwa bila cheti cha daktari, *(over the counter medication)* na kuna dawa zile ambazo ni lazima uwe na cheti cha daktari, ili uweze kununua, *(prescription medication)*.

Je, Serikali inafanya jitihada gani na ina mikakati gani thabiti ya kuhakikisha kwamba, zile dawa ambazo zinahitaji cheti cha daktari hazinunuliwi *over the counter*? Yani, hazinunuliwi bila cheti cha daktari; na hasa kwa sababu, dawa za aina hii zinatumika na wale wenye uraibu wa dawa za kulevya?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Katimba, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni mambo ambayo tunakuwa tunaelimisha. Katika elimu hii tunayoitoa ni kuhakikisha kwamba watu wetu hawafanyi hivyo. Ukimsikia Mbunge mwenzetu akisema kuna baadhi ya maduka ya dawa ambayo tumekuwa tunawafungia na wamekuwa wakipewa adhabu mbalimbali, ni kwa sababu ya makosa kama hayo na kuna utaratibu wa kusimamia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka kukuhakikishia tukienda sasahivi kuhakikisha kwamba maduka ambayo wafamasia waliopo wanaweka vyeti vyao badala ya kuweka cheti sasa wanaajiriwa wafamasia kwenye eneo husika, tutaondokana na matatizo kama hayo. Hii ni kwa sababu kwenye *site* atakuwepo mtaalamu wa dawa, atakuwepo na nesi ambaye ana utaalamu huo wa kuuza dawa na mambo mengine ambayo yatazuia hicho. Kwa sababu, hata kama ni duka la chini kabisa ni lazima anayeuza pale anajua dawa. Kwa hiyo, hayo matatizo yanadhibitika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara hiyohiyo, Mheshimiwa Asia Abdulkarim.

Na. 132

**Kutoa Bima ya Afya kwa wafungwa**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kutoa bima za afya kwa wafungwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdulkarim Halamga, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa hakuna mpango mahususi wa bima ya afya kwa kundi la wafungwa. Katika kuhakikisha kuwa wafungwa wanapata haki yao ya msingi ya kupata huduma ya afya, Serikali imeweka utaratibu maalum wa kutoa huduma za matibabu kwa wafungwa katika magereza mbalimbali nchini kupitia vituo vya kutolea huduma za afya vya serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakamilisha Muswada wa Bima ya Afya kwa Wote, ambapo utakapokamilika utakuwa suluhisho la upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi yote ya kijamii wakiwemo wafungwa. Naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Asia.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kutoa huduma ya afya bure kwa wafungwa, lakini kwa kuwa Waziri amekiri kwamba, suluhisho la matatizo yote ya afya ni kupitishwa kwa muswada wa bima ya afya;

Je, changamoto wanazokutananazo kwa sasa wafungwa juu ya huduma za afya, Serikali haioni haja ya kukaa na kupitia utaratibu ambao imeuweka kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, lakini nianze kwa kusema kwanza ni wakati muafaka sisi Wabunge na sisi viongozi wote kujirudi na kutafakari kwa makini muswada wa bima ya afya kwa watu wote, moja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwa leo tu ukienda pale Mirembe wako wafungwa wa namna hiyo zaidi ya 270 na wanahudumiwa na wanapewa tiba bure na Serikali. Lakini pia, kweli kumekuwepo maeneo kama unavyosema Mheshimiwa Mbunge ambayo wakati mwingine akifika mfungwa anatakiwa kupewa huduma, anapewa zote bure, lakini kuna dawa inakosekana, saa nyingine ndugu anatafutwa kununua hiyo dawa iliyokosekana. Waziri wa Afya ameshatoa maelekezo kuhakikisha kwa kutumia watu wetu wa ustawi wa jamii mfungwa huyo anapitia kwenye utaratibu hata kwenye mapato ya ndani mfungwa huyo anatafutiwa dawa wakati tukishirikisna na Wizara ya Mambo ya Ndani kuona tunafanya nini, ili hilo tatizo lisiwepo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tendega.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Wakati tunasubiri Musawada wa Bima ya Afya kwa wote.

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba, watu wenye ulemavu wanapata bima ya afya wasio na uwezo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kumuomba Mbunge mimi nayeye ili tusisubiri muswada wa bima ya afya, tuusukume kwa pamoja tuhakikishe unatokea. Lakini pia, ukweli ni kwamba kila hospitali yetu anakuwepo mtu wa ustawi wa jamii. Kazi yake

ni kuhakikisha watu wa namna hiyo wanashughulikiwa na wanapata huduma. Hao walemavu hakuna ambaye hana uwezo ambaye amekosa huduma.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea, Wizara ya Maji, Mheshimiwa Kimei.

Na. 133

**Gharama za kuwaunganishia maji wananchi – vijijini**

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI** aliuliza: -

Je, kwa nini Serikali isiingize gharama za mita za maji kwenye vitabu vyao vya fedha badala ya kuweka pale inapounganishwa maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, Mbunge wa Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Serikali ni kuhakikisha kunakuwa na dira za maji na kuwafungia wateja wanaoomba huduma za maji. Kwa kutambua changamoto za uunganishaji wa maji kwa wateja hususani kwenye suala la dira, Serikali imeandaa mwongozo wa ugharamiaji wa maunganisho ya maji vijijini ambao pia utajumuisha suala la dira za maji kuwa ni sehemu ya gharama za Serikali. Mwongozo huo utaanza kutumika mwezi Julai, 2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kimei.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naomba niulize Maswali mawili madogo tu: -

(i) Je, Serikali inaweza ikatudokeza kidogo kitu gani tutegemee kutokana na huo mwongozo?

(ii) Kwa vile Serikali imeweza kutoa ruzuku kwa maunganisho ya umeme, ni nini kinazuwia kutoa ruzuku kwa maunganisho ya maji ilhali tunajua maji ni uhai?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sijamuelewa, sijayapata maswali yake.

**NAIBU SPIKA:** Anaomba uulize tena swali.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza na ninauliza, je, tutegemee nini kutokana na huo mwongozo ambao unasema utakuja kutumika mwezi Julai?

Mheshimiwa Naibu Spika, na la pili; kwa vile Serikali itatoa ruzuku kwa maunganisho ya umeme, 27,000 vijijini; je, ni kitu gani kinazuwia Serikali kutoa ruzuku kwa maunganisho ya maji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge.

Swali la kwanza, kwa nini tunashindwa kutumia ruzuku kwenye maunganisho ya maji; hili suala naomba nilichukue tuweze kulifanyia kazi. Vilevile swali lake la kwanza naomba niwe nimelipokea nitalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuwena Bushiri, jiandae Mheshimiwa Profesa.

**MHE. ZUENA A. BUSHIRI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakamilisha mradi wa maji wa Njoro II, Rombo, ili kuwatua akinamama wa Rombo ndoo kichwani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zuena Bushiri, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu tunaendelea na utekelezaji wake; na kadiri tunavyopata fedha, Mheshimiwa Mbunge wewe ni shahidi, tunaendelea kupeleka fedha ili mradi huu ukamilike, kwa sababu lengo la Serikali ni kuona akina mama tunawatua ndoo kichwani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Profesa. Jiandae Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, ni lini Serikali itakuja na bei elekezi ya kuunganisha maji nchi nzima kama ilivyo kwenye umeme?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge,

Profesa Ndakidemi kuhusu bei elekezi nchi nzima kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uunganishaji wa maji tunazingatia umbali kwa sababu ya mabomba na miundombinu ambayo inatumika. Tunaangalia kutokea kwenye *main line* kuja kwa wewe mtumiaji pale ulipo ndivyo ambavyo gharama inakwenda.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mtemvu.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona. Kwa kuwa wananchi wa Kibamba wanayo shukrani ya kukamilisha matenki ya Tegeta A – Goba na Mshikamano – Mbezi na mtaa Msumi hauna maji toka kupata uhuru.

Je, ni lini Serikali mtapeleka miundombinu ya kutosha, ili Mtaa huu wa Msumi, Kata ya Mbezi kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mtemvu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari Wizara tumeagiza vifaa vya kuhakikisha mradi huu na miradi yote ya eneo lile la jimbo lake tunakwenda kuikamilisha. Tayari tumeshagharamia miundombinu ya matenki makubwa kwa hiyo sasa usambazaji ndio unaofuata.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Raymond.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa wananchi wengi wanalalamikia sana bili kubwa za maji pale ambapo hata hawatumii maji nikiwemo mimi, ilhali hatupo hapa Dodoma naletewa bili kubwa. Ni lini sasa Wizara ya maji italepa *prepaid meters* kwa wengi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, *prepaid meters* tunaendelea kufunga maeneo mbalimbali. Kwa hiyo naomba niseme tu Mheshimiwa Mbunge, tuendelee kuwasiliana, hata wewe ukihitaji leo unaweza ukafungiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile bili kubwa hizi za maji Waheshimiwa Wabunge pamoja na wananchi wote naomba niseme kwamba, tuangalie miundombinu yetu. Wakati fulani ni wewe mhusika peke yako ndiye unaepata bili kubwa kwa sababu, labda mita yako hapo nje inapitisha hewa au kuna tatizo la uvujaji. Kwa hiyo hizi bili kubwa naomba tutoe taarifa kwa mafundi wetu, ili tuweze kuzidhibiti.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Edwin Swale.

Na. 134

**Ujenzi wa barabara ya Kibena hadi Madeke**

**MHE. EDWIN E. SWALLE** aliuliza:-

Je, lini ujenzi wa barabara ya Kibena Stop – Lupembe hadi Madeke kwa kiwango cha lami utaanza?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imepanga kuanza ujenzi wa Barabara ya Kibena – Lupembe hadi Madeke yenye km 126 kwa awamu, ambapo katika mwaka wa fedha 2023/2024 itaanza ujenzi wa km 25 kwa sehemu ya kutoka Kibena hadi Nyombo. Kwa sasa Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* wanaendelea kuandaa nyaraka kwa ajili ya kutangaza zabuni. Zabuni zinatarajiwa kutangazwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2023.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kulingana na upatikanaji wa fedha hadi ikamilike yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Swalle.

**MHE. EDWIN E. SWALLE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Kwa kuwa barabara hii ina ahadi ya muda mrefu; Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari baada ya Bunge hili kwenda Jimboni Lupembe kuwaambia wananchi juu ya ahadi hii nzuri ya Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, wananchi wa Nyombo, Kidegembye, Matembwe, Barazani, Madeke na Mfiriga nyumba zao zimewekwa X tangu mwaka 2014. Ni upi mpango wa Serikali sasa kuwalipa fidia wananchi hawa kwa ajili ya ujenzi wa barabara hii? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Edwin Enosy Swalle, Mbunge wa Lupembe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hiyo nimeshaitembelea. Na kwa kuwa tunaenda kuanza niko tayari baada ya kikao hiki cha Bunge kwenda jimboni kwa Mheshimiwa Mbunge na kuweza kuongea na wananchi, kuwaeleza nini tutakachokifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tulikuwa tumefanya tathmini muda na tayari tumeshamu-*engage consultant* kwa ajili ya kuhuisha ule uhakiki uliofanyika, ili sasa tuweze kupata taarifa za sasa kwa ajili ya kuwalipa fidia wananchi hawa ambao wote waliwekewa alama za "X" ili tuanze ujenzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi, barabara inayotoka Handeni kwenda Songe na Kiteto ni siku ya pili sasa hivi haipitiki kutokana na na mvua zinazonyesha, na shughuli zote za uchumi zimesimama. Je, nini kauli ya Serikali juu ya barabara hiyo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niwape pole wananchi wa Kilindi kwa adha wanayoipata kwa sababu ya changamoto ya mvua. Napenda nitumie nafasi hii kumuagiza Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tanga aweze kufika maeneo yote ambayo yameathirika na kuweza kurejesha mawasiliano kwa muda, na pale ambapo changamoto itakuwa ni kubwa, basi aweze kuwasiliana na *TANROADS* Makao Makuu kwa ajili ya kutoa msaada mkubwa zaidi, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kassinge.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa upembuzi na usanifu wa barabara ya kutoka Kiranjeranje – Makangaga – Nakiu – Nanjirinji mpaka Ruangwa umekamilika, lini Serikali itajenga barabara hii kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Kassinge, Mbunge wa Kilwa Kusini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshafanya kama alivyosema upembuzi yakinifu, na yote hayo ni maandalizi ya kuijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tuna mpango wa kuijenga hii barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kiranjeranje hadi Ruangwa kwa kadri fedha itakavyopatikana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mzanva, nimemuita Mheshimiwa Mnzava.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naitwa Nicodemas Henry Maganga.

**NAIBU SPIKA:** Hapana bwana sikujua, Mheshimiwa Maganga okay.

**MHE. NICODEMAS H. MAGANGA:** Naomba kumuuliza Naibu Waziri; barabara itokayo Masumbwe – Lugunga kuelekea Geita, ni lini itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Maganga, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ipo kwenye mpango wa *RICE,* na sasa hivi kinachoandaliwa ni *document tender* kwa ajili ya kuitangaza ili barabara hii iweze kuanza kujengwa kwa kiwango cha lami kwa maeneo ambayo yameainishwa. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Twaha.

**MHE. TWAHA A. MPEMBENWE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya Bungu – Nyamisati imekuwa kilio cha muda mrefu sana kwa wananchi wa Jimbo la Kibiti; je, ni lini Serikali mtaitengeneza barabara hii katika kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la

nyongeza la Mheshimiwa Twaha Mpembenwe, Mbunge wa Kibiti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii tayari tumeshakamilisha usanifu wa kina na Serikali inaendelea kutafuta fedha ili tuweze kuijenga barabara hii yote kwa kiwango cha lami kuanzia Bungu mpaka Nyamisati. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyohiyo; Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava.

Na. 135

**Hitaji la ujenzi wa barabara ya Kahama – Solwa hadi Mwanza**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanza na kukamilisha ujenzi wa barabara ya Kahama – Solwa hadi Mwanza kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeanza ujenzi wa barabara ya Kahama – Solwa hadi Mwanza kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha ambapo kipande cha kilometa 5.65 kuanzia Kahama kuelekea Solwa pamoja na kipande cha mita 540 katika Mji Mdogo wa Bulige tayari imejengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga jumla ya shilingi milioni 750.62 kwa ajili ya ujenzi wa kilometa 1.2 kati ya Solwa na Bulige ambapo mkandarasi tayari amepatikana na amekabidhiwa mradi ili kuanza kazi. Kazi imepangwa kukamilika mwezi Septemba, 2023.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea na ujenzi wa barabara hii kwa awamu hadi kukamilika yote kulingana na upatikanaji wa fedha, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, na pia namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali imekwisha kutenga fedha kwa mwaka wa fedha 2022/2023, je, ni lini Serikali itatoa hizo fedha ili ujenzi wa barabara uendelee?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa mkandarasi amekwisha kupatikana, na Naibu Waziri amesema kwamba Septemba ile kazi itakabidhiwa. Je, kwa kuwa mkandarasi amepatikana, ni lini ataanza hiyo kazi ili Septemba aikabidhi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mkandarasi akishakabidhiwa anachofanya ni maandalizi ya ujenzi, na kwa hiyo kwa kuwa tumeshamkabidhi, na tumekubaliana lini atamaliza kazi,

mkandarasi yuko *site* kwa maana ya kufanya maandalizi, na mwezi Septemba tunategemea atakuwa amekamilisha hiyo kazi, na kadri Serikali itakavyoendelea kupata fedha, barabara hii tuna uhakika itakamilishwa yote, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ni lini Serikali itajenga barabara kwa kiwango cha lami kuanzia Kazegunga – Mahembe – Kitanga – Kinazi mpaka Buhigwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Josephine Genzabuke, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara aliyoitaja ya Mahembe – Buhigwe – Kitanga ni barabara ya mkoa ambayo tayari tumeshakamilisha kufanya usanifu na sasa tunaendelea kumlipa huyo *consultant* na baada ya hapo tutaanza kufanya maandalizi kuijenga barabara hiyo kwa kiwango cha lami, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, natambua kwamba ujenzi wa barabara ya Kisorya – Nyamswa – Bunda tayari umeshafika Nyamswa, lakini bado ujenzi unatakiwa uendelee na imekomea pale Makongoro Sekondari na inatakiwa ifike mpaka Isenye. Je, ni lini sasa ujenzi huo utaendelea kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nielewe kipande ambacho Mheshimiwa Mbunge anasema kwamba kimebaki ili niweze kumjibu vizuri.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

Haukusikia swali Mheshimiwa Waziri? Haya, rudia swali lako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema tayari ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami umeshatoka Kisorya, umeshapita Bunda kwenda Nyamswa, sasa umekomea pale Nyamswa, unatakiwa uendelee kutoka pale kuanzia Makongoro Sekondari kwenda Isenye na kuendelea; sasa ni lini huko utaendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ester Bulaya, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ukishafika Nyamswa unapita kwenye T, aidha uende Mjini Musoma ama uende upande wa Nata. Na upande wa Nata ndiyo Isenye ambapo tayari kuna mkandarasi ambaye ameshajenga kutoka Makutano – Sanzate na Sanzate kwenda Nata tayari mkandarasi yuko *site,* nadhani kuna eneo Isenye pale tayari wameshajenga. Na wiki kama tatu nimekuwepo pale wakiwa wanaomba baada ya kuinua tuta wanahitaji kurekebisha maji pale, tumeshawarekebishia. Kwa hiyo, hiyo barabara iko kwenye ujenzi na mkandarasi yuko *site* (kilometa 40).

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza.

Je, ni lini Serikali itaanza kujenga barabara ya Mbuguni inayounganisha Mikoa ya Arusha na Manyara kwa kiwango cha lami?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (MHE. ENG. GODFREY K. MSONGWE):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, Mbunge Arumeru Mashariki, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ilishaahidiwa kujengwa kwa kiwango cha lami, na tayari tumeshakamilisha usanifu. Sasa hivi Serikali inaendelea kuweka mipango ili tuweze kuijenga kwa kiwango cha lami. Naomba Mheshimiwa Mbunge avute subira tuangalie kwenye bajeti tunayokwenda kuileta mbele yenu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yamekwisha na muda wetu umekwisha.

Matangazo ya wageni; wageni waliopo Jukwaa la Spika ni wageni wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambao ni viongozi wakuu na wakuu wa taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo; Ndugu Mululi Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Ndugu Juma Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ndugu Xavier Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. *(Makofi)*

Wengine ni Mheshimiwa Jaji Sivangilwa Mwangesi, Kamishna wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ndugu Ashery Mwanda, Mwakilishi wa Ofisi ya Rais; *CP* Salum Hamduni, Mkurugenzi Mkuu Taasisi ya TAKUKURU; na Ndugu Ladislaus Mwamanga, Mkurugenzi Mtendaji Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Kadari Singo, Mtendaji Mkuu Taasisi ya UONGOZI; Kepteni Budodi Budodi, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu Wakala wa Ndege za Serikali; Ndugu Firimin Msiangi, Mkurugenzi Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; Ndugu Hassan Kitenge, Katibu wa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Wengine ni Dkt. Ernest Mabonesho, Kaimu Mkuu wa Chuo na Afisa Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania; *Engineer* Benedict Ndomba, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Serikali Mtandao *(eGA);* Ndugu Mathew Kirama, Katibu wa Tume ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka Jimboni kwake Chalinze; Ndugu Arafa Mohamed Kikwete, mke wake; Ndugu Godbless Naibala, Mwenyekiti wa CCM Kata ya Lugoba; Mheshimiwa Debora Rashid, Diwani wa Viti Maalum na Ndugu Agness Frank, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Wilaya CCM. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni 76 wa Mheshimiwa Innocent Bashungwa, Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa ambao ni wanafunzi wa vyuo vikuu na vya kati vilivyopo Mkoa wa Dodoma, wanaotokea Karagwe, Mkoani Kagera, karibuni. *(Makofi)*

Wageni 50 wa Mheshimiwa Anthonty Mavunde, Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni waratibu wa *Dodoma Gala* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wengine tisa wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni *Modest Queens of Tanzania* kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni 60 wa Mheshimiwa Cecilia Paresso ambao ni wachungaji na vijana kutoka makanisa ya kiinjili yenye kujishughulisha na huduma ya mtoto na kijana kutoka klasta ya Monduli, Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mchungaji Wilbert Mollel. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Lucy Sabu ambaye ni Katibu wa UVCCM kutoka Maswa, Ndugu Victor Leopord. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ester Bulaya ambaye ni mtoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Brighton Babile.

Wageni watatu wa Mheshimiwa Mwakagenda ambao ni marafiki zake kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Ghati Chomete ambaye ni mdogo wake kutoka Mkoani Mara, Ndugu Sunzi Chambili. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha *UDOM*, Ndugu David Ntezidyo na Ndugu Irine Vithalis. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Sylvia Sigula ambao ni wanafunzi kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Antipas Mgungusi ambao ni mawakala wa pembejeo kutoka Mkoa wa Morogoro; karibu. *(Makofi)*

Wageni nane wa Mheshimiwa Daniel Sillo kutoka Babati Vijijini Mkoa wa Manyara. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; mwanafunzo kutoka Chuo cha Diplomasia cha Jijini Dar es Salaam, Ndugu Kiiza Alphonce Kazige. *(Makofi)*

Pia wapo wageni watatu kutoka *Dar es Salaam Ceramic Center. (Makofi)*

Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wapo katika viwanja vya Bunge kwa ajili ya kutoa huduma zinazohusu sekta za ardhi na nyuma kwa Wabunge na watumishi. Huduma hiyo imeanza tarehe 17 Aprili na itaendelea hadi tarehe 30 Juni. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kutumia fursa hiyo muhimu.

Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## KAULI ZA MAWAZIRI

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kuna kauli ya Waziri, namwita sasa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, na naomba kutoa taarifa kwa Bunge kuhusu hali ya amani na usalama nchini Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 15 April, 2023, nchini Sudan, kulizuka mapigano kati vikosi vya Serikali *(Sudan Armed Forces)* na Vikosi vya Msaada *(Rapid Support Forces),* katika Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum na katika maeneo mengine nchini humo. Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa

mapigano hayo yamesababisha vifo 185, majeruhi zaidi ya 1,000, na uharibifu wa mali, ikiwa ni pamoja na ndege. Aidha, mapigano hayo yamechangia kurudisha nyuma jitihada zinazoendelea za kutafuta amani Nchini Sudan.

Mheshimiwa Naibu Spika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasikitishwa na hali ya kuzorota kwa amani na usalama, na imeendelea kufuatilia hali hiyo. Kama Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono tamko lililotolewa na Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, katika Mkutano wake uliofanyika tarehe 16 Aprili, 2023, kulaani mapigano yanayoendelea nchini Sudan, na inatoa wito kwa pande zote mbili katika mgogoro huo, kusitisha mapigano yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania inazitaka pande mbili zinazohasimiana kutatua mgogoro huo kwa njia ya amani na usalama, huku zikihakikisha mahitaji ya kibinadamu, usalama na ustawi wa raia wa Sudan na raia toka nchi nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na Ubalozi wetu uliopo Khartoum, ili kujua hali inavyoendelea. Tunao Watanzania takriban 210 Nchini Sudan, ambapo 171 kati ya hao ni wanafunzi walioko huko kwa masomo, na wengine ni maafisa Ubalozi, na raia wengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa hakuna Mtanzania aliyeripotiwa kuathiriwa na mapigano hayo. Namshukuru sana Mheshimiwa Balozi wetu Silima Kombo Haji, kwa kuhakikisha usalama wa raia wetu nchini humo na raia wote kwa uvumilivu mkubwa ambao wameuonesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inawahakikishia Watanzania kuwa inachukua hatua stahiki kwa kushirikiana

na nchi jirani, Jumuiya za Kikanda, Umoja wa Afrika, Umoja wa Mataifa na taasisi nyingine za kimataifa ili kuhakikisha kuwa Watanzania waliopo nchini humo na raia wengine wanakuwa salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeendelea na juhudi hizi tangu haya yalipojitokeza, juhudi hizi zimewezesha mapigano hayo kusitishwa kwa muda kwa masaa 24 kuanzia jana tarehe 18 Aprili 2023 saa kumi jioni ili kutoa fursa za mahitaji ya kibinadamu.

Aidha, kufuatia juhudi hizi zinazoendelea upo uwezekano na mwelekeo uliopo ni kusitisha mapigano na kuruhusu njia za kutatua mgogoro huu kwa amani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufuatilia na kuandaa mpango wa kuwachukua raia wa Tanzania *(evacuation)* kadri itakavyohitajika. Serikali inatoa pole kwa wananchi wa Sudan na raia wengine na wote walioathirika na kuzorota na hali ya amani nchini humo kwa namna moja au nyingine, tunaendelea kuzitaka pande zote mbili kusitisha mapigano na kurudi kwenye meza ya mazungumzo kwa ustawi wa Sudan, Afrika na Dunia kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI- KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Hoja za Serikali, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayohusu Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, sasa naomba Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2022/2023 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24 ya Ofisi ya Rais, Ikulu - Fungu Na. 20 na Fungu Na. 30; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – Fungu Na. 33; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Fungu 32); Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - Fungu 67; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma - Fungu Na. 94; na Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa - Fungu Na. 04.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyoada naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa wema na huruma ambae ametuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema, amani na utulivu hasa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kwa kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayochangia katika kujenga

ustawi wa Taifa. Pia, tunamshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika kipindi hiki cha Mkutano wa Kumi na Moja wa Bunge la Kumi na Mbili kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na kutafakari mipango ijayo katika kuyafikia malengo ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwa kuendelea kunipa dhamana hii ya kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba sera, sheria, kanuni, taratibu na miongozo mbalimbali ya usimamizi wa Utumishi wa Umma inazingatiwa na watumishi wa umma wanawajibika na kuwa wasikivu wanapotoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako Tukufu na Watanzania wote kuwa nitaendelea kutumia uwezo wangu wote ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa na kuhakikisha kwamba Bajeti hii inasimamiwa vema na kutekelezwa ipasavyo. Ni dhahiri kwamba mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yametokana na maono makubwa ya Rais katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Tunajivunia na kumshukuru Mungu kwa kuwa na kiongozi mwenye maono chanya kwa mustakabali wa Taifa letu. Naomba tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya thabiti, hekima, busara na ustahimilivu katika kuliongoza Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, niruhusu tena nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza kipindi cha miaka miwili akiwa ameshika hatamu kwa

mafanikio makubwa yanayojidhihirisha kupitia kazi mbalimbali zinazoendelea katika sekta zote. Ni ukweli usiopingika kwamba Rais wetu amekuwa ni mfano wa kuigwa Kitaifa na Kimataifa kwa kuhakikisha kuwa demokrasia yetu inazidi kustawi na Serikali inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na maovu katika jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika,napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyochapa kazi na kumsaidia Rais kutekeleza majukumu yake katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake za dhati za kuimarisha utendaji wenye malengo ya kuleta maendeleo Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia utendaji kazi za kila siku za Serikali na uwajibikaji Serikali ambapo ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kukupongeza wewe binafsi pamoja na Mheshimiwa Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge lako Tukufu kwa umahiri mkubwa unaodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu, hakika mmesimama imara katika kuusimamia Muhimili huu muhimu katika kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa na Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu zaidi. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza vyema vikao vya Bunge letu, ni dhahiri kuwa

mmetendea haki nafasi zenu na mmekuwa na mchango mkubwa katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza na kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Madaba na Makamu wake Mheshimiwa Florent Kyombo, Mbunge wa Nkenge kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Ofisi yangu kwa mwaka 2023/2024. Naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya mapato na matumizi ya mwaka 2022/2023 na makadirio ya mapato na matumizi ya mwaka 2023/2024. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya Awamu ya Sita kwa kuendelea kupewa dhamana ya kuwatumikia Watanzania, kwa kusimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Maelekezo ya Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tuendelee kushirikiana kwa pamoja katika kulijenga Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kwa kuaminiwa na kupewa dhamana na Mheshimiwa Rais kuhudumu katika nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Dkt. Moses Kusiluka -Katibu Mkuu Kiongozi, Ndugu Mululi Mahendeka - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu, Ndugu Juma S. Mkomi - Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma

na Utawala Bora, Ndugu Xavier M. Daudi - Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais, Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiriwa na Watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:-

Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Norway, Finland, Uswisi, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vilevile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia *OFID-OPEC Fund for International Development, Foreign Commonwealth Development Office, KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP*, Jumuiya ya Madola, *JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund*, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa *(IMF)* na *Bill and Melinda Gates Foundation.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapokuwa nikitekeleza majukumu ya kazi za Serikali. Kwa moyo wa dhati naishukuru familia yangu kwa ushirikiano

wanaonipa wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kitaifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, viongozi na Watumishi wa Umma kutokana na majanga mbalimbali yaliyosababisha uharibifu wa mali na kukatisha uhai kwa Watanzania wenzetu ikiwemo ajali za moto katika Hifadhi ya Taifa Mlima Kilimanjaro na Mikoa mbalimbali, ajali ya ndege ya Kampuni ya *Precision Air* Mkoani Kagera – Bukoba, mvua zilizoambatana na upepo mkali katika mikoa ya Mtwara (Tandahimba), Songwe (Momba), Mbeya (Rungwe), Dodoma (Mpwapwa) na upepo mkali katika Mkoa wa Rukwa (Sumbawanga), mafuriko Mkoa wa Mbeya (Jiji la Mbeya) na mlipuko wa ugonjwa wa *Marburg* hivi karibuni katika Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, majanga haya yamesababisha vifo kwa Watanzania wenzetu, uharibifu wa nyumba, miundombinu mbalimbali na vitega uchumi vikiwemo mashamba na mifugo. Kwa nafasi hii muhimu, nawapa pole Wabunge wenzangu wanaotoka katika maeneo yaliyokumbwa na kadhia hizo. Salamu za pole ziwafikie viongozi wa Mikoa husika na Watanzania wenzangu walioathirika kwa namna moja au nyingine. Kwa waliotangulia mbele za haki, tunamuomba Mwenyezi Mungu awarehemu na kuwapumzisha kwa amani. Aidha, Watanzania walioathirika na afya hazijarejea, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awaponye ili warejee kwenye majukumu ya kustawisha maisha yao na Taifa pia. Natoa rai kwa Watumishi wa Umma wanaohusika katika kutoka huduma kwa waathirika, kuendelea kujitoa kwa moyo kuhakikisha Watanzania wenzetu hawa wanarejea katika shughuli zao za kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2022/2023 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, maombi

ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayowezesha Ofisi yangu kutimiza majukumu yake. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa mwaka 2022/2023 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya mpango na bajeti kwa mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha 2022/23. Mpango bajeti kwa kipindi cha mwaka 2022/2023 ulitekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya Kitaifa ambayo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuhutubia Bunge la 12, Tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na maelekezo yake mbalimbali. Aidha, utekelezaji umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 - 2025/2026), pia unatokana na Tanzania ambao unataka kwamba Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - Ikulu na Taasisi zake. Katika mwaka 2022/2023, Fungu Na. 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa Shilingi Bilioni 29.8 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2023 Shilingi Bilioni 21.9 sawa na asilimia 73.3 zilipokelewa na kutumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake mwaka 2022/2023, Fungu Na. 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inayojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa shilingi bilioni 741.29 kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 577.2 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 164.09 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 shilingi bilioni 596 sawa na asilimia 80.5 zilipokelewa na kutumika ambapo shilingi bilioni 453.94 ni

Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 142.85 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, yafuatayo ni maelezo ya matumizi kwa kila taasisi: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na nchi nzima kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kazi zifuatazo zilitekelezwa na kazi hizi tumezieleza katika ukurasa wa 08 – 10 wa hotuba yangu ambayo yote ipo kwenye Vishikwambi na Wabunge wote wanaweza kufuatilia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa – TAKUKURU; katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kutokomeza rushwa nchini na kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imetekeleza kazi zifuatazo: -

i. Miradi ya maendeleo 896 yenye thamani ya shilingi trilioni 6.93 ilifuatiliwa ambapo miradi 137 yenye thamani ya shilingi bilioni 55.48 ilibainika kuwa na kasoro mbalimbali. Kati ya miradi yenye kasoro, miradi 26 elimu ilitolewa kwa watekelezaji kuhusu usimamizi wa miradi, miradi 20 ilifanyiwa udhibiti ili ikamilike kama ilivyopangwa na miradi 91 ilianzishiwa uchunguzi ili hatua stahiki ziweze kuchukuliwa.

ii. Mpango wa TAKUKURU RAFIKI unaolenga kuongeza wigo wa ushiriki wa wadau katika kuzuia na kupambana na rushwa umezinduliwa na kuanza kutekelezwa katika Mikoa na Wilaya nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo ya majukumu hayo yaliyofanyika yameelezwa katika ukurasa wa 10 -15 wa hotuba yangu ndefu iliyopo kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uongozi; katika kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Taasisi ya Uongozi ilitekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Utafiti kuhusu tathmini ya athari za kimazingira ikiambatana na tathmini ya athari za haki za binadamu katika ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* kipande cha tatu na nne kutoka Makutupora hadi Isaka kupitia Tabora umefanyika.

(ii) Tawasifu inayoelezea maisha ya Hayati Edward Moringe Sokoine, Waziri Mkuu Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuandikwa. Aidha, Kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa kilichotafsiriwa katika lugha ya kiswahili kilichapishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 15 na ukurasa wa 17 wa hotuba yangu.

(a) Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Mashamba 7,825 ya wakulima yamerasimishwa katika Halmashauri za Iramba na Chemba ambapo jumla ya Hati Miliki 7,111 zimeandaliwa na Hati Miliki 5,316 kutolewa kwa wananchi.

(ii) Mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara yametolewa kwa wafanyabiashara 3,827 katika Halmashauri za Kibaha 1,665 na Halmashauri ya Temeke 1,956.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya shughuli zilizofanyika za MKURABITA yanapatikana ukurasa wa 17 hadi ukurasa wa 19 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF)*, umetekeleza kazi zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mosi, uhakiki wa awali wa kaya umefanyika katika Mamlaka za Utekelezaji 186. Jumla ya kaya 713,350 zilihakikiwa ambapo kaya 670,566 zilikidhi vigezo vya uhakiki wa awali wa kuendelea kuwepo katika Kipindi cha Pili cha Mpango na zaidi ya kaya 156,000 zimeboreka kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ruzuku ya Shilingi bilioni 218 ilihawilishwa kwa kaya 1,371,916 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika Kipindi cha Pili cha Mpango kutoka maeneo ya utekelezaji 186 kwa Tanzania Bara, Pemba na Unguja kwa Zanzibar kufikia Machi, 2023. Jumla ya miradi 14,236 iliibuliwa na jamii na kuanza kutekelezwa katika mamlaka za utekelezaji 123 ambapo kaya za walengwa 660,000 zimeshiriki katika kutekeleza miradi hiyo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 40.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi ya majukumu na kazi zilizofanywa na *TASAF* kwa kipindi hicho yanapatikana katika ukurasa wa 19 hadi 21.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Wakala ya Ndege za Serikali ilitekeleza kazi zifuatazo:-

Mosi, huduma ya usafiri wa anga zimeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa.

Pili, matengenezo makubwa ya ndege aina ya *Gulfstream* 550 inayohudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa yamekamilika.

Tatu, wanaanga 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ili kuhuisha leseni zao. Maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 22 hadi 23.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2022/2023, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa shilingi 12,730,049,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 9.26 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.47 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopokelewa na kutumika ni Shilingi bilioni 6.7. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 6.04 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 659.8 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza kazi zifuatazo: -

Mosi, hadi kufikia Desemba, 2022, matamko ya viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni yapatayo 14,941 kati ya matarajio 15,893 yamepokelewa ikiwa ni sawa na asimilia 94.

Pili, uhakiki kuhusu rasilimali, madeni na mgongano wa maslahi ulifanyika kwa jumla ya viongozi 592. Kati yao 8% walibainika kuwa na dosari katika matamko, na 4% walibainika kuwa na mgongano wa masilahi. Maelezo zaidi yanapatikana Ukurasa wa 23 hadi 24 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu Na. 32 inayojumuisha Mamlaka na Taasisi zilizo chini yake ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 47.6 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 39.54 ni matumizi ya kawaida sawa na asilimia 83.05 ya bajeti iliyoidhinishwa na shilingi bilioni 8.07 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 16.95 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2023 shilingi bilioni 41.3 sawa na asilimia 86.74 ya bajeti iliyoidhinishwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 34.67 ni matumizi ya kawaida na Shilingi bilioni 6.6 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo: -

Mosi, Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma *(PEPMIS* na *PIPMIS)* umeendelea kuimarishwa. Aidha, zoezi la utekelezaji wa mfumo kwa majiribio katika taasisi 12 limefanyika kwa lengo la kubaini kama mfumo unakidhi mahitaji ya taasisi tumizi.

Pili, mfumo wa taarifa za kiutumihi na Mishahara *(HCMIS)* umekamilika na *Module* ya *Utumishi Portal* yenye huduma za kielektroniki za uhamisho wa watumishi, mikopo ya watumishi, taarifa binafsi za watumishi na tati za malipo ya mishahara imeboreshwa.

Tatu, Mkakati wa Serikali wa Kujilinda na Majanga ya Kimtandao wa mwaka 2022 umeandaliwa na kukamilika. Mkakati huu unalenga kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi wa usalama wa Serikali mtandao.

Nne, Taasisi 433 kati ya 522 zimewezeshwa kutumia mfumo wa kiutumishi na mishahara katika kuandaa Ikama, kulipa mishahara, kusafisha taarifa na kubadilisha kada.

Tano, Serikali imelipa madai malimbikizo ya mishahara ya watumishi 14,398 yenye jumla ya Shilingi bilioni 25.6 hadi Machi 2023. Maelezo zaidi ya eneo hili na Shughuli zilizofanyika yameoneshwa katika ukurasa (25 – 31) wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na: Watumishi wa umma wapya 1,739 walipatiwa Mafunzo ya awali na watumishi 321 wamejengewa uwezo katika utaalamu wa fani za Menejimenti na Utumishi wa Umma katika ngazi za kitaifa na Kimataifa. Aidha, ushauri wa Kitaalamu katika maeneo tisa umetolewa ili kuwezesha watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 31 - 32 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Serikali Mtandao (*e-GA),* matokeo ya utafiti wa Benki ya Dunia *(World Bank)* ya hivi karibuni ya Ulinganifu baina ya nchi katika Faharasa ya Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia *(Government Technical Maturity Index)* yamebainisha kuwa Tanzania imeshika moja ya nafasi za juu katika matumizi ya Serikali Mtandao miongoni mwa nchi zilizoshindanishwa pamoja na nchi nyingine za ukanda wake. Matokeo hayo yamezidi kubainisha kuwa kuna maeneo ambayo kwa sasa Tanzania inachuana kwa ukaribu na nchi vinara kama vile China, Israel na Ireland. Aidha, katika Bara la Afrika, Tanzania imeshika nafasi ya tatu ikizikaribia Misri pamoja na Mauritius na kuwa kinara katika ukanda wa Afrika Mashariki. Mafanikio

haya yametokana utekelezaji wa sera mbalimbali, miongozo pamoja na mikakati ya matumizi ya TEHAMA nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mamlaka ya Serikali Mtandao imetekeleza Shuguli zifuatazo:-

Mosi, ujenzi wa Mfumo Maalum wa Kuwezesha Mifumo ya Serikali Kusomana na Kubadilishana Taarifa *(Government Enterprise Service Bus - GovESB)* umekamilika ambapo mifumo 55 ya Taasisi 50 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa.

Pili, miundombinu ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini *(GePG)* umeboreshwa ambapo vituo vya kutolea huduma na taasisi mpya 100 zimeunganishwa katika mfumo huo.

Tatu, Taasisi za Umma 134 zimewezeshwa kuhifadhi mifumo na taarifa kwenye Vituo Vikuu vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya Serikali *(Government Data Centres)* vyenye usalama na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali. Maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 32 – 36.

Mheshimiwa Naibu Spika,katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, *Watumishi Housing Investment* imetekeleza shughuli zifuatazo:-

Mosi, Ujenzi wa nyumba 175 umekamilika katika mradi wa nyumba 1,000 eneo la Njedengwa Jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine zikiwemo wilaya mpya. Vilevile, vitalu kadhaa vimechukuliwa na vimenunuliwa na Shirika kwa ajili ya ujenzi wa miradi mingine.

Pili, viwanja Na. 326 katika eneo la *USA RIVER* Jijini Arusha lenye ekari 112 vimepimwa kwa ajili ya kuuzwa. Kazi

ya kuweka miundombinu ya madaraja na barabara imefikia asilimia 70.

Tatu, jumla ya nyumba 52 zimejengwa kwa ajili kuwauzia watumishi wa umma na wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika Mikoa ya Dodoma eneo la Kisasa Hilltop Njedengwa nyumba 25, Dar es Salaam tisa na Morogoro 18, ambapo katika mradi wa Kisasa *Hilltop Njedengwa* nyumba zimeuzwa kwa zaidi ya asilimia 90. Maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 36 – 37.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/23, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 8.7. Kati ya fecha hizo, shilingi bilioni 5.06 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.65 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2023 shilingi bilioni 5.2 sawa na asilimia 59.8 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.13 ni Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 2.08 kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira, katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

Mosi, Matangazo ya kazi 347 yalitolewa katika tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya waajiri 319 kutoka Wizara na Taasisi za Umma; pili, Maombi ya kazi 368,672 kwa kada mbalimbali yalipokelewa na kuchambuliwa, ambapo maombi 193,391 yalikidhi sifa na waombaji waliitwa kwa ajili ya usaili na maombi 175,281 hayakukidhi sifa kwa mujibu wa miundo ya kiutawala; na tatu, saili 23 ziliratibiwa na kusimamiwa kwa niaba ya waajiri 319 ikiwa ni utekelezaji wa kibali cha ajira mpya kwa mwaka

2021/2022 ambapo jumla ya wasailiwa 10,704 wamepangiwa vituo mbalimbali vya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 37 – 40 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2022/2023, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 5.9. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 5.6 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi milioni 300 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Machi, 2023 shilingi bilioni 4.39 sawa na asilimia 73.5 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 4.09 ni Matumizi ya Kawaida na shilingi milioni 299.9 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Mosi, Mikutano mitatu kati ya minne ya kisheria ya Tume imefanyika na kutolea maamuzi rufaa 323 kati ya rufaa 604 zilizokuwa na vielelezo. Hadi kufikia Machi, 2023 kulikuwa na jumla ya rufaa 764 ambapo rufaa 50 uchambuzi wake ulikamilika, na rufaa 247 zilikuwa zinaendelea kuchambuliwa na ufuatiliaji wa vielelezo vya rufaa 144 ulikuwa unaendelea kutoka kwa mamlaka husika.

Pili, Malalamiko 108 kati ya malalamiko 168 yalishughulikiwa ambapo malalamiko 37 kati 59 yenye vielelezo yametolewa maamuzi. Aidha, malalamiko 71 yalitolewa ufafanuzi na kuhitimishwa na Sekretarieti. Malalamiko 60 yalibaki, 28 yanaendelea kuchambuliwa, na malalamiko 32 yanasubiri vielelezo kutoka kwa mamlaka

husika. Maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 40 - 43 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naiba Spika, katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya Shilingi bilioni 4.91. Kati ya fedha hizo, Shilingi bilioni 3.5 ni kwa ajili Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 1.4 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naiba Spika, hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya Shilingi bilioni 3.209 zilipokelewa ambapo kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 1.8 ni Matumizi ya Kawaida sawa na asilimia 51.63, na Shilingi bilioni 1.39 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, sawa na asilimia 99.28.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi hicho, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imetekeleza majukumu yafuatayo:-

Mosi, Jumla ya nyaraka 2,963 zimekusanywa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 kati ya 45 na Taasisi za Umma 11 kati ya 15 zilizopangwa; Pili, jumla ya nyaraka 165 za Waasisi wa Taifa (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) zimekusanywa na kuhifadhiwa. Aidha, Idara imetambua na kusajili Mnara wa Kura Tatu uliowekwa katika Soko Kuu Tabora kama kumbukumbu ya uamuzi wa busara wa kushiriki uchaguzi wa kura tatu uliofanywa na Mkutano Mkuu wa *TANU* Januari,1958.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, *Video Documentary* kuhusu maisha binafsi na harakati za kisiasa za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa mwanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Wavulana, Tabora na akiwa Mwalimu katika Shule ya Sekondari *St. Mary's* Mihayo, imeandaliwa. Pia Uwekaji wa majalada 1,873 kwenye mfumo wa kidigitali umefanyika. Maelezo zaidi katika eneo hili yanapatikana katika ukurasa wa 43 – 47.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/2024 umeandaliwa kwa kuzingatia, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026), wenye dhima ya Tanzania kuwa na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu, na pia Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge Aprili 2021; miongozo hii ni nguzo muhimu ya mpango unaotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2023/2024. Shughuli zitakazotekelezwa ni kama zifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Ikulu na taasisi zake kwa mwaka 2023/2024 ni hizi zifuatazo:-

Moja, kuendelea kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Demokrasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi.

Pili, kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu *(IMTC),* na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri.

Tatu, kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kitaifa na kimataifa hususan, masuala ya uchumi, jamii, sheria, ulinzi, usalama, na masuala mengine yote yatakayowasilishwa; na kupokea, na kupitia uchambuzi wa rufaa 300 na malalamiko 400 ya utumishi wa umma na wananchi.

Nne, kufanya ufuatiliaji kwa kuzingatia sheria na maelekezo yaliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya usimamizi na

utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 48 – 50.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa *(*TAKUKURU) imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika sekta za umma na binafsi ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo;

(ii) Pili, Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fecha;

(iii) Kuendelea kutekeleza mpango wa TAKUKURU Rafiki;

(iv) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa;

(v) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329; maelezo zaidi yanaptatikana ukurasa wa 50 hadi 52.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Uongozi, tasisi hii kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa bodi 100 za Mashirika ya Umma, taasisi za umma na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa utendaji.

(ii) Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 50 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimaliwatu. Lakini maelezo zaidi yanapatikana ukurasa wa 52 hadi 54 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *(TASAF), TASAF* imepanga kufanya shughuli zifuatazo kwa mwaka 2023/2024:-

(i) Kuhakiki zoezi la kutambua hali ya ustawi wa maisha ya kaya za walengwa wa Mpango zipatazo 380,000 iwapo zimeimarika kiuchumi kwa kutumia vigezo vya umaskini na utaratibu uliokubaliwa kitakwimu kwenye maeneo yote ya utekelezaji 186.

(ii) Kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 972,603 zinazokidhi vigezo vya Mpango; maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 54 hadi 56

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakala wa Ndege za Serikali, katika mwaka 2023/2024, Wakala ya Ndege za Serikali umepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa;

(ii) Kulipia gharama za bima za ndege pamoja na wanaanga;

(iii) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na

(iv) Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanaanga kwa ajili ya kuhuisha leseni zao. Maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 56 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais, Ikulu: Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 32,157,384,000. kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri: Fungu 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 860,186,476,000. kati ya fedha hizo, shilingi 678,193,941,000 ni matumizi ya kawaida na shilingi 80,598,000,000 kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi bilioni 101.39 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi Wa Umma, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaendelea na vipaumbele vikuu viwili ambavyo ni kuimarisha matumizi ya Tehama katika utoaji wa huduma kwa taasisi na wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi; na kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma na Kupitia vipaumbele hivyo shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa na shughuli hizi zimeelezwa katika ukurasa wa 57 hadi 58 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 12.76 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni10.8 ni matumizi ya kawaida na shilingi 1,500,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi 450,000,000. ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zilizo chini yake. Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

(i) Kujenga uwezo wa watumishi na taasisi za umma kuhusu namna ya kutumia Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji Kazi wenye moduli mbili za *Public Employee's Performance Management Information System*

na *Public Institution Performance Management Information System* katika Utumishi wa Umma.

(ii) Kujenga uwezo wa taasisi za umma kuanza kutekeleza Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma katika taasisi za umma 215 (wizara 26, sekretarieti za mikoa 26, mashirika na taasisi za umma 70 na mamlaka za serikali za mitaa 93); maelezo zaidi ya shughuli hizo yameoneshwa katika ukurasa wa 58 hadi 62 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Chuo cha Utumishi Wa Umma, kwa mwaka 2023/2024, Chuo cha Utumishi wa Umma kimepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya uongozi na maendeleo, menejimenti na usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 5,260 katika maeneo 25 na watumishi 2,300 kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kuendeleza stadi, weledi na ujuzi; aidha maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 62 hadi 63.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), katika mwaka 2023/2024, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kusimamia na kutathmini hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya Tehama, hatimaye kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha inafanya kazi na kutoa huduma kwa taasisi za umma na wananchi kwa wakati. Maelezo zaidi ya eneo hili yameelezwa katika ukurasa wa 63 hadi 65 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Watumishi Housing Investment*, katika mwaka 2023/2024, *Watumishi Housing Investment* imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine;

(ii) Kutekeleza ujenzi wa nyumba 80 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani hususan katika wilaya mpya;

(iii) Kukuza Mfuko wa Faida ufikie thamani ya shilingi bilioni 30 maelezo zaidi ya eneo hili yanapatikana ukurasa wa 65 hadi 66 wa hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi bilioni 69.317 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 57.13 ni matumizi ya kawaida na shilingi 12.07 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na shilingi milioni 117.2 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika,Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, kwa mwaka 2023/2024 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma itatekeleza shughuli zifuatazo ambazo zinapatikana katika ukurasa wa 66 hadi 67 wa hotuba yetu

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma fungu 67 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 13.7 Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 10.13 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 3.5 ni fedha za miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Utumishi wa Umma, katika mwaka 2023/2024 majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na:-

(i) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za Umma 180;

(ii) Kufanya mikutano minne ya kisheria kwa ajili ya kujadili na kutolea uamuzi rufaa;

(iii) Kuelimisha taasisi za Umma na watumishi wa Umma; maelezo zaidi yanapatikana katika ukurasa wa 67 hadi 68.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi shilingi bilioni 8.6 ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 8.3 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 300,000,000 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, katika mwaka 2023/2024 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itaendelea kutekeleza majukumu kama yalivyoelezwa katika ukurasa wa 68 hadi 70 hotuba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2023/2024, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu 4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 4.3 Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 3.8 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 450,000,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, majumuisho, kimsingi Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo yenye dhamana ya maamuzi juu ya nchi na kwa umuhimu wake inahusika pia na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo kwa pamoja inakuwa nguzo muhimu na mtambuka katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba turejee kuwa Utumishi wa Umma umeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi ambayo kwa sasa Tanzania ni

miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kipato cha kati cha kiwango cha chini. Ni wazi kuwa tunayo matarajio makubwa kuwa mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo utaendelea kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kama inavyoshajiishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu *(Five Year Development Plan III)* Baadhi ya viashiria vinaonekana kwa Nchi yetu kuwa ya tatu katika Afrika na ya kwanza katika Afrika ya Mashariki kwa namna unavyotumia Tehama katika shughuli za Serikali na Utoaji huduma kwa umma kwa uratibu na umahiri wa Mamlaka ya Serikali Mtandao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa tarehe 22 Aprili, 2021 wakati akilihutubia Bunge la 12 aliposema na ninaomba kunukuu; 'Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao.' Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya Ofisi ya Rais yatawezesha vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Hivyo, kupitisha bajeti ya Ofisi hii ni kuchangia katika uimarishaji na uwezeshaji wake vyombo hivyo na malengo yake kwa Taifa. Aidha, kupitisha bajeti hii ni njia ya kuimarisha na kuchangia kukuzwa kwa Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma kwenye nchi na hivyo kupata tija ya rasilimaliwatu na rasilimalifedha kwa kuwa na matumizi yenye tija ya rasilimali hizo kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bajeti hii, Serikali itayapa kipaumbele maeneo ya usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimalifedha. Vilevile, bajeti itaiwezesha Serikali kupandisha vyeo watumishi; ubadilishwaji wa kada au muundo wa utumishi; kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kutoa ajira mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali, Serikali kwa ujumla inafanya maboresho ya kisekta na mtambuka, wajibu wa Ofisi ya Rais itakuwa ni kuhakikisha maboresho yanayofanywa katika nchi yetu hayana urudufu na yanaleta tija katika Utumishi wa Umma na kuchochea maendeleo. Aidha, Ofisi itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi ngazi ya chini. Katika kuimarisha misingi ya utawala bora ya ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji, Ofisi ya Rais itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali na kuweka imara mifumo ya mrejesho wa utoaji huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nchi yetu na kwa mujibu wa Hati idhini inayotoa mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji wa mipango ya bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya

Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, nalihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma kwa kufanyia mapitio ya michakato ya utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2022/2023 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi kwa mwaka 2023/2024 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 20, Ofisi ya Rais Ikulu, Matumizi Kawaida ni bilioni 32.15, Fungu 30, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Matumizi ya Kawaida ni bilioni 678.19, Matumizi ya Maendeleo ni bilioni 189.199.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 33, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Matumizi ya Kawaida ni bilioni 10.8, Matumizi ya Maendeleo, ni bilioni 1.9. Fungu 32, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Matumizi ya Kawaida ni bilioni 57.173, Matumizi ya Maendeleo ni bilioni 12.187.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 67, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Matumizi ya Kawaida bilioni 10.13, na Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni bilioni 3.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, Matumizi ya Kawaida ni bilioni 8.3 na Matumizi ya Maendeleo ni milioni 300. Fungu Na. 4, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, Matumizi ya kawaida ni bilioni 3.8 na Matumizi ya Maendeleo ni Milioni 450.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2023/2024, ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, jumla ya Matumizi ya Kawaida ni bilioni 800,655,546,000 na Jumla Kuu Matumizi ya Miradi ya Maendeleo ni bilioni 200,452,507,000 na hivyo kufanya jumla kuu yote kuwa trilioni 1,001,108,053,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, na Wabunge wenzangu, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha ili Ofisi hii na Wizara hii iende ikatekeleze majukumu yake.

## HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/24 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

### UTANGULIZI

***1. Mheshimiwa Spika,*** Naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako ***Tukufu*** baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria inayohusu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Sasa naomba Bunge likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti

ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2022/23 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2023/24 ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (Fungu 32); Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); na Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04).

***2. Mheshimiwa Spika,*** Kama ilivyo ada naomba uniruhusu nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa wema na huruma ambaye ametuwezesha kukutana hapa tukiwa na afya njema, amani na utulivu hasa katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani kwa kutuwezesha kuendelea kutekeleza majukumu yetu yanayochangia katika kujenga ustawi wa Taifa. Pia, tumshukuru Mungu kwa kutuwezesha kukutana katika kipindi hiki cha Mkutano wa nane wa Bunge la 12 kwa ajili ya kupokea utekelezaji wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na kutafakari mipango ijayo katika kuyafikia malengo ya Nchi.

***3. Mheshimiwa Spika,*** Napenda kutumia fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa imani yake kwangu kwa kuendelea kunipa dhamana hii ya kusimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ina jukumu kubwa la kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma inazingatiwa na watumishi wa umma wanawajibika na kuwa wasikivu wanapotoa huduma kwa wananchi.

***4. Mheshimiwa Spika,*** Naomba nitumie fursa hii kuliahidi Bunge lako ***Tukufu*** na Watanzania wote kuwa nitaendelea

kutumia uwezo wangu wote ili kuendeleza mafanikio yaliyofikiwa na kuhakikisha kwamba Bajeti hii inasimamiwa vema na kutekelezwa ipasavyo. Ni dhahiri kwamba mafanikio makubwa yaliyofikiwa katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yametokana na maono makubwa ya Rais katika kuwaletea Watanzania maendeleo. Tunajivunia na kumshukuru Mungu kwa kuwa na kiongozi mwenye maono chanya kwa mustakabali wa Taifa letu. Naomba tuendelee kumuombea kwa Mwenyezi Mungu aendelee kumjalia afya thabiti, hekima, busara na ustahimilivu katika kuliongoza Taifa letu.

***5. Mheshimiwa Spika,*** niruhusu tena nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu Mhe. Dkt Samia Suluhu Hassan kwa kutimiza kipindi cha miaka miwili akiwa ameshika hatamu kwa mafanikio makubwa yanayojidhihirisha kupitia kazi mbalimbali zinazoendelea katika sekta zote. Ni ukweli usiopingika kwamba Rais wetu amekuwa ni mfano wa kuigwa Kitaifa na Kimataifa kwa kuhakikisha kuwa demokrasia yetu inazidi kustawi na Serikali inaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, utawala wa sheria, kuheshimu haki za binadamu na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na maovu katika jamii.

***6. Mheshimiwa Spika,*** Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyochapa kazi na kumsaidia Rais kutekeleza majukumu yake katika kuliletea Taifa letu maendeleo. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa jitihada zake za dhati za kuimarisha utendaji wenye malengo ya kuleta maendeleo Zanzibar.

***7. Mheshimiwa Spika***, niruhusu pia nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuratibu na kusimamia utendaji kazi za kila siku za Serikali na uwajibikaji Serikalini ambapo ufuatiliaji wake umetoa mwangwi wa uwajibikaji katika Utumishi wa Umma. Lakini, pia namshukuru sana kwa malezi na upendo wake kwangu, ambao napenda nimhakikishie kwamba nitaenzi upendo wake katika maisha yangu yote.

***8. Mheshimiwa Spika***, Naomba nikupongeze wewe binafsi pamoja na Naibu Spika kwa kuliongoza Bunge letu ***Tukufu*** kwa umahiri mkubwa unaodhihirika katika kufikia maamuzi yenye manufaa kwa ustawi wa Taifa letu, hakika mmesimama imara katika kuusimamia Muhimili huu muhimu katika kufanya maamuzi yenye tija kwa maendeleo ya Taifa na Mwenyezi Mungu aendelee kuwatia nguvu zaidi. Vilevile, nawapongeza Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza vyema vikao vya Bunge letu, ni dhahiri kuwa mmetendea haki nafasi zenu na mmekuwa na mchango mkubwa katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

***9. Mheshimiwa Spika,*** Kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza na kuwashukuru wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa *Dkt.* Joseph K. Mhagama, Mbunge wa Madaba, na Makamu wake Mheshimiwa Florent L. Kyombo, Mbunge wa Nkenge kwa ushauri, maoni na ushirikiano mkubwa walioutoa wakati wa maandalizi ya bajeti ya Ofisi yangu kwa mwaka 2023/2024. Naishukuru sana Kamati kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2022/2023 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2023/2024. Napenda kulihakikishia Bunge lako ***Tukufu*** kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa yamezingatiwa katika bajeti hii.

***10. Mheshimiwa Spika,*** naomba nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mawaziri wenzangu wote wa Serikali ya

Awamu ya Sita kwa kuendelea kupewa dhamana ya kuwatumikia Watanzania, kwa kusimamia utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Maelekezo ya Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020. Tuendelee kushirikiana kwa pamoja katika kulijenga Taifa letu.

***11. Mheshimiwa Spika,*** Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa Ridhiwani Jakaya Kikwete kwa kuaminiwa na kupewa dhamana na Mheshimiwa Rais kuhudumu katika nafasi hiyo. Nikuhakikishie kuwa kijana huyu ni hodari, makini na mchapakazi.

***12. Mheshimiwa Spika***, nawashukuru Dkt. Moses M. Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Bw. Mululi M. Mahendeka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Bw. Juma S. Mkomi, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Bw. Xavier M. Daudi, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazofanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo pamoja na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

***13. Mheshimiwa Spika***, Kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China, Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Marekani,

Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Norway, Finland, Uswisi, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vilevile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, Foreign Commonwealth Development Office (FCDO), KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Bill and Melinda Gates Foundation.

***14. Mheshimiwa Spika***, Kipekee nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wananchi wa Jimbo langu la Kibakwe kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha katika kuharakisha maendeleo ya Jimbo na Wilaya yetu. Kwa moyo wa dhati naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa wakati wote ninapokuwa katika utekelezaji wa majukumu ya Kitaifa.

***15. Mheshimiwa Spika,*** kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, viongozi na watumishi wa Umma kutokana na majanga mbalimbali yaliyosababisha uharibifu wa mali na kukatisha uhai kwa Watanzania wenzetu ikiwemo ajali za moto katika Hifadhi ya Taifa Mlima Kilimanjaro na mikoa mbalimbali, Ajali ya ndege ya Kampuni ya *Precision Air* Mkoani Kagera (Bukoba); mvua zilizoambatana na upepo mkali katika mikoa ya Mtwara (Tandahimba), Songwe (Momba), Mbeya (Rungwe), Dodoma (Mpwapwa) na upepo mkali katika Mkoa wa Rukwa (Sumbawanga), mafuriko Mkoa wa Mbeya (Jiji la Mbeya) na mlipuko wa ugonjwa wa *Marburg* hivi karibuni katika Mkoa wa Kagera.

***16. Mheshimiwa Spika,*** Majanga haya yamesababisha vifo kwa Watanzania wenzetu, uharibifu wa nyumba, miundombinu mbalimbali na vitega uchumi vikiwemo mashamba na mifugo. Kwa nafasi hii muhimu, nawapa pole Wabunge wenzangu wanaotoka katika maeneo yaliyokumbwa na kadhia hizo. Salamu za pole ziwafikie

viongozi wa mikoa husika na Watanzania wenzangu walioathirika kwa namna moja au nyingine. Kwa waliotangulia mbele za haki, tunamuomba Mwenyezi Mungu awarehemu na kuwapumzisha kwa amani. Aidha, Watanzania walioathirika na afya hazijarejea, nawaombea kwa Mwenyezi Mungu awaponye ili warejee kwenye majukumu ya kustawisha maisha yao na Taifa. Natoa rai kwa watumishi wa Umma wanaohusika katika kutoka huduma kwa waathirika, kuendelea kujitoa kwa moyo kuhakikisha Watanzania wenzetu hawa wanarejea katika shughuli zao za kila siku.

***17. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2022/23 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayowezesha Ofisi yangu kutimiza majukumu yake. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa mwaka 2022/23 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24.

**MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2022/23**

***18. Mheshimiwa Spika,*** Mpango na Bajeti kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/23 ulitekelezwa kwa kuzingatia miongozo ya kitaifa ambayo ni Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, Hotuba ya Mheshimiwa, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa kuhutubia Bunge la 12 tarehe 22 Aprili, 2021 pamoja na maelekezo yake mbalimbali. Aidha, utekelezaji umezingatia Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/22 - 2025/26), unaotaka Tanzania iwe na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu.

**OFISI YA RAIS - IKULU NA TAASISI ZAKE**

***19. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa **shilingi 29,828,203,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2023 **shilingi 21,993,230,572.76** sawa na asilimia **73.3** zilipokelewa na kutumika.

***20. Mheshimiwa Spika,*** Katika kutekeleza majukumu yake mwaka 2022/23, Fungu 30 Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inayojumuisha taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **shilingi 741,299,267,000.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 577,206,673,000.00** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **shilingi 164,092,594,000.00** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 **shilingi 596,802,557,606.95** sawa na asilimia 80.5 zilipokelewa na kutumika ambapo **shilingi 453,947,339,289.80** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 142,855,218,317.15** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo ya matumizi kwa kila taasisi:-

**A. OFISI YA RAIS - IKULU**

***21. Mheshimiwa Spika***, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali na nchi nzima kwa ujumla. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ajili ya kufanya maamuzi katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda na Kimataifa;

ii. Ofisi imewezesha utekelezaji wa ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutekeleza shughuli zake kama zilivyopangwa;

iii. Huduma zimeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

iv. Mkutano wa faragha (retreat) wa Mawaziri, Makatibu Wakuu, na baadhi ya Viongozi wa Taasisi ulifanyika Arusha kuanzia tarehe 02 – 04 Machi, 2023;

v. Mikutano 16 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 35 zilichambuliwa. Aidha, Mikutano 11 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 26 zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano nane (8) ya kazi ya Makatibu Wakuu ilifanyika ambapo mada 10 ziliwasilishwa na kujadiliwa;

vi. Mikutano mitano (5) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 17 zilijadiliwa na kutolewa uamuzi. Vilevile, mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 12 ilijadiliwa;

vii. Kumbukumbu za Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wakati kwa wahusika. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa;

viii. Mafunzo kuhusu Nyaraka za Baraza la Mawaziri kwa baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Makamu wa Rais yalitolewa;

ix. Mkutano wa faragha (retreat) kati ya Makatibu Wakuu, Makatibu Tawala wa Mikoa na baadhi ya Viongozi wa Taasisi ulifanyika ambapo mada nane (8) zilijadiliwa na kutolewa uamuzi;

x. Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilichambua na kumshauri Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kiuchumi, kijamii, kisheria, kiulinzi, kiusalama na kimataifa;

xi. Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) kwa Wajumbe 65 wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu na watumishi wengine 173 wa Taasisi za Umma yametolewa;

xii. Kikao kimoja (1) cha Waratibu wa Programu za Maboresho kimefanyika kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

xiii. Maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu Kitaifa tarehe 10 Desemba, 2022 yakijumuisha Taasisi za Umma na AZAKI yaliratibiwa na kufanyika;

xiv. Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Nne unaendelea kuandaliwa;

xv. Ziara za ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa zimefanyika katika Mikoa ya Ruvuma, Lindi na Mtwara;

xvi. Rufaa 157 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 442 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

xvii. Majibu na ushahidi kwenye kesi za madai tano (5) kati ya sita (6) kuhusu watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu zinazopinga uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu

Mkuu Kiongozi yalitolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

xviii. Ujenzi wa Ikulu ya Chamwino umekamilika kwa asilimia 100. Taratibu za awali za kuanza ujenzi wa ukumbi wa mikutano na baadhi ya majengo ya ofisi katika Ikulu ya Chamwino zinaendelea. Aidha, ukarabati wa majengo katika Ikulu Ndogo ya Tunguu-Zanzibar na "*Rest House*" iliyoko eneo la Mbweni, Zanzibar unaendelea; na

xix. Ujenzi wa majengo ya Mapokezi, Polisi, Geti Kuu na jengo la mitambo ya umeme umekamilika. Aidha, ujenzi wa ukuta na baadhi ya majengo katika Ikulu Ndogo ya Arusha unaendelea.

**B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)**

***22. Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kuzuia na kupambana na rushwa kwenye sekta ya umma, mashirika na sekta binafsi kwa kuchambua mifumo ya utendaji kazi na utoaji huduma, kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa wa tuhuma za rushwa na ufisadi mahakamani pamoja na kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa, wajibu wao wa kushiriki kwenye kuzuia na kupambana na rushwa na juhudi za Serikali katika kukabiliana na rushwa nchini.

***23. Mheshimiwa Spika***, Katika kutekeleza dhamira ya Serikali ya kutokomeza rushwa nchini jitihada zimeongezwa kwenye kuzuia vitendo vya rushwa katika maeneo yote ambapo katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

**Uzuiaji Rushwa**

i. Miradi ya maendeleo 896 yenye thamani ya shilingi trilioni 6.93 ilifuatiliwa ambapo miradi 137 yenye thamani ya shilingi bilioni 55.48 ilibainika kuwa na kasoro mbalimbali. Kati ya miradi yenye kasoro, miradi 26 elimu ilitolewa kwa watekelezaji kuhusu usimamizi wa miradi, miradi 20 ilifanyiwa udhibiti ili ikamilishwe kama ilivyopangwa na miradi 91 uchunguzi umeanza ili hatua stahiki zichukuliwe;

ii. Tafiti mbili (2) zimefanyika kuhusu ufanisi wa matumizi ya '*force account*' katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na madai, na kuhusu malipo katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF);

iii. Chambuzi 485 za mifumo zenye lengo la kubaini mianya ya rushwa zilifanyika katika maeneo ya **Nishati, Misitu, Fedha, Maji na Huduma** na mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa yalitolewa;

iv. Vikao kazi 304 vya wadau na kazi 236 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati ya kuziba mianya ya rushwa iliyobainishwa katika matokeo ya kazi za utafiti, uchambuzi wa mifumo na ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma katika miradi ya maendeleo vilifanyika; na

v. Mpango wa TAKUKURU RAFIKI unaolenga kuongeza wigo wa ushiriki wa wadau katika kuzuia na kupambana na rushwa umezinduliwa na kuanza kutekelezwa katika mikoa na wilaya zote nchini;

**Uelimishaji umma**

i. Vikao vitatu (3) vya Wadau wa ndani na nje vimefanyika kwa ajili ya kutoa maoni na kupitisha maboresho ya rasimu ya Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano. Mkakati huu unalenga kuimarisha njia za utoaji wa taarifa, uelimishaji na mawasiliano ili kushirikisha wadau wengi

katika harakati na juhudi za kujenga utawala bora na kutokomeza rushwa nchini;

ii. Njia za mawasiliano za kimkakati zilitumika kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kushiriki katika kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa. Njia hizo ni kufungua klabu za wapinga rushwa 69 katika shule za msingi na 20 katika shule za sekondari, kuimarisha klabu za wapinga rushwa 4,992 na kuelimisha vijana wa Skauti ili kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kupitia kazi 63;

iii. TAKUKURU imeshiriki katika kazi ya uboreshaji wa mitaala ya Elimu nchini, kusudi masuala ya rushwa yafundishwe kuanzia ngazi ya shule za awali hadi Chuo Kikuu;

iv. Kutumia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ili kuushirikisha umma katika mapambano hayo, ambapo vipindi vya redio 19 vya 'Rushwa Adui wa Haki' vilirushwa kupitia TBC Taifa, kuandaa na kurusha vipindi vitatu (3) vya televisheni kupitia TBC1, vipindi vitatu (3) kupitia televisheni za Azam (1) UTV (1) na ITV (1) kuandaa na kurusha vipindi 74 vya televisheni mtandao kupitia TAKUKURU TV, kushiriki katika vipindi 321 vya redio jamii na kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa na kuandaa na kusambaza matangazo (*graphic adverts*) 40 katika mitandao ya kijamii;

v. Uelimishaji kwa njia ya runinga wakati wa mikesha ya Mbio za Mwenge wa Uhuru mwaka 2022 ulifanyika katika mikoa sita (6) ya Mara, Singida, Songwe, Rukwa, Katavi na Kagera ambapo jumla ya maonesho 25 yalifanyika kupitia filamu ya BAHASHA inayosisitiza uadilifu na madhara ya rushwa ili kuhamasisha umma kushiriki katika kuzuia na kupambana na rushwa. Makala picha

zinazohamasisha wananchi kushiriki kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao zilirushwa kupitia runinga. Jumla ya wananchi 45,422 walifikiwa na elimu ya mapambano dhidi ya rushwa kupitia maonesho hayo;

vi. Mtandao wa Wabunge wa Afrika wanaopambana na Rushwa (African Parliamentarian's Network Against Corruption - APNAC) walipatiwa semina kuwakumbusha kuhusu nafasi yao katika mapambano dhidi ya rushwa. Aidha, semina ilitolewa kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa (USEMI) kuhusu Programu ya TAKUKURU RAFIKI kwa lengo la kuwajengea uwezo wabunge kuhusu Programu na namna itakavyotekelezwa kwa ushirikiano wa TAKUKURU, viongozi na wananchi katika ngazi ya kata ili kutafuta majawabu ya kero ambazo zinaweza kusababisha vitendo vya rushwa;

**Uchunguzi na Mashtaka**

i. Kesi 758 ziliendeshwa mahakamani zikiwemo kesi mpya 261. Kati ya kesi mpya zilizofunguliwa mahakamani sita (6) ni kesi za rushwa kubwa ambazo zilifunguliwa katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Kesi 300 ziliamuliwa mahakamani ambapo Jamhuri ilishinda kesi 172 kwa watuhumiwa kuhukumiwa kifungo au/na kulipa faini. Kesi 458 zinaendelea mahakamani. Aidha, kiasi cha Shilingi bilioni 1.39 zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi uliofanyika kote nchini ambapo shilingi milioni 257.39 ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini na shilingi bilioni 1.13 zilidhibitiwa;

ii. Mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329 unaendelea ambapo maoni kutoka kwa wadau yamekusanywa. Aidha, rasimu ya Waraka wa Baraza la Mawaziri

imeandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

**Uwezeshaji**

i. Ujenzi wa majengo ya ofisi za TAKUKURU uliendelea ambapo; Jengo la ghorofa tano la Makao Makuu linalojengwa katika eneo la NCC - Dodoma, Kiwanja namba 10 Kitalu A, ujenzi wake umefikia asilimia 60 katika awamu ya kwanza (Phase I). Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Mkoa wa Simiyu umefikia asilimia 15, Wilaya ya Momba asilimia 30, Nyasa asilimia 45 na taratibu za kuanza ujenzi wa "*Safe house*" zinaendelea. Ujenzi wa uzio katika Ofisi ya Mpwapwa na Bahi umekamilika kwa asilimia 100, Masasi asilimia 65, Namtumbo asilimia 50. Ukarabati wa jengo la Chato umefikia asilimia 90, na taratibu za kuanza ukarabati wa jengo la Ofisi ya Mwanza na jengo la Mkoa wa Dodoma zinaendelea. Usanifu wa jengo la ghorofa la TAKUKURU Mkoa wa Iringa umefanyika na taratibu nyingine za kuanza ujenzi zinaendelea;

ii. Mifumo ya TEHAMA imeimarishwa kwa kununua Server nne (4), Computer 184, Ukarabati wa Mtandao Kiambo katika Ofisi ya Mkoa wa Arusha, na Matengenezo Kinga ya vifaa vya TEHAMA; na

iii. Watumishi 1,525 wamepatiwa mafunzo ya kujenga uwezo ili kuongeza weledi wa kutekeleza majukumu kwa ufanisi.

## C. TAASISI YA UONGOZI

***24. Mheshimiwa Spika;*** Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu (*Centre of Excellence*) cha kuendeleza viongozi barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni viongozi waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama. Katika

kipindi cha mwezi Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

i. Utafiti tumizi mmoja ulitekelezwa kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania kama ilivyopangwa. Utafiti ulihusu tathmini ya athari za kimazingira ikiambatana na tathmini ya athari za haki za binadamu (Human Rights Due Diligence) katika ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR kipande cha tatu na nne kutoka Makutupora hadi Isaka kupitia Tabora ili kukidhi vigezo vya sheria na taratibu za kimataifa za kimazingira na kijamii za IFC (*International Financing Cooperation*);

ii. Bodi za Wakurugenzi wa Taasisi na Mashirika ya Umma 34 kati ya 40 zilizopangwa zimepatiwa mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa rasilimali za umma, usimamizi wa rasilimaliwatu, na usimamizi wa viashiria hatarishi kwa ajili ya kuongeza ufanisi, uwajibikaji na uzalendo wa utendaji wa kazi katika mashirika;

iii. Tawasifu inayoelezea maisha ya Hayati Edward Moringe Sokoine, Waziri Mkuu Mstaafu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaendelea kuandikwa. Aidha, Kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Hayati Benjamin William Mkapa kilichotafsiriwa katika lugha ya kiswahili kilichapishwa

iv. Programu mahsusi kwa viongozi wanawake 50 ilitekelezwa kama ilivyopangwa. Programu hii inalenga kuchangia jitihada za kitaifa katika kushughulikia suala la uwakilishi mdogo wa wanawake katika nafasi za juu za maamuzi katika serikali, siasa, biashara na taasisi za kiraia. Vilevile, ushauri wa kuondokana na changamoto binafsi zinazowakabili katika kutimiza wajibu kama viongozi (*coaching*) ulitolewa;

v. Kozi 38 za muda mfupi zimetolewa ikiwa ni zaidi ya lengo la kozi 30 kwa viongozi 2,439. Kozi hizo zina lengo la kuimarisha uwezo wa viongozi kufanya maamuzi ya kimkakati, kuongoza rasilimaliwatu na matumizi ya rasilimali nyingine. Vilevile, kuwajengea uwezo binafsi katika masuala ya mawasiliano, uhusiano, maadili, tabia, mienendo na athari zake;

vi. Awamu ya sita ya Programu ya Stashahada ya Uzamili inayoendeshwa kwa kushirikiana na Chuo cha Aalto toka nchini Finland iliendelea kutekelezwa. Awamu hii, inajumuisha maafisa waandamizi 39 kutoka wizara, taasisi na mashirika ya Umma, taasisi za kiraia na taasisi binafsi. Moduli sita (6) zinazohusu ujuzi wa fedha kwa watendaji, uongozi wa matokeo, ubunifu na maendeleo endelevu na maadili ya kiongozi na mawasiliano ya kimkakati zilitekelezwa kama zilivyopangwa;

vii. Awamu ya tatu ya Programu ya Cheti juu ya Uongozi inayoendeshwa kwa kushirikiana na Chuo cha Aalto toka nchini Finland ilianza kutekelezwa. Awamu hii, inajumuisha maafisa waandamizi 65 kutoka wizara, taasisi na mashirika ya Umma, taasisi za kiraia na taasisi binafsi;

viii. Makongamano sita (6) ya kitaifa yalifanyika na kuvuka malengo yaliyowekwa ya kufanya makongamano matano (5) kwa kipindi cha nusu mwaka kutokana na ongezeko la Taasisi kuomba kushirikiana katika kuandaa makongamano ya kisera nchini. Baadhi ya mada zilizojadiliwa ni usimamizi wa rasilimali za fukwe na kukuza utamaduni wa kujisomea vitabu kwa viongozi;

ix. Ushauri wa kitaalamu kwa Shirika la Reli Tanzania umetolewa juu ya kutathmini ukubwa wa tatizo la uvamizi

wa makazi katika maeneo ya hifadhi ya reli kutoka Makutupora mpaka Mwanza ili kulinda maeneo ya hifadhi ya reli. Vilevile, ushauri ulitolewa kwa Wizara ya Katiba na Sheria jinsi ya kuhuisha Mkakati wa Utekelezaji wa Misingi ya Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusu Umiliki wa Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi Sura 449 na Sheria ya Mapitio kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba ya Utajiri Asili na Maliasilia za Nchi Sura 450. Aidha, ushauri ulitolewa kwa Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira, kuhusu Tanzania inavyoweza kunufaika na fedha kutoka mifuko mbalimbali ya kimataifa, kwa mfano fedha zinazotengwa kwa ajili ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi (*climate financing*); na

x. Kipindi kimoja cha mahojiano na Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu Balozi Ombeni Sefue juu ya utamaduni wa kujisomea kiliandaliwa na kufanyika.

## D. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)

***25. Mheshimiwa Spika,*** Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa Wa Umiliki wa Rasilimali na Uendeshaji Wa Biashara Nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Mashamba 7,825 ya wakulima yamerasimishwa katika Halmashauri za Iramba na Chemba ambapo jumla ya Hati Miliki 7,111 zimeandaliwa na Hati Miliki 5,316 kutolewa kwa wananchi. Urasimishaji umefanyika kwa kuwashirikisha wadau wa viwanda vya usindikaji, Mifuko ya Pembejeo, Wakala wa Mbegu za Alizeti, wamiliki wa maghala, vyama vya ushirika na taasisi za fedha;

ii. Mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara yametolewa kwa wafanyabiashara 3,827 katika Halmashauri za Kibaha (1,665) na Temeke (1,956). Aidha, upande wa Zanzibar mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji biashara yametolewa kwa wafanyabiashara 206 ambapo wafanyabiashara 50 ni wa Kusini -Unguja na 156 wa Micheweni - Pemba;

iii. Ujenzi wa Masijala nne (4) za ardhi za vijiji unaendelea katika Halmashauri tatu (3) za Wilaya ambazo ni Songea (1) ujenzi umefikia asilimia 90, Chemba (1) na Iramba (2) ujenzi umefikia asilimia 5 mtawalia na unatarijiwa kukamilika kabla ya Juni, 2023;

iv. Ujenzi wa Vituo Jumuishi vitatu (3) vya urasimishaji na uendelezaji biashara unaendelea katika halmashauri za miji ambapo Tunduma umefikia asilimia 80, Bunda asilimia 80 na Mpanda asilimia 95 na unatarijiwa kukamilika kabla ya Juni, 2023;

v. Ukarabati wa Vituo Jumuishi vitatu (3) vya urasimishaji na uendelezaji wa biashara unaendelea ambapo katika Halmashauri za Temeke na Mji wa Korogwe umekamilika kwa asilimia 100 na asilimia 50 katika Manispaa za Ilemela. Ukarabati katika Manispaa ya Ilemela unatarijiwa kukamilika kabla ya Juni, 2023; na

vi. Ufuatiliaji na tathmini umefanyika katika Halmashauri za Wilaya 15 Tanzania Bara ambapo tathmini imebainisha kuwa wananchi wamenufaika na urasimishaji biashara na ardhi.

**E. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)**

***26. Mheshimiwa Spika,*** Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa

kuweka kipaumbele kwenye maeneo ya ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeleza kazi zifuatazo:-

i. Uhakiki wa awali wa kaya umefanyika katika Mamlaka za Utekelezaji 186. Jumla ya kaya 713,350 zilihakikiwa ambapo kaya 670,566 zilikidhi vigezo vya uhakiki wa awali wa kuendelea kuwepo katika Kipindi cha Pili cha Mpango na zaidi ya kaya 156,000 zimeboreka kiuchumi;

ii. Ruzuku ya shilingi bilioni 218 ilihawilishwa kwa kaya 1,371,916 zilizokidhi vigezo vya kuingia katika Kipindi cha Pili cha Mpango kutoka maeneo yote ya utekelezaji 186 kwa Tanzania Bara, Pemba na Unguja kwa Zanzibar kufikia Machi, 2023;

iii. Mfuko umepokea na kuanza kushughulikia rufaa za wananchi ambao hawakuingizwa kwenye Mpango wakati wa zoezi la utambuzi na uandikishaji kutoka maeneo yote 186 ya utekelezaji ili watakaokidhi vigezo waingizwe kwenye Mpango ifikapo Mei 2023;

iv. Jumla ya miradi 14,236 iliibuliwa na jamii na kuanza kutekelezwa katika mamlaka za utekelezaji 123 ambapo kaya za walengwa 660,000 zimeshiriki katika kutekeleza miradi hiyo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 40.2. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 18.1 ni kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi na shilingi bilioni 13.2 kwa ajili ya ujira wa kaya za walengwa wanaofanya kazi katika miradi hiyo, shilingi bilioni 5.6 kwa ajili ya maandalizi ya miradi na shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wakati wa utekelezaji;

v. Miradi 550 ya kuendeleza miundombinu iliibuliwa na utekelezaji wake upo katika hatua mbalimbali. Miradi 63 imekamilika na kuanza kutoa huduma katika sekta za elimu, afya, maji, mazingira, barabara na ujasiriamali. Jumla ya shilingi billioni 25.9 zimetumika katika utekelezaji wa miradi hiyo na jumla ya wataalam 120 kutoka mamlaka 44 za utekelezaji wa Mpango walipatiwa mafunzo ya uwezeshaji na usimamizi wa miradi;

vi. Jumla ya vikundi 12,054 viliundwa vyenye wanachama 165,608 (wanawake 137,451 na wanaume 28,157) kwenye Mamlaka 72 za utekelezaji kwa Tanzania Bara, Unguja na Pemba kwa Zanzibar. Hivyo, kufanya jumla ya vikundi vilivyoundwa na Mpango Tanzania Bara na Zanzibar kuwa 43,302 vyenye wanachama 587,397 (wanawake 497,479 na wanaume 89,918). Aidha, vikundi hivyo vimeweka akiba kiasi cha shilingi bilioni 7.9 na kukopeshana kiasi cha bilioni 3.1. Vilevile, mafunzo yamefanyika kwa wawezeshaji 1,474 wa ngazi ya Wilaya yanayohusu uhamasishaji na uundaji wa vikundi, uwekaji kumbukumbu za taarifa za fedha, usimamizi wa mikopo na utatuzi wa migogoro;

vii. Jumla ya Walengwa 24,019 kati ya 29,000 waliopangwa, walipokea ruzuku ya kuanzisha shughuli za kiuchumi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.81 kwa wastani wa shilingi 240,000 kwa mlengwa;

viii. Jumla ya mamlaka za maeneo ya utekelezaji 186 zilifikiwa kupitia Mpango wa Ulipaji kwa Njia ya Kielekroniki ambapo walengwa 378,375 sawa na asilimia 27.7 (asilimia 89 ni wanawake) walilipwa katika kipindi cha Novemba – Desemba 2022;

ix. Tathmini ya awali ya Kipindi cha Pili cha Mpango imefanyika katika Maeneo ya Utekelezaji 32 kutoka katika

Vijiji, Mitaa na Shehia 434 ambapo Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (OCGS) zilihusika. Uchakataji wa takwimu zilizokusanywa kwa walengwa na uandaaji wa taarifa ya tathmini hii unaendelea. Aidha, utekelezaji wa shughuli katika maeneo ya sampuli umeanza kufanyika ili kuwezesha hapo baadaye kupima mafanikio ya Mpango kwa walengwa; na

x. Mapitio ya pamoja ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango yamefanyika katika vipindi viwili (2) vya Julai, 2022 na Januari, 2023. Taarifa zote za mapitio zimeonesha utekelezaji wa Mpango unaendelea vizuri na unawasaidia walengwa kuondokana na umaskini na kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kuwaendeleza watoto katika afya na elimu bora. Wadau wa Maendeleo wameahidi kuendelea kushirikiana katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, wadau hao wameahidi kushirikiana na Serikali katika kuongeza muda wa utekelezaji kwa kipindi cha miaka miwili (2) ili kufidia muda uliopotea kutokana na kuchelewa kuanza kwa utekelezaji.

**F. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI**

***27. Mheshimiwa Spika,*** Wakala ya Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, mwaka 2016 Wakala iliongezewa jukumu la kuratibu ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo kwa niaba ya Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2022 hadi Machi, 2023 kazi zifuatazo zimetekelezwa:-

i. Huduma ya usafiri wa anga imeendelea kutolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa;

ii. Matengenezo makubwa ya Ndege aina ya Gulfstream 550 inayohudumia Viongozi Wakuu wa kitaifa yamefanyika nchini Marekani na ndege imekwisharejea nchini;

iii. Matengenezo makubwa ya injini (Engine overhaul) ya akiba ya ndege aina ya Fokker 50 yanaendelea nchini Singapore;

iv. Wanaanga 41 wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi nje ya nchi ili kuhuisha leseni zao. Aidha, watumishi wengine 30 wa Wakala wamewezeshwa kwenda mafunzo mbalimbali ili kuboresha utendaji kazi wao;

v. Wakala umekamilisha awamu ya kwanza ya ujenzi wa Karakana ya Dar es Salaam ya ndege za Serikali kwa asilimia 100 ambao umehusisha ujenzi wa ofisi na stoo ya kuhifadhia vipuri vya ndege. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa Karakana hiyo inayohusisha eneo la maegesho na matengenezo ya ndege unaendelea;

vi. Gharama za bima za ndege pamoja na bima za wanaanga zimelipwa; na

vii. Ununuzi wa ndege umeratibiwa na mikataba ya ukodishwaji wa ndege za Serikali kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL) imesimamiwa.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

***28. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **shilingi 12,730,049,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 9,260,049,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 3,470,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2023 fedha zilizopokelewa na kutumika ni **shilingi 6,700,542,089.33.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 6,040,699,726.12** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 659,842,363.21** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***29. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilipanga na kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Hadi kufikia Desemba 2022, Matamko ya viongozi wa umma kuhusu rasilimali na madeni yapatayo 14,941 kati ya matarajio 15,893 yamepokelewa ikiwa ni sawa na asimilia 94;

ii. Malalamiko 169 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 133 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na malalamiko 36 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma hivyo yalipelekwa kwa taasisi husika. Aidha, malalamiko 11 yanayohusu Sheria uchunguzi wake umekamilika, 68 yalitolewa ushauri na 54 uchunguzi unaendelea. Malalamiko husika yanajumuisha maeneo ya migogoro ya ardhi, rushwa na jinai.

iii. Uhakiki kuhusu Rasilimali, Madeni na Mgongano wa Maslahi ulifanyika kwa jumla ya Viongozi 592. Kati yao, asilimia 8 walibainika kuwa na dosari katika matamko, na asilimia 4 walibainika kuwa na mgongano wa masilahi. Viongozi wenye kasoro watafanyiwa uchunguzi wa kina

na ambao tuhuma zitathibitika watafikishwa kwenye Baraza la Maadili;

iv. Elimu kuhusu maadili na dhana ya Mgongano wa Maslahi ilitolewa kwa Viongozi wa Umma 1,561, Watumishi wa Umma 4,423 na Wananchi 3,264;

v. Klabu 22 za Maadili zenye wanachama 1,000 zilianzishwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo. Klabu 31 zilitembelewa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili miongoni mwa wanafunzi na wanachama wa klabu. Lengo la klabu hizi ni kukuza na kuendeleza vijana katika kuzingatia maadili na kujiandaa kuwa viongozi;

vi. Mapitio ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya mwaka 1995 yamefanyika; na

vii. Ujenzi wa jengo la Ofisi ya makao makuu na kanda ya kati Dodoma la Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma umefikia asilimia 90.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA NA TAASISI ZAKE**

***30. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Fungu 32 inayojumuisha Mamlaka na Taasisi zilizo chini yake ilitengewa jumla ya **shilingi 47,611,581,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo**.** Kati ya fedha hizo, shilingi **39,541,381,000.00** ni matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 83.05** ya bajeti iliyoidhinishwa na **shilingi 8,070,200,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 16.95** ya bajeti iliyoidhinishwa.

***31. Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi, 2023 kiasi cha **shilingi 41,300,525,557.88** sawa na **asilimia 86.74** ya bajeti

iliyoidhinishwa kilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **shilingi 34,670,422,884.74** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 6,630,102,673.14** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA**

***32. Mheshimiwa Spika,*** Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2022 hadi Machi, 2023 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Mfumo mpya wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma wenye moduli mbili za Usimamizi wa Utendaji Kazi wa Mtumishi wa Umma *(Public Employees Performance Management Information System - PEPMIS)* na Usimamizi wa Utendaji Kazi kwa Taasisi za Umma *(Public Institutions Performance Management Informantion System - PIPMIS)* umeendelea kuimarishwa. Aidha, zoezi la utekelezaji wa mfumo kwa majiribio katika taasisi 12 limefanyika kwa lengo la kubaini kama mfumo unakidhi mahitaji ya taasisi tumizi. Taasisi hizo ni: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais -TAMISEMI; Wizara ya Kilimo; Wizara ya Maliasili na Utalii; Shirika la Viwango Tanzania (TBS); Mamlaka ya Bandari ya Tanzania (TPA); Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO); Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT); Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU); Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma; na Halmashauri ya Wilaya ya Songea Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (CWF) na kubaini kuwa mfumo unafanya kazi vizuri;

ii. Katika kuwezesha utendaji kazi wa mifumo na watumiaji wa mifumo, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) na kuboresha moduli ya Watumishi Portal yenye huduma za kielektroniki za uhamisho wa watumishi, mikopo ya watumishi, taarifa binafsi za mtumishi na Hati ya Malipo ya Mishahara;

iii. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa mifumo ya taasisi zake inabadilishana taarifa ambapo Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara umeunganishwa na: Mfumo wa PSSSF kwa ajili ya kubadilishana taarifa za michango ya watumishi na nyaraka za hitimisho la ajira; Mfumo wa Mikopo ya Elimu ya Juu (HESLB) kwa ajili ya kubadilishana taarifa za mikopo ya elimu ya juu ya watumishi; Mfumo wa Ajira Portal kwa ajili ya kubadilishana taarifa za waajiriwa wapya; Mfumo wa NIDA kwa ajili ya kubadilishana taarifa za utambulisho wa Taifa wa watumishi; Mfumo wa malipo Serikalini (MUSE) kwa ajili ya kubadilishana taarifa za malipo ya watumishi kwenye akaunti zao za benki; Mifumo ya benki kwa ajili ya kubadilishana taarifa za akaunti za benki na mikopo ya watumishi; Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma kwa ajili ya kubadilishana taarifa za utendaji kazi kwa watumishi wa umma; Mfumo wa Mahudhurio (Biometric Attendace System) kwa ajili ya kubadilishana taarifa za mahudhurio ya watumishi; na Mfumo wa *PlanRep* kwa ajili ya kubadilishana taarifa za bajeti ya mishahara ya watumishi;

iv. Mkakati wa Serikali wa Kujilinda na Majanga ya Kimtandao wa mwaka 2022 umeandaliwa na kukamilika. Mkakati huu unalenga kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi wa usalama wa mitandao ya Serikali pamoja na kujenga uelewa wa kutosha kwa wadau kuhusu usimamizi wa vihatarishi vya usalama wa mitandao ya Serikali. Vilevile, Mwongozo wa Matumizi Bora, Sahihi na Salama ya Vifaa, Data na Mifumo ya TEHAMA kwenye Taasisi za Umma wa Mwaka 2022 umeandaliwa na kukamilika. Mwongozo huu unalenga kuweka utaratibu madhubuti wa kusimamia mifumo, data na vifaa vya TEHAMA Serikalini;

v. Taasisi 433 kati ya 522 zimewezeshwa kutumia Mfumo wa Kiutumishi na Mishahara katika kuandaa Ikama, kulipa mishahara, kusafisha taarifa, kubadilisha kada, kushughulikia upandishwaji vyeo, kuandaa taarifa za

uhamisho pamoja na kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa Maafisa Utumishi 412, Wakuu wa Idara za Utumishi na Utawala 83, Wakaguzi wa Ndani 97 na Wahasibu 98 wa Taasisi za Umma;

vi. Taarifa za kiutumishi kwa watumishi wa Umma zimechakatwa kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wa huduma mbalimbali serikalini.

vii. Serikali imelipa madai malimbikizo ya mishahara ya watumishi 14,398 yenye jumla ya **shilingi 25,655,848,954.61** hadi Machi 2023**.** Vilevile, madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma **2,942** waliokoma utumishi wao yenye thamani ya **shilingi 8,534,408,682.65** yamelipwa. Aidha, kwa kipindi cha mwaka mmoja, kuanzia Februari, 2021 hadi Machi, 2023 Serikali ya Awamu ya Sita imelipa jumla ya madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi **119,098** yenye thamani ya **shilingi 204,420,741,285.25;**

viii. Vibali vya ajira mpya **30,000** na vibali vya ajira mbadala **7,721** kwa waajiri kutoka katika taasisi mbalimbali vimetolewa;

ix. Uhakiki kupitia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara kwa watumishi wa Umma kwa waajiri 380 kati ya waajiri wote 433 umefanyika kwa lengo la kuboresha huduma na masilahi ya watumishi;

x. Ufadhili wa mafunzo kwa watumishi wa Umma 355 umetolewa ambapo watumishi 100 walipata mafunzo ya muda mrefu kutoka Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China, Korea, Japan na India na watumishi 255 walipata mafuzo ya muda mfupi kutoka Serikali ya Japan, India, China na

Korea. Serikali inaendelea kuweka mkazo ili utekelezaji wa mafunzo hayo uzingatie ujuzi unaohitajika kwa sasa, malengo ya Dira ya Taifa ya mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III);

xi. Vibali 630 vya wataalam wa kigeni vyenye msamaha wa ada katika Sekta mbalimbali za maendeleo pamoja na Mashirika ya Kimataifa na Kikanda, Kiserikali na yasiyo ya Kiserikali vilitolewa. Wataalam hao hutumika katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati;

xii. Mafunzo ya Mfumo wa kielektroniki wa e-Mrejesho yametolewa kwa maafisa 148 wanaoshughulikia mrejesho kwa lengo la kutoa ufafanuzi na ufumbuzi wa masuala mbalimbali yanayohusu huduma zitolewazo na Serikali. Mfumo utarahisisha upatikanaji wa huduma kwa wateja popote walipo badala ya kusafiri kwa lengo la kupata huduma hizo;

xiii. Taasisi 62 zimewezeshwa kuandaa na kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu na kuidhinishwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

xiv. Serikali imeandaa Mfumo wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma (*HR Assessment System*) unaowezesha kubaini idadi ya watumishi waliopo, kada zao, nafasi ya kazi, vituo vya kazi na majukumu wanayotekeleza. Lengo ni kubaini mahitaji halisi, upungufu au ziada ya watumishi katika taasisi za umma kwa ajili ya kuchukua hatua. Hadi sasa waajiri wote wamejaza taarifa muhimu katika Mfumo; Mfumo umewezesha kubaini watumishi waliopo wa Kada ya Walimu 256,479 (kati ya hao, walimu wa Msingi ni 171,920; na Sekondari ni 84,559); Mfumo pia umebaini mahitaji ya walimu kwa nchi nzima. Vilevile, Mfumo huo umetengenezewa Moduli yenye

kuwezesha uchambuzi wa kada nyingine na kazi ya uchambuzi inaendelea;

xv. Taasisi zote za Umma zimejengewa uelewa wa kuandaa na kutekeleza mkataba wa huduma kwa mteja. Taasisi zote kwa sasa zinahuisha mikataba yao na itazinduliwa upya kwa pamoja Mei, 2023 na kuanza kutumika. Utekelezaji wa mikataba unasaidia kuongeza uwajibikaji wa watumishi wa Umma katika kuhudumia wateja kwa viwango na ahadi zilizowekwa katika Mkataba. Mikataba hiyo inalenga kuboresha utoaji wa huduma za Taasisi na kuimarisha utamaduni wa utendaji kazi unaozingatia matakwa ya wateja;

xvi. Serikali imebuni dhana ya Daftari la Huduma za Serikali Tanzania ***(Government Service Directorate - GSD)***. Hatua zilizotekelezwa ni pamoja na kusanifu Mfumo wa GSD; taarifa za huduma 925 za Serikali zimekusanywa kutoka katika Taasisi 58 (Wizara 7 na Taasisi 51 zilizo chini yake) ikiwemo Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Uwekezaji; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari; Wizara ya Maliasili na Utalii; Wizara ya Viwanda na Biashara; na Wizara ya Katiba na Sheria. Zoezi la kukusanya taarifa linatarajiwa kuendelea katika Taasisi 525;

xvii. Serikali imeanzisha vituo viwili (2) vya Huduma kwa Pamoja katika majengo ya Ofisi za POSTA mikoa ya Dodoma na Dar es salaam kwa majaribio. Huduma zitolewazo katika vituo hivyo ni kutoka katika Taasisi za NIDA, RITA, TRA, NSSSF, PSSSF, UHAMIAJI, BRELA, NHIF na POLISI. Mpango wa Serikali ni kupeleka huduma hizi kila mkoa;

xviii. Vibali vya uteuzi 689, vibali vya kukaimu 941, vibali vya uhamisho 5,034, vibali vya likizo bila malipo 257 na vibali vya ajira za mikataba 1,065 vimetolewa. Vibali hivyo vinalenga kuimarisha utawala wa utumishi wa umma ili kupata viongozi wenye sifa stahiki, weledi na maono ya utumishi wa umma wenye kuzingatia Dira ya Maendeleo na mikakati mbalimbali ya kitaifa;

xix. Utafiti wa Hali ya Uadilifu katika Utumishi wa Umma Mwaka 2022 umefanyika ambapo umebainisha kuwa kiwango cha uadilifu katika utumishi wa umma kimeongezeka na kufikia asilimia 75.9 ikilinganishwa na asilimia 66.1 mwaka 2014;

xx. Mafunzo ya maadili ya utendaji kazi katika utumishi wa Umma kwa watumishi 9,101 kutoka katika taasisi za Umma 108 yameendeshwa kati ya 150 zilizopangwa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili na uadilifu katika Utumishi wa Umma. Aidha, kampeni za kimaadili kupitia vyombo vya habari zimefanyika kupitia vipindi vya runinga (ITV) na redio (TBC FM na E-FM) pamoja na kushiriki katika Maadhimisho 40 ya Wiki ya Uadilifu Kitaifa yaliyofanyika Desemba, 2022 jijini Dodoma;

xxi. Ujenzi na ukarabati wa majengo ya ofisi na nyumba za viongozi umeendelezwa, ambapo ujenzi wa jengo la ghorofa tano (5) la Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika eneo la Mtumba umefikia asilimia 68, ujenzi wa Klabu ya Viongozi - Makao Makuu eneo la Nzuguni umeanza kwa kujenga uzio ambao umefikia asilimia 65, ujenzi wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Tano Hayati Dkt. John Magufuli umefikia asilimia 99 na ukarabati wa nyumba ya makazi ya Rais wa Awamu ya Kwanza Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius K. Nyerere umefikia asilimia 58; na

xxii. Kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali majibu na ushahidi umetolewa kwenye mashauri ya madai saba (7) yaliyofunguliwa Mahakama Kuu kupinga maamuzi ya Katibu Mkuu Utumishi, kesi tano (5) kati ya kesi saba (7) zilizofunguliwa zimehitimishwa na kwa sasa zimebaki kesi mbili (2) zinazoendelea Mahakama Kuu.

**B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA TANZANIA (TPSC)**

***33. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Mafunzo ya awali yametolewa kwa watumishi wa umma wapya 1,739, mafunzo ya uongozi na maendeleo kwa watumishi wa umma 4,508 na mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya utumishi wa umma kwa watumishi 1,399;

ii. Uwezo wa watumishi 321 umejengwa katika utaalam wa fani mbalimbali ikiwemo menejimenti ya utumishi wa umma kwa ngazi ya kitaifa na kimataifa kupitia midahalo iliyosaidia kubadilishana uzoefu kwa njia ya mtandao;

iii. Mafunzo ya muda mrefu yametolewa kwa wanachuo 10,032 katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, kompyuta, utunzaji wa fedha za Umma, menejimenti ya rasilimaliwatu, usimamizi na ununuzi wa Umma, uongozi na utawala bora. Mafunzo hayo, yanalenga kuimarisha stadi, weledi na ujuzi wa kazi za Serikali; na

iv. Ushauri wa kitaalam katika maeneo tisa (9) umetolewa ili kuwawezesha watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma.

## C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA)

***34. Mheshimiwa Spika,*** Matokeo ya utafiti wa Benki ya Dunia (World Bank) ya hivi karibuni ya Ulinganifu baina ya nchi katika Faharasa ya Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia (***Government Technical Maturity Index***) yamebainisha kuwa, Tanzania imeshika moja ya nafasi za juu katika matumizi ya Serikali Mtandao miongoni mwa nchi zilizoshindanishwa pamoja na nchi nyingine za ukanda wake. Matokeo hayo yamezidi kubainisha kuwa kuna maeneo ambayo kwa sasa Tanzania inachuana kwa ukaribu na nchi vinara kama vile China, Israel na Ireland wakati ikiwa kinara Afrika Mashariki.

***35. Mheshimiwa Spika,*** Ukilinganisha na nchi nyingine Barani Afrika, Tanzania imeshika nafasi ya tatu (3) ikizikaribia Misri pamoja na Mauritius. Katika ukanda wa Afrika Mashariki, Tanzania ndiyo Kinara kwa nchi wenza ikifuatiwa na Uganda wakati Kenya na Rwanda zikishika nafasi za katikati. Tanzania imefanikiwa kushika nafasi za juu katika ulinganifu huo, kufuatia utekelezaji wake mzuri wa Sera mbalimbali, Miongozo pamoja na Mikakati ya matumizi ya TEHAMA chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA). Mamlaka ya Serikali Mtandao imekuwa ni msimamizi kinara wa juhudi za Serikali katika kuelekea mapinduzi ya Kidijiti.

***36. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Ujenzi wa Mfumo maalum wa kuwezesha Mifumo ya Serikali Kusomana na Kubadilishana Taarifa *(Government Enterprise Service Bus - GovESB)* umekamilika ambapo mifumo 55 ya Taasisi 50 imewezeshwa kuwasiliana na kubadilishana taarifa;

ii. Utafiti na ubunifu wa matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA katika utoaji huduma kwa Umma na utendaji wa Serikali umefanyika katika maeneo ya *Digital Currency, BlockChain, Internet of Things* (IoT), *Artificial Intelligence*

(AI), na *Machine Learning (ML)*. Aidha, mifumo mipya imebuniwa na kuboreshwa ikiwemo mifumo ya e-Mrejesho, e-Mikutano, e-Rufaa, e-Dodoso, pamoja na *Shared Helpdesk*. Vilevile, Mamlaka imeendeleza ushirikiano na Watafiti wa ndani na nje ya nchi;

iii. Ujenzi wa Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) nchini umekamilika na kuwezesha mikoa 26 na vyama vya ushirika zaidi ya 3,700 kuanza kusimamiwa na Tume ya Ushirika kupitia Mfumo huo;

iv. Ujenzi wa Mfumo wa kusimamia Kazi za Wakala wa Ununuzi Serikalini (GIMIS) umekamilika na kuanza kutumika na taasisi za Umma katika kufanya ununuzi mbalimbali ikiwemo mafuta kwa magari na mitambo ya Serikali;

v. Ujenzi wa Mfumo wa Uwekezaji wa Pamoja wa Watumishi Housing Investment (FAS) umekamilika na unatumika;

vi. Ujenzi wa Mfumo wa Taifa wa Kusimamia Ajira umejengwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu - Kazi ambao unalenga kuwezesha kuwa na taarifa zote za ajira nchini, nafasi za kazi na kuweza kupata takwimu kamili za hali ya Soko la Ajira nchini. Mfumo upo katika hatua za ukamilishaji, ambapo mfumo huu una moduli tatu (3), moduli ya kwanza ni Huduma za Ajira inayosimamiwa na TaESA imekamilika na inatumika, moduli ya pili kwa ajili ya kusimamia shughuli za watu wenye ulemavu, imefikia asilimia 95 na ipo katika majaribio na mafunzo, moduli ya tatu ni ya soko la ajira, ambao upo kwenye hatua ya usanifu na ujenzi;

vii. Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi (ERMS) umeboreshwa na taasisi mpya tisa (9) zimeunganishwa kwenye Mfumo huo na kufanya jumla ya Taasisi

zilizounganishwa kufikia 37. Aidha, uunganishwaji wa mfumo wa ERMS na MAJIIS umekamilika;

viii. Ujenzi umeendelezwa kwa Mfumo Maalum wa Kusimamia Utoaji Huduma kwenye Zahanati na Vituo vya Afya (GoTHOMIS Lighter Version) ambapo umefikia asilimia 83 na upo katika hatua za majaribio;

ix. Mfumo wa kusimamia mikopo ya asilimia 10 kwenye Halmashauri umekamilishwa na kuanza kutumika;

x. Taasisi mpya za Umma 25 zimewezeshwa kutoa huduma kwa njia ya simu za mkononi kupitia Mfumo Mkuu wa kutoa Huduma kupitia Simu za Mkononi (GovSMS) na kufanya jumla ya taasisi zilizowezeshwa kutoa huduma kwa njia ya simu za mkononi kufikia 307;

xi. Taasisi za Umma 134 zimewezeshwa kuhifadhi mifumo na taarifa kwenye Vituo Vikuu vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya Serikali (*Government Data Centres*) vyenye usalama na uhakika wa upatikanaji wa taarifa za Serikali;

xii. Miundombinu ya Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini (*Government e-Payment Gateway* – GePG) umeboreshwa ambapo taasisi mpya 100 zimeunganishwa kwenye mfumo huo na kufanya jumla ya taasisi na vituo vya kutolea huduma vilivyounganishwa kufikia 973. Vilevile, ujenzi wa Mfumo wa Tiketi za Kieletroniki katika Shirika la Meli Tanzania (MSCL) umefikia asilimia 47 ambapo ujenzi wa Mfumo Mkuu umekamilika na hatua inayoendelea ni ujenzi wa mifumo mlishi kama tovuti ya kukatia tiketi, aplikesheni za kufanya uhakiki kupitia mageti, pamoja na aplikesheni za kukata na kuhakiki tiketi kwa njia ya POS;

xiii. Ushirikiano umeendelezwa kati ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) na Wakala ya Serikali Mtandao Zanzibar (eGAZ) ili kuendeleza jitihada za Serikali Mtandao kwa kubadilishana uzoefu katika utendaji kazi na utoaji huduma kwa Umma. Ushirikiano huo umewezesha kuanza kwa matumizi ya mifumo mbalimbali katika Serikali ya Zanzibar ikijumuisha Mfumo wa Barua pepe Serikalini (GMS), *e*-Office, ZanMalipo unaotokana na mfumo wa GePG, ZanAjira unaotokana na Mfumo wa Ajira Portal, e-Wawakilishi unaotokana na e-Parliament, na Mfumo wa Ankara za maji kwa ajili ya ZAWA;

xiv. Matumizi ya mifumo ya kutolea huduma kwa wananchi imewezeshwa, kama vile Mfumo wa Kusaidia Kutoa Huduma kwa Kinamama na Watoto (M-MAMA) kwa kushirikiana na Vodacom Foundation, Wizara ya Afya na TAMISEMI;

xv. Taasisi mpya 14 zimeunganishwa kwenye Mfumo wa Barua Pepe wa Serikali (*Government Mailing System*) na kufanya taasisi na vituo vya kutolea huduma vinavyotumia mfumo kufikia 616;

xvi. Usimamizi wa uendeshaji wa mifumo shirikishi inayotumiwa na taasisi nyingi kwa pamoja imefanyika ili kupata tija na ufanisi wa matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika utendaji kazi na utoaji wa huduma kwa Umma. Mifumo hiyo ni pamoja na Mfumo wa Malipo ya Serikali (GePG), Mfumo wa Malipo Serikalini (MUSE), Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS), Mfumo wa Mipango na Bajeti (PlanRep), Mfumo wa Kukusanya Mapato kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa (TAUSI), Mfumo wa Ankara za Maji (MAJIIS), Mfumo wa Ofisi Mtandao (e-Office), Mfumo wa Bunge Mtandao, Mfumo wa Ununuzi Serikali (NEST), Mfumo wa Kusimamia Utendaji Kazi wa Watumishi (PEPMIS) na Taasisi za Umma (PIPMIS), Mfumo wa Ajira

Portal, Mfumo wa Barua Pepe (GMS) na Mfumo wa Huduma kupitia Simu za Mkononi (M-Gov) uliounganishwa na kampuni binafsi za watoa huduma za mawasiliano wote ili kuwafikia wananchi kwa urahisi. Mifumo hii imejengwa kwa kufuata viwango na miongozo na inaweza kubadilishana taarifa inapohitajika; na

xvii. Ushiriki katika ujenzi na uendeshaji wa mifumo ya Kitaifa mfano; Mfumo wa Single window (TPA na TRA), LUKU Mpya (TANESCO), TIPS (BOT), NAPA (Mawasiliano) na Mfumo wa SENSA (NBS).

**D. WATUMISHI HOUSING INVESTMENT (WHI)**

***37. Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na:

i. Ujenzi wa nyumba 175 umekamilika katika mradi wa nyumba 1,000 eneo la Njedengwa jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine zikiwemo wilaya mpya. Vilevile, vitalu Na. 383, 384, 385, 549 katika eneo la Chamwino Buigiri na Mtumba Kitalu Na. 695 vimenunuliwa kwa ajili ya ujenzi;

ii. Viwanja 326 katika eneo la WHI - USA RIVER jijini Arusha lenye ekari 112 vimepimwa kwa ajili ya kuuzwa ambapo idhini ya Mipango miji imepatikana. Kazi ya kuweka miundombinu ya madaraja na barabara imeanza kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Arumeru na TARURA. Kazi hiyo imefikia asilimia 70 na inatarajiwa kukamilika ifikapo Mei, 2023. Mauzo ya viwanja tayari yameanza;

iii. Jumla ya nyumba 52 zimejengwa kwa ajili kuwauzia watumishi wa umma na wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii katika Mikoa ya Dodoma eneo la Kisasa Hilltop Njedengwa nyumba 25, Dar es Salaam (9) na Morogoro (18). ambapo, katika mradi wa Kisasa Hilltop Njedengwa nyumba zimeuzwa kwa zaidi ya asilimia 90;

iv. Mfuko wa Uwekezaji wa Pamoja wa Faida Fund umeanzishwa ambapo vipande vyenye thamani kiasi cha Shilingi bilioni 14.20 vimenunuliwa na wawekezaji wapatao 1,557. Thamani halisi ya mfuko imefikia shilingi bilioni 14.45;

v. Huduma za ujenzi na ushauri kwa taasisi za Serikali zimetolewa kama ifuatavyo: Ujenzi wa ukuta kwa nyumba za Chuo Kikuu cha Dodoma na geti kuu la Chuo Kikuu cha Dodoma; kutoa ushauri elekezi na usimamizi wa miradi mitatu (3) ya ujenzi wa majengo ya ofisi za Serikali na Taasisi (Makao Makuu la *Universal Communication Service Access Fund* – UCSAF, Usimamizi wa ujenzi wa jengo la ofisi ya Rais Utumishi Mji wa Serika Mtumba na ujenzi wa Jengo la maabara ya *Digital Forensic* la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi) na ujenzi wa jengo la Wizara ya Afya jijini Dodoma.

**OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

***38. Mheshimiwa Spika,*** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilianzishwa kwa mujibu wa Sera ya Menejimenti na Ajira Katika Utumishi wa Umma toleo la pili la mwaka 2008 aya ya 4.6 na 6.6 pamoja na kifungu cha 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 iliyorejewa 2019, ambazo zinaelekeza kuwepo kwa chombo maalum cha kushughulikia mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma. Jukumu kuu la Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ni kuwezesha mchakato wa ajira katika Utumishi wa Umma. Ofisi ya Rais -Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inatekeleza majukumu kwa mujibu wa kifungu cha 29 (7) cha Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura ya 298 iliyorejewa 2019.

***39. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 8,721,849,000.00** Kati ya kiasi hicho, **shilingi**

**5,063,849,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 3,658,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***40. Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi, 2023 **Shilingi 5,211,962,534.10** sawa na asilimia **59.8** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,130,572,665.00** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,081,389,868.82** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

***41. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:

i. Matangazo ya kazi 347 yaliandaliwa na kutolewa kupitia tovuti ya Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa niaba ya Waajiri 319 kutoka Wizara na Taasisi za Umma;

ii. Maombi ya kazi 368,672 kwa kada mbalimbali yalipokelewa na kuchambuliwa, ambapo maombi 193,391 yalikidhi sifa na waombaji waliitwa kwa ajili ya usaili na maombi 175,281 hayakukidhi sifa kwa mujibu wa miundo ya kiutawala;

iii. Saili 23 ziliratibiwa na kusimamiwa kwa niaba ya waajiri 319 ikiwa ni utekelezaji wa kibali cha ajira mpya kwa mwaka 2021/22 ambapo jumla ya wasailiwa 10,704 wamepangiwa vituo mbalimbali vya kazi. Saili hizo zilifanyika katika Kanda tano (5) ambazo ni Kanda ya Mashariki (Dar es Salaam), Kanda ya Ziwa (Mwanza), Kanda ya Kati (Dodoma), Kanda ya Kaskazini (Arusha, Kilimanjaro na Tanga), Kanda ya Nyanda za Juu Kusini (Mbeya na Iringa) na Kituo Maalum kimoja (1) - Zanzibar;

iv. Usaili wa ajira za muda kwa niaba ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) ulisimamiwa kwa nafasi za wasimamizi wa maudhui, wasimamizi wa TEHAMA na makarani wa Sensa

ambapo jumla ya maombi 689,935 yalipokelewa na waombaji 612,023 waliitwa kwenye usaili, kati ya hao waombaji 205,000 walifaulu na kupangiwa vituo vya kazi;

v. Maboresho ya Kanuni za Sekretarieti ya Ajira yalifanyika ambapo uhai wa kanzidata umeongezwa kutoka miezi sita (6) hadi miezi 12 na kuweka ukomo wa juu wa miezi tisa (9) wa muda wa adhabu kwa msailiwa aliyebainika kufanya udanganyifu wakati wa usaili. Aidha, Muda wa kutoa matangazo umeboreshwa na kuwa kati ya siku saba (7) na 21;

vi. Huduma ya utatuzi wa hoja za wadau na msaada kwa watumiaji wa mfumo wa '*Ajira Portal*' ulitolewa, ambapo kati ya Julai na Machi, 2023 jumla ya wadau 9,389 walihudumiwa. Kati ya hao, wadau 6,014 walihudumiwa kwa njia simu, wadau 1,242 walihudumiwa kwa kufika ofisini na wadau 2,133 walihudumiwa kwa njia ya barua pepe;

vii. Mfumo wa Maombi ya Kazi kwa Njia ya Simu (Ajira *Portal Mobile App*) umeboreshwa ili kuongeza kasi ya upatikanaji na kurahisisha matumizi. Hadi kufikia Machi, 2023 Ajira App ilikuwa imepakuliwa na zaidi ya watumiaji 80,000 na kushika nafasi ya pili miongoni mwa *Mobile App* zinazotumiwa zaidi nchini katika kundi la magazeti na majarida;

viii. Usanifu umekamilishwa na ujenzi unaendelea kwa mfumo wa usaili wa kuandika kwa njia ya mtandao "***Online Aptitude Testing System***" ambao unalenga kupima uelewa na ufahamu wa wasailiwa. Mfumo huu utawezesha usaili kufanyika katika ngazi ya Wilaya na hivyo kuwapunguzia wasailiwa gharama za usafiri, malazi na chakula kwa kuwa usaili utafanyika katika maeneo wanakotoka; na

ix. Ujenzi wa mfumo wa kupima haiba za wasailiwa **"*Psychometric Testing System*"** umeanza kwa kukusanya maoni ya watumiaji (*user requirements*). Mfumo huu utaiwezesha Serikali kutambua haiba na tabia za waombaji kazi kwa lengo la kuwasaidia waajiri kubaini maeneo ya kuwajengea uwezo waajiriwa wapya.

**OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

***42. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 5,981,827,000.00.** Kati ya kiasi hicho, **shilingi 5,681,824,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 300,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***43. Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi, 2023 **Shilingi 4,397,319,957.17** sawa na asilimia **73.5** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,097,324,957.17** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 299,995,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

***44. Mheshimiwa Spika*,** katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 hadi Machi 2023, Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

i. Mikutano mitatu (3) kati ya minne (4) ya kisheria ya Tume imefanyika na kufanyia maamuzi rufaa 323 sawa na asilimia 53.5 kati ya rufaa 604 zilizokuwa na vielelezo. Hadi kufikia Machi, 2023 kulikuwa na jumla ya rufaa 764 ambapo rufaa 50 uchambuzi wake ulikamilika, rufaa 247 zilikuwa zinaendelea kuchambuliwa na ufuatiliaji wa vielelezo vya rufaa 144 ulikuwa unaendelea kutoka kwa mamlaka husika;

ii. Malalamiko 37 kati ya jumla ya malalamiko 59 yenye vielelezo, sawa na asilimia 62.7 yameshughulikiwa na kuyatolea maamuzi. Aidha, malalamiko 71 yalitolewa ufafanuzi na kuhitimishwa na Sekretarieti. Jumla ya

malalamiko yaliyoshughulikiwa ni 108 kati ya malalamiko 168 yaliyokuwepo sawa na asilimia 64.3. Kati ya malalamiko 60 yaliyobaki 28 yanaendelea kuchambuliwa na malalamiko 32 yanasubiri vielelezo kutoka kwa mamlaka husika;

iii. Maulizo 1,492 ya watumishi wa Umma, waajiri, mamlaka za ajira na Mamlaka za nidhamu kuhusu rufaa na malalamiko yamepokelewa na kushughulikiwa;

iv. Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume katika Mji wa Serikali Mtumba unaendelea na upo katika hatua ya ujenzi wa msingi;

v. Ukaguzi wa uzingatiaji wa sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma kwa taasisi 104 umekamilishwa kati ya 150 zilizopangwa. Kati ya taasisi hizo, Serikali Kuu ni 29, Mamlaka za Serikali za Mitaa ni 44 na Taasisi za Umma ni 31. Aidha, Ukaguzi kwa Taasisi 46 zilizobaki unaendelea;

vi. Miongozo mitatu (3) ambayo ni: Mwongozo wa Masuala ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Mwongozo wa Nidhamu, Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma; na Mwongozo wa Uwasilishaji wa Taarifa Tume imehuishwa. Aidha, miongozo miwili (2) ambayo ni Mwongozo wa Nidhamu, Rufaa na Malalamiko katika Utumishi wa Umma na Mwongozo wa Uwasilishaji wa Taarifa Tume umewasilishwa katika Mkutano wa Tume na kupata ridhaa ya kuanza kutumika;

vii. Miongozo mipya miwili (2) ya ndani (*Internal Guidelines*) ambayo ni Mwongozo wa Uchambuzi wa Rufaa na Malalamiko na Mwongozo wa Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Utumishi wa Umma imeandaliwa na

kuwasilishwa kwenye Mkutano wa Tume na kupata ridhaa ya kuanza kutumika;

viii. Maboresho ya Mfumo wa Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika usimamizi wa Utumishi wa Umma yamefanyika kwenye maeneo sita (6) yaliyokaguliwa awali. Aidha, maeneo mapya saba (7) ya kukaguliwa yalianzishwa kwa lengo la kuongeza tija na kupata uwanda mpana zaidi wa kuishauri Serikali kuhusu viwango vya uzingatiaji katika usimamizi wa masuala ya Kiutumishi;

ix. Mafunzo kwa watumishi wa Umma katika taasisi 28 yametolewa kuhusu uzingatiaji wa sheria katika masuala ya kiutumishi. Kati ya Taasisi hizo, Serikali Kuu zilikuwa nane (8), Taasisi za Umma yalikuwa 13 na Mamlaka za Serikali za Mitaa zilikuwa saba (7).

x. Elimu kuhusu uzingatiaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 (Marejeo ya Mwaka 2019) imetolewa kupitia vipindi sita (6) vya Televisheni za TBC 1, Star TV, Channel 10 na AZAM TV na vipindi vitano (5) vya Redio za Magic FM, TBC Taifa na 92.6 AFM Dodoma. Vilevile, elimu imetolewa kuhusu uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Utumishi wa umma kwa wadau 1,250 waliotembelea banda la Tume kwenye maadhimisho ya Siku ya Maadili na Haki za Binadamu ambapo vipeperushi 650 kuhusu maudhui hayo vilisambazwa;

xi. Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume katika kipindi cha mwaka 2021/2022 imeandaliwa na kuwasilishwa kwa Mamlaka;

xii. Taarifa ya Ukaguzi wa Uzingatiaji wa Sheria katika Usimamizi wa Utumishi wa Umma kwa Mwaka 2021/2022 uliofanyika katika Taasisi za Serikali 110 imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye Mamlaka; na

xiii. Ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Rufaa na Ukaguzi umetekelezwa kwa hatua nne (4) kati ya saba (7) ambazo ni: Mapitio ya taratibu za ufanyaji kazi (Business Process Review), Uainishaji wa mahitaji ya mfumo (Establishment of System Requirement), Uainishaji wa Vigezo wa mfumo (Establishment of System Specification), na Usanifu wa mfumo (System Design);

**OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

***45. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2022/23, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa iliidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,914,791,000.00.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,504,791,000.00** ni kwa ajili matumizi ya kawaida na **shilingi 1,410,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

***46. Mheshimiwa Spika,*** Hadi kufikia Machi, 2023 jumla ya **shilingi 3,209,351,423.86** zilipokelewa ambapo kati ya fedha hizo **shilingi 1,809,514,464.41** ni matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 51.63** na **shilingi 1,399,836,959.45** ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na **asilimia 99.28**.

***47. Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa imetekeleza majukumu yafuatayo:

i. Jumla ya nyaraka 2,963 zimekusanywa kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 kati ya 45 na Taasisi za Umma 11 kati ya 15 zilizopangwa;

ii. Majalada 3,933 yaliyofungwa yamekusanywa na kuyahifadhi katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu – Dodoma ambapo kati ya majalada hayo, majalada 3,600 ni ya Mashauri yaliyofungwa kutoka Mahakama Kuu

ya Tanzania na majalada 333 kutoka Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi;

iii. Jumla ya nyaraka 165 za Waasisi wa Taifa (Mwl. Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume) zimekusanywa na kuhifadhiwa. Aidha, Idara imeweza kutambua na kusajili kumbukumbu za Muasisi wa Taifa (Mwl.Julius Kambarage Nyerere) kutoka katika Shule ya Wavulana Tabora mahali ambapo alisoma na kuhitimu masomo yake ya Sekondari 1942. Pia kutambua kumbukumbu na vitu husika katika Shule ya Sekondari *St. Marry's* Mihayo ambayo inamilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora (Shule ambayo Mwalimu Julius K. Nyerere alifundisha kabla ya kwenda Masomoni nje ya nchi). Kutambua na kusajili Mnara wa Kura Tatu uliowekwa katika Soko Kuu Tabora kama kumbukumbu ya uamuzi wa busara wa kushiriki uchaguzi wa kura tatu uliofanywa na Mkutano Mkuu wa TANU Januari 1958;

iv. *Video Documentary* kuhusu maisha binafsi na harakati za kisiasa za Mwalimu Julius Kambarage Nyerere akiwa mwanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Wavulana Tabora imeandaliwa. Vilevile, imefanyika akiwa Mwalimu katika Shule ya Sekondari *St. Marry's* Mihayo inayomilikiwa na Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora. Waliofanyiwa mahojiano katika *Video Documentary* hiyo ni pamoja na Askofu Mkuu, Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Tabora, Uongozi wa Shule Sekondari ya Wavulana Tabora, St. *Marry's* Mihayo Sekondari pamoja na baadhi ya wanafunzi katika shule husika;

v. Maboresho ya Mfumo wa Ofisi Mtandao (*e-Office Management System*) yamefanyika kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) pamoja na kuwajengea uwezo Maafisa Rasilimaliwatu, Maafisa

Kumbukumbu, Wasaidizi wa Kumbukumbu na Maafisa TEHAMA kutoka taasisi za Umma 129;

vi. Uwekaji wa Mfumo wa Masijala Mtandao (*e-Office Management System*) katika taasisi za Umma 16 umekamilishwa kati ya 30 zilizopangwa;

vii. Uwekaji wa Mfumo wa Utunzaji wa Kumbukumbu za Kiutendaji (*Keyword Filing System*) katika taasisi za Umma 27 umekamilishwa kati ya 30 zilizopangwa;

viii. Ukaguzi wa hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma 58 umekamilishwa kati ya 70 zilizopangwa kwa lengo la kujua hali halisi ya utunzaji wake ili kubaini changamoto wanazokabiliana nazo na kuzipatia ufumbuzi;

ix. Tathmini ya idadi na elimu ya watumishi wa masijala katika taasisi za Umma 20 umekamilishwa kwa lengo la kujua idadi ya watumishi na elimu zao kwa ajili ya kufanya msawazo katika mamlaka zao za ajira;

x. Tathmini (*appraisal*) ya majalada 126,738 ya Mahakama ya Tanzania umekamilishwa ambapo kati ya hayo majalada 2,370 yalibainika kuwa na umuhimu wa kutunzwa daima (*records for permanent preservation*) na majalada 124,368 yalibainika kufikia ukomo wa mahitaji yake kwa mujibu wa Sheria;

xi. Uwezeshaji wa utengenezaji wa Miongozo ya utunzaji na uteketezaji kumbukumbu katika taasisi za Umma saba (7) umekamilishwa kati ya taasisi 10 zilizopangwa. Taasisi hizo ni: Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi (PSPDB); Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA); Shirika la

Wakala wa Meli Tanzania (TASAC); Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA); Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE); Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART); na Wizara ya Maliasili na Utalii;

xii. Uwekaji wa majalada 1,873 kwenye mfumo wa kidigitali (*Digital Records Management and Preservation System*) umekamilishwa kati ya majalada 2,500 kwa lengo la kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi ili ziweze kudumu kwa muda mrefu;

xiii. Mashubaka 683 yamenunuliwa kwa ajili ya kuhifadhia nyaraka katika Kituo cha Kumbukumbu Kanda ya Ziwa – Mwanza;

xiv. Utoaji mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu katika taasisi za Umma 25 ukamilishwa kwa lengo la kuwajengea uwezo kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali na;

xv. Watumishi wanne (4) wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo mbalimbali kwa lengo la kuwaongezea ujuzi. Kati ya hao, mtumishi moja (1) amewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu katika Shahada ya Uzamili na watumishi watatu (3) walipata mafunzo ya muda mfupi.

**MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/24 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

***48. Mheshimiwa Spika****,* Mpango na Bajeti kwa mwaka 2023/24 umeandaliwa kwa kuzingatia, Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020, Mpango wa Tatu wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26), wenye dhima ya Tanzania kuwa na Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu na

Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan akihutubia Bunge Aprili 2021. Miongozo hii ni nguzo muhimu ya mpango unaotarajiwa kutekelezwa kwa mwaka 2023/24. Shughuli zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

**OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE**

**A. OFISI YA RAIS – IKULU**

***49. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kuendelea kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

ii. Kuwezesha ratiba ya kila siku ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

iii. Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

iv. Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

v. Kuandaa mikutano miwili (2) ya tathmini ya mwaka kati ya waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

vi. Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa

maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri;

vii. Kuchambua na kutoa ushauri kwa Katibu Mkuu Kiongozi katika masuala ya kitaifa na kimataifa hususani masuala ya uchumi, jamii, sheria, ulinzi, usalama, na masuala mengine yote yatakayowasilishwa;

viii. Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

ix. Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Binafsi;

x. Kupokea na kuchambua taarifa za robo mwaka za utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Programu nyingine za maboresho;

xi. Kuendelea kujenga uwezo wa taasisi za umma kuhusu uzingatiaji wa utawala bora katika kutoa huduma kwa umma;

xii. Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa programu za maboresho katika ngazi za utekelezaji;

xiii. Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa 300 na malalamiko 400 ya watumishi wa umma na wananchi;

xiv. Kuendesha mikutano mitatu (3) ya watendaji na maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja na kufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

xv. Kufanya ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma yanayohusu masuala ya usimamizi wa utawala wa Utumishi kwenye Wizara, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

xvi. Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

xvii. Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino kwa kuanza ujenzi wa ukumbi wa mikutano (Multi Purpose Hall) na baadhi ya ofisi;

xviii. Kuendelea na ukarabati wa Ikulu Ndogo ya Tunguu-Zanzibar;

xix. Kuanza ujenzi wa jengo jipya la makazi katika Ikulu Ndogo ya Arusha; na

xx. Kuendelea na ukarabati majengo ya Ikulu Ndogo za Mwanza, Tabora, Moshi, Shinyanga na Lushoto.

**B. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)**

***50. Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2023/24, TAKUKURU imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya utafiti na uchambuzi wa mifumo ya kiutendaji na utoaji huduma katika sekta za umma na binafsi ili kubaini maeneo yenye mianya ya rushwa na kushauri namna ya kuziba mianya hiyo;

ii. Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji unazingatia thamani halisi ya fedha;

iii. Kuendelea kutekeleza mpango wa TAKUKURU RAFIKI ili kuwashirikisha wadau wengi zaidi kwenye kuzuia na kupambana na rushwa;

iv. Kufanya vikao kazi vya kuwashirikisha wadau kuweka mikakati ya kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo

v. Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kwa kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;

vi. Kuendelea kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kupambana na rushwa;

vii. Kuendelea kushirikisha umma katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kuandaa ajenda zenye maudhui ya mapambano hayo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii;

viii. Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;

ix. Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura 329;

x. Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na

xi. Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuwajengea umahili wa utendaji kazi na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Taasisi.

## C. TAASISI YA UONGOZI

***51. Mheshimiwa Spika***, Taasisi ya UONGOZI itaendelea kujengea uwezo viongozi ili kuongeza tija katika utekelezaji wa kazi kwa kupitia mafunzo na semina. Katika mwaka 2023/24, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kufanya tafiti tumizi sita (6) kuhusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ili kutoa ushauri wa kisera kwenye masuala muhimu yanayohusu maendeleo ya nchi ikiwemo maendeleo ya Nne ya Viwanda (Artificial Intelligence) na mabadiliko ya tabianchi;

ii. Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa bodi 100 za Mashirika ya Umma, taasisi za umma na Wakala za Serikali kwa lengo la kuimarisha usimamizi na utendaji. Mafunzo haya yatahusu uongozi wa kimkakati, usimamizi wa Mashirika ya Umma, usimamizi wa rasilimali za umma na rasilimaliwatu na usimamizi wa viashiria hatarishi;

iii. Kuandaa tawasifu inayoelezea maisha ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa, aliyekuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuweka kumbukumbu za viongozi mashuhuri wa Taifa letu katika maandishi;

iv. Kutekeleza programu maalum ya mafunzo ya uongozi kwa wanawake viongozi waandamizi na viongozi wanaochipukia 50 kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, usimamizi wa rasilimali za Serikali na rasilimaliwatu. Mafunzo haya yanalenga kukuza vipaji vya uongozi kwa viongozi wanawake wanaochipukia. Mada zitakazotolewa zinajumuisha: akili hisia; sanaa ya uongozi; itifaki; utaalamu na taswira ya kiongozi mwanamke; kuoanisha majukumu ya nyumbani na kazi; muundo wa Serikali na mawasiliano; maadili ya uongozi; masuala ya jinsia; mawasiliano na mbinu za majadiliano; uchambuzi wa kimkakati na jinsi ya kufanya maamuzi; viashiria hatarishi na udhibiti wa mifumo ya ndani; uchambuzi wa kifedha; uandishi wa taarifa; na matumizi bora ya muda;

v. Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 35 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine ili kuongeza tija;

vi. Kutoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi kwa njia ya mtandao kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 65 katika maeneo ya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine, matumizi ya takwimu (*data analytics*);

vii. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 40 kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi 1,200 katika maeneo ya uongozi na maendeleo endelevu kwa ajili ya kuimarisha utendaji wao kwa kuzingatia mahitaji na maombi ya walengwa;

viii. Kuandaa mikutano minne (4) ya kitaifa na miwili (2) ya kimataifa katika masuala ya uongozi kwa viongozi 460 kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

ix. Kuandaa vipindi vinne (4) vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, juu ya uongozi na maendeleo endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao ya kijamii na kuonekana katika bara zima la Afrika;

x. Kutoa ushauri wa kitaalam kwa taasisi tano (5) za Serikali katika maeneo yanayohusu masuala ya uongozi na maendeleo endelevu;

xi. Kufanya tathmini ya muda wa kati wa Mpango Mkakati wa mwaka 2021/22 - 2025/26 ili kuweza kupima ufanisi na matokeo ya kazi zitakazotekelezwa;

xii. Kutoa machapisho 11 juu ya masuala ya uongozi na maendeleo endelevu ikiwemo Tawasifu ya Hayati Edward Moringe Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Awamu ya Kwanza; na

xiii. Kukamilisha maandalizi ya ujenzi wa kituo cha mafunzo katika Kijiji cha Kondo, Bagamoyo. Ujenzi wa kituo hiki utafanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia utaratibu wa *Public Private Partnership* (PPP). Aidha, Taasisi itaandaa Mpango Kazi na michoro ya majengo na kuanza awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la ofisi jijini Dodoma.

## D. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

***52. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, TASAF imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kufanya zoezi la kuhakiki na kutambua hali za ustawi wa maisha ya kaya za walengwa wa Mpango zipatazo 380,000 iwapo zimeimarika kiuchumi kwa kutumia vigezo vya umaskini na utaratibu uliokubaliwa kitakwimu kwenye maeneo yote ya utekelezaji 186. Zoezi hili litatoa fursa ya kubainisha kaya zilizoimarika kiuchumi;

ii. Kuendelea kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini 972,603 zinazokidhi vigezo vya Mpango;

iii. Kuwezesha utekelezaji wa miradi ya jamii ya kutoa ajira ya muda kwa kaya za walengwa katika mamlaka za utekelezaji 153. Jumla ya miradi 13,000 ya jamii na ya kutoa ajira za muda itatekelezwa katika ngazi ya Vijiji/Mitaa/Shahia na inategemewa kutoa ajira za muda kwa walengwa 400,000;

iv. Kuwezesha jamii kutekeleza miradi ya kuendeleza miundombinu ya huduma za jamii katika sekta mbalimbali. Jumla ya miradi 550 itatekelezwa katika Vijiji/Mitaa/shehia katika sekta za afya, elimu, maji, mazingira na ujasiriamali. Aidha, wafanyakazi 120 wa halmashauri watapewa mafunzo juu ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi hiyo;

v. Kuwezesha uundaji wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza katika mamlaka za utekelezaji 67 ambapo jumla ya vikundi 16,000 vya jamii vinatarajiwa kuundwa na kuwawezesha walengwa kuanzisha shughuli za kiuchumi na kaya zilizofikia hatua hiyo kupatiwa ruzuku ya kuboresha biashara zao. Aidha, mafunzo kwa wawezeshaji 2,010 yatatolewa katika maeneo husika

kuhusu uundaji wa vikundi vya kuweka akiba na kuwekeza;

vi. Kuongeza maeneo ya utekelezaji 39 yatakayoshiriki malipo kwa njia ya mtandao;

vii. Kuongeza mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na benki) kwenye maeneo yote ya utekelezaji 186. Njia hii ya malipo itawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa walengwa wengi na kuwafikia kwa haraka. Aidha, mifumo ya habari, mawasiliano, uendeshaji na utoaji taarifa wa shughuli za Mpango katika maeneo ya utekelezaji wa TASAF Makao Makuu utaendelea kuimarishwa na kuboreshwa;

viii. Kufanya tathmini na ufuatiliaji wa shughuli za Mpango ili kuona ni kwa kiwango gani malengo ya Mpango yanafikiwa, kubainisha changamoto na kuzishughulikia ili kuboresha utendaji kazi na matokeo ya Mpango yanayotarajiwa; na

ix. Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango.

**E. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI**

***53. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa;

ii. Kuratibu ununuzi pamoja na kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Tanzania (ATCL);

iii. Kulipia gharama za bima za ndege pamoja na wanaanga;

iv. Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na

v. Kutoa mafunzo ya kisheria kwa wanaanga kwa ajili ya kuhuisha leseni zao.

***54. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Ikulu: Fungu 20 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 32,157,384,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri: Fungu 30 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 860,186,476,000.00** kati ya fedha hizo, **shilingi 678,193,941,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 80,598,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 101,394,535,000.00** fedha za nje.

**SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA**

***55. Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaendelea na vipaumbele vikuu viwili (2) ambavyo ni kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma kwa taasisi na wananchi ili kuweza kuwafikia kwa urahisi; na kuimarisha uwajibikaji wa pamoja miongoni mwa viongozi wa umma hasa katika suala la viongozi kukinzana kunakosababisha shughuli za maendeleo kutotekelezeka kwa wakati. Kada za viongozi zitakazojumuishwa katika eneo hili ni pamoja na Wakuu wa Idara na Madiwani kutoka katika halmashauri ambazo hazijafikiwa na kupatiwa mafunzo husika. Kupitia vipaumbele hivyo shughuli zifuatazo zimepangwa kutekelezwa:

i. Kupokea Tamko la Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na Madeni linalopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

ii. Kupokea malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa Maadili kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma kutoka kwa wananchi;

iii. Kuchunguza tuhuma yoyote ya kuvunjwa kwa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

iv. Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 820;

v. Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

vi. Kuelimisha Viongozi wa Umma na Wananchi kwa ujumla kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma, Hati ya Ahadi ya Uadilifu na Uwajibikaji wa pamoja;

vii. Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

viii. Kuendeleza na kuanzisha Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini; na

ix. Kuendeleza ujenzi wa Ofisi ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Ziwa pamoja na kuanza ujenzi kwa Kanda za Kaskazini na Mashariki.

***56. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma: Fungu 33 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 12,763,016,000.00** Kati ya fedha hizo, **shilingi 10,813,016,000.00** ni matumizi ya kawaida na

**shilingi 1,500,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 450,000,000.00** fedha za nje.

**OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE**

**A. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA**

***57. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kujenga uwezo wa watumishi na taasisi za umma kuhusu namna ya kutumia Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji Kazi wenye moduli mbili (2) za Public Employee's Performance Management Information System (PEPMIS) na Public Institution Performance Management Information System (PIPMIS) katika Utumishi wa Umma. Utekelezaji utahusisha kufundisha wakufunzi/wawezeshaji 94 wa kuwezesha watendaji wa taasisi za Umma kuanza utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi;

ii. Kujenga uwezo wa taasisi za umma kuanza kutekeleza Mfumo Mpya wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma katika taasisi za umma 215 (wizara 26, sekretarieti za mikoa 26, mashirika na taasisi za umma 70 na mamlaka za serikali za mitaa 93);

iii. Kuandaa Sera za Mifumo ya TEHAMA na taarifa za kielektroniki Serikalini kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa Serikali Mtandao;

iv. Kujenga mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kusimamia na kuratibu ukopaji na uuzaji wa magari chakavu ya Serikali, kusimamia na kuratibu fursa za mafunzo na vibali vya ajira

za wataalam wa kigeni katika utumishi wa Umma na mfumo kwa ajili ya maktaba ya OR-MUUUB (e-Library);

v. Kusimamia na kuendelea kuboresha mifumo ya HCMIS, PEPMIS, PIPMIS, HR Assessment, e-HRP, na Watumishi Portal ili kuendana na mahitaji ya watumiaji na mabadiliko ya teknolojia;

vi. Kujenga toleo la aplikesheni ya simu za mkononi kwa ajili ya mifumo ya PEPMIS, PIPMIS na Watumishi Portal;

vii. Kuchambua malalamiko ya masuala ya rasilimaliwatu katika utumishi wa Umma yanayotokana na uvunjwaji wa Sheria, Taratibu, Kanuni na Miongozo mbalimbali na kufuatilia utekelezaji wa utatuzi wake;

viii. Kufuatilia uzingatiaji wa Mkakati wa Serikali Mtandao wa mwaka 2022, Mkakati wa Usalama wa Mtandao wa Serikali wa mwaka 2022 na Mwongozo wa Matumizi Bora, Salama na Sahihi ya Mifumo ya TEHAMA, Data na Vifaa vya TEHAMA wa mwaka 2022;

ix. Kuratibu utekelezaji wa Mradi wa Tanzania ya Kidigitali katika kuongeza masafa (government internet bandwith), kuongeza taasisi za umma zilizounganishwa kwenye mtandao wa Serikali, kuendeleza uanzishwaji wa vituo vya Huduma Pamoja na kuongeza uwezo wa Serikali katika kuhifadhi mifumo ya Serikali Mtandao katika vituo salama;

x. Kujenga uelewa kuhusu taratibu za nidhamu na kutoa misaada ya kisheria kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali inayosimamia Utumishi wa Umma

kwenye Wizara, Idara, Wakala, Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Taasisi mbalimbali za Umma kadiri ya uhitaji;

xi. Kufanya mapitio ya Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali;

xii. Kufanya mapitio ya miundo na mgawanyo wa majukumu ya taasisi mbalimbali za umma na uchambuzi wa mahitaji ya watumishi kwa kada mbalimbali kadri itakavyojitokeza;

xiii. Kuzijengea uwezo Taasisi za umma kuhusu uandaaji wa mipango ya motisha kwa watumishi wa umma na kutoa ushauri wa kitaalamu katika uandaaji na uhuishaji wa miundo ya maendeleo ya utumishi;

xiv. Kuchambua takwimu za kiuchumi na kuandaa taarifa ya gharama za maisha kwa lengo la kupendekeza mishahara inayowezesha watumishi wa umma kumudu gharama za maisha;

xv. Kufanya tafiti juu ya mazingira ya kazi ili kupendekeza motisha kwa lengo la kuwavutia na kuwabakiza watumishi wanaofanya kazi katika maeneo yenye mazingira magumu katika Utumishi wa Umma;

xvi. Kuendelea kutumia mikakati mbalimbali ya mawasiliano inayojumuisha vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa ajili ya kuuhabarisha Umma juu ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

xvii. Kuandaa maadhimisho ya Wiki ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kupata mrejesho kutoka kwa wadau na

kutatua changamoto mbalimbali zitakazojitokeza katika Utumishi wa Umma;

xviii. Kufanya kampeni za kimaadili katika taasisi za Umma na ufuatiliaji wa uzingatiaji wa maadili;

xix. Kujenga uwezo kwa maafisa malalamiko 100 na watumishi wa Umma waandamizi 300 kutoka katika taasisi za Umma 120 katika matumizi ya Mfumo wa e-Mrejesho;

xx. Kushughulikia vibali vya ajira ili kujaza nafasi 43,464 zilizoidhinishwa katika Ikama;

xxi. Kuhakiki na kuidhinisha madai ya malimbikizo ya mishahara na kusahihisha taarifa (Data Cleaning) zinazohusiana na masuala ya kiutumishi na mishahara ya watumishi kwa taasisi 433;

xxii. Kukagua Orodha ya Malipo ya Mshahara katika taasisi 150;

xxiii. Kutoa mafunzo ya matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) kwa watumishi 640 kwa ngazi tofauti ili kuwajengea uwezo wa kutoa huduma bora;

xxiv. Kuwezesha taasisi 50 kutumia Mfumo wa HCMIS na kufanya ufuatiliaji na tathmini kwa Taasisi zilizoingizwa katika Mfumo;

xxv. Kufanya tathmini ya utendaji kazi ya Wakala za Serikali 27;

xxvi. Kukamilisha Kiunzi cha Mpango wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma na Mwongozo wa Kuandaa Mpango wa Mafunzo katika Taasisi za Umma;

xxvii. Kuzijengea uwezo Taasisi za Umma ili kuandaa na kutekeleza Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Mafunzo na Mipango ya Urithishanaji Madaraka;

xxviii. Kuratibu utoaji wa vibali vya kazi na ukaazi kwa wataalam wa kigeni wanaokuja kufanya kazi katika Sekta ya Umma nchini;

xxix. Kuratibu fursa za mafunzo zinazotolewa na Wadau wa Maendeleo katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia malengo ya Dira Taifa ya mwaka 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III);

xxx. Kuendelea kuratibu ajira za wataalam wazawa katika Taasisi za Kikanda na Kimataifa;

xxxi. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi la ghorofa tano (5) katika eneo la Mtumba na Klabu ya Viongozi – Dodoma;

xxxii. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa; na

xxxiii. Kuendelea kutoa huduma kwa Viongozi wa Kitaifa Wastaafu (Viongozi 11 na wajane nane (8)) kwa mujibu wa sheria.

## B. CHUO CHA UTUMISHI WA UMMA (TPSC)

***58. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC) kimepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kutoa mafunzo ya uongozi na maendeleo, menejimenti na usimamizi wa ofisi kwa watumishi wa umma 5,260 katika maeneo 25 na watumishi 2,300 kwa njia ya mtandao kwa ajili ya kuendeleza stadi, weledi na ujuzi;

ii. Kutoa mafunzo ya awali katika utumishi wa umma kwa watumishi 3,400 kwa ajili ya kujenga uelewa wa kiutendaji serikalini kwa waajiriwa wapya;

iii. Kutoa ushauri elekezi katika maeneo 16 ya kitaalam kwa taasisi za Umma kwa ajili ya kutambua changamoto halisi za utendaji na kuchangia katika utoaji wa maamuzi yanayozingatia matokeo ya utafiti;

iv. Kufanya tafiti tumizi 10 katika utumishi wa umma zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi;

v. Kuendelea na ujenzi wa majengo yatakayotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi za Singida; na

vi. Kuboresha Kampasi ya Tabora ili iweze kutoa huduma bora katika ufundishaji wa kozi za uhaziri.

## C. MAMLAKA YA SERIKALI MTANDAO (e-GA)

***59. Mheshimiwa Spika***, Katika mwaka 2023/24, Mamlaka ya Serikali Mtandao imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kusimamia na kutathmini hali ya usalama wa mifumo na miundombinu ya TEHAMA, hatimaye kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake ili kuhakikisha inafanya kazi na kutoa huduma kwa taasisi za umma na wananchi wakati wote;

ii. Kuendelea kuiunganisha mifumo ya taasisi za Umma kwenye Mfumo wa kuwezesha Mifumo ya Serikali

kuwasiliana na kubadilishana taarifa (*Government Enterprise Service Bus* - GovESB);

iii. Kuongeza wigo wa miundombinu ya mtandao wa mawasiliano serikalini (*Government Network*) ili kuifikisha katika wilaya zote nchini na kuziwezesha taasisi nyingi zaidi kuwafikishia huduma wananchi kupitia mtandao;

iv. Kufanya maboresho na kuihusisha mifumo ya TEHAMA shirikishi, mifumo ya kisekta na mifumo ya kitaasisi inayotumika ili iweze kuendelea kutoa huduma kwa ufanisi na usalama zaidi;

v. Kufanya uchambuzi, usanifu na ujenzi wa mifumo mipya ya kisekta kwa taasisi zenye taratibu za utendaji kazi zinazoendana kwa lengo la kuboresha utoaji huduma na kupunguza wingi wa Mifumo ya TEHAMA Serikalini;

vi. Kumalizia ujenzi na kuanza matumizi ya mfumo mkuu wa Ununuzi wa Umma (NeST) kwa kushirikiana na PPRA;

vii. Kujenga mfumo wa pamoja wa ankara mbalimbali *(Universal Billing System)* kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango;

viii. Kushirikiana na Wizara ya Ardhi kuendelea kujenga mfumo mpya jumuishi wa usimamizi wa huduma za ardhi;

ix. Kuboresha huduma za Serikali Mtandao kwenye Halmashauri na Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na TAMISEMI;

x. Kushirikiana na Taasisi husika katika kukamilisha mifumo ya pamoja kama vile Single Window (TPA/TRA), TIPS (BOT), New LUKU (TANESCO);

xi. Kusimamia uzingatiaji wa sera, sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Serikali Mtandao katika matumizi ya TEHAMA serikalini na taasisi zake. Hii ni pamoja na, kukagua mifumo ya kimkakati, kisekta na kitaasisi ili kuhakikisha kuwa imetengenezwa na inatumika kwa kufuata sheria, kanuni, viwango na miongozo iliyopo na kushauri maeneo ya kuboresha na kufuatilia utekelezaji wake;

xii. Kuendeleza utafiti na ubunifu katika matumizi ya teknolojia mpya za TEHAMA ili kuibua huduma mpya kwa Umma kupitia TEHAMA na kuwezesha matumizi sahihi ya teknolojia mpya zinazoibuka;

xiii. Kusimamia, kuendesha na kuendeleza mifumo na miundombinu shirikishi ya TEHAMA ya Serikali na Taasisi zake, mtandao wa mawasiliano katika mji wa Serikali Mtumba pamoja na kusimamia na kuboresha vituo vya kuhifadhi mifumo na taarifa za Serikali na vituo vya kujikinga na majanga;

xiv. Kuwajengea uwezo watumishi katika kusimamia mifumo na miundombinu ya TEHAMA katika taasisi za Umma pamoja na kutoa mafunzo kwa watumiaji kuhusu matumizi sahihi na salama ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA; na

xv. Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwenye maeneo ya TEHAMA kwa taasisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa viwango na miongozo inafuatwa, na kuwa na matumizi ya TEHAMA yenye tija na kupunguza gharama.

**D. WATUMISHI HOUSING INVESTMENT (WHI)**

***60. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Watumishi Housing Investment imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:

i. Kuendeleza mradi wa ujenzi wa nyumba 1,000 jijini Dodoma pamoja na mikoa mingine;

ii. Kutekeleza ujenzi wa nyumba 80 za Mradi wa Makazi kwa Watumishi wa Umma Wilayani hususan katika wilaya mpya;

iii. Kukuza Mfuko wa Faida ufikie thamani ya shilingi bilioni 30 ifikapo tarehe 30 Juni 2024; na

iv. Kuuza viwanja 226 kati ya viwanja 326 vilivyopimwa USA RIVER Jijini Arusha.

***61. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi 69,317,460,000.00.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 57,130,005,000.00** ni matumizi ya kawaida na **shilingi 12,070,200,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa fedha za ndani na **shilingi 117,255,000.00** fedha za nje.

**SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

***62. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuwezesha kupatikana wataalam katika Utumishi wa Umma katika maeneo ya vipaumbele kama ifuatavyo:-

i. Kuendesha na kusimamia michakato ya ajira kwa ajili ya kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

ii. Kushiriki kama wataalam waalikwa kwenye saili zinazoendeshwa na taasisi zinazotumia sheria zilizokasimiwa kwa taasisi husika;

iii. Kuendelea kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira Zanzibar kwa ajili ya kuwezesha michakato ya ajira za Muungano;

iv. Kuelimisha Umma kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwa ajili ya kukuza uelewa;

v. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi za Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma Jijini Dodoma;

vi. Kuongeza uwezo wa Taasisi kufanya usaili kwa kuongeza vituo vya usaili katika kanda na mikoa;

vii. Kuendelea kuboresha mifumo ya usaili kwa njia ya TEHAMA;

viii. Kuendelea kuboresha mfumo wa usaili wa kuandika kwa njia ya mtandao "**Online Aptitude Testing System**";

ix. Kuendelea na ujenzi wa mfumo wa kupima haiba za wasailiwa "**Psychometric Testing System**"; na

x. Kuendelea na ujenzi wa maabara ya kompyuta kwa ajili ya uendeshaji wa saili za vitendo kwa kada za TEHAMA.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma fungu 67 inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 13,711,815,000.00**. Kati ya fedha hizo **shilingi 10,139,298,000.00** ni matumizi ya

kawaida na **shilingi 3,572,517,000.00** ni fedha za miradi ya maendeleo.

**TUME YA UTUMISHI WA UMMA (PSC)**

***64. Mheshimiwa Spika*,** Majukumu yaliyopangwa kutekelezwa na Tume kwa mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:-

i. Kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi za Umma 180 na Ukaguzi Maalum katika taasisi za Umma 10 kwa ajili ya kubainisha uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

ii. Kufanya mikutano minne (4) ya kisheria ya Tume kwa ajili ya kujadili na kutolea uamuzi rufaa, malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

iii. Kuandaa rejea ya Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali kuhusu masuala ya ajira na nidhamu katika utumishi wa Umma na kuisambaza kwa waajiri, mamlaka za ajira na nidhani;

iv. Kujenga uwezo kwa washiriki 1,500 kutoka Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uzingatiaji wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa Umma;

v. Kuelimisha taasisi za Umma na watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utumishi wa Umma kupitia ziara za viongozi, vikao kazi, vyombo vya habari, machapisho na tovuti;

vi. Kuandaa taarifa ya hali ya utumishi wa Umma na utekelezaji wa majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka 2022/23 na kuiwasilisha kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

vii. Kuendelea kuhudhuria na kutoa ushahidi kwenye mashauri Mahakamani yanayoihusisha Tume;

viii. Kuimarisha uhusiano wa Tume ya Utumishi wa Umma na Tume nyingine ndani ya Muungano na Ukanda wa Afrika Mashariki;

ix. Kufanya utafiti kuhusu usimamizi wa masuala ya Kiutumishi kwenye Utumishi wa Umma;

x. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ushughulikiaji wa rufaa ili kuongeza ufanisi kwa kuwawezesha watumishi wa Umma kuwasilisha na kufuatilia rufaa zao kwa njia ya mfumo wa kielektroniki; na

xi. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Ofisi ya Tume katika Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma.

***65. Mheshimiwa Spika**,* katika mwaka 2023/24, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi **shilingi 8,624,091,000.00** ili kutekeleza shughuli zilizotajwa hapo juu. Kati ya fedha hizo **shilingi 8,324,091,000.00** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 300,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani.

**OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA**

***66. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2023/24 Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itaendelea kutekeleza shughuli zifuatazo:-

i. Kukusanya taarifa, kumbukumbu na nyaraka mbalimbali zinazohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za Umma, taasisi na watu binafsi;

ii. Kufanya ukarabati wa nyaraka kongwe zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la nyaraka na zinazotarajiwa kukusanywa;

iii. Kuingiza nyaraka katika Mfumo wa Kidigitali wa Kuhifadhi Kumbukumbu na Nyaraka (*Digital Records Management and Preservation System*) kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka, kurahisisha upatikanaji wake na kulinda nakala halisi;

iv. Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika taasisi za umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma serikalini;

v. Kuzijengea uwezo taasisi za umma kuhusu sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali kupitia mikutano na mafunzo kazi kwa watumishi wa umma;

vi. Kutathmini kumbukumbu tuli za taasisi za Umma zilizohifadhiwa kwa ajili ya kubaini kumbukumbu tuli zenye umuhimu wa kuendelea kuhifadhiwa na zilizofikia ukomo kwa lengo la kuziteketeza kwa mujibu wa sheria;

vii. Kukagua, kuchambua na kuhamisha kumbukumbu tuli kutoka katika taasisi za umma na kuzihifadhi katika vituo vya kumbukumbu vya idara;

viii. Kuwezesha taasisi za umma kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu (*record retention and disposal schedule*) kwa mujibu wa sheria;

ix. Kukagua hali ya utunzaji wa kumbukumbu katika taasisi za umma;

x. Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

xi. Kuendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika maendeleo ya Taifa letu; na

xii. Kujenga Jengo la Utawala la Idara katika Makao Makuu ya nchi Dodoma.

***67. Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2023/24, Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Fungu 4, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 4,347,811,000.00.** Kati ya fedha hizo, **shilingi 3,897,811,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 450,000,000.00** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani**.**

**MAJUMUISHO**

***68. Mheshimiwa Spika,*** kimsingi Ofisi ya Rais ikiongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndiyo yenye dhamana ya maamuzi juu ya nchi na kwa umuhimu wake inahusika pia na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo kwa pamoja inakuwa nguzo muhimu na mtambuka katika uendeshaji na uendelezaji wa nchi. Naomba turejee kuwa Utumishi wa Umma umeendelea kutoa mchango mkubwa katika maendeleo ya nchi ambayo kwa sasa Tanzania ni miongoni mwa nchi zenye uchumi wa kipato cha kati cha kiwango cha

chini. Ni wazi kuwa tunayo matarajio makubwa kuwa mchango wa watumishi wa umma katika maendeleo utaendelea kuwezesha nchi kufikia uchumi wa kati wa kiwango cha juu. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kuongezeka kwa kuimarisha uchumi shindani na viwanda kwa maendeleo ya watu kama inavyoshajiishwa katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (Five Year Development Plan III – FYDP III). Baadhi ya viashiria vinaonekana kwa Nchi yetu kuwa ya tatu katika Afrika na ya kwanza katika Afrika ya Mashariki kwa namna unavyotumia TEHAMA katika shughuli za Serikali na Utoaji huduma kwa umma kwa uratibu na umahiri wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

***69. Mheshimiwa Spika,*** Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, ukizingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo katika kujenga imani zaidi kwa wananchi na kuendana na kauli ya Rais, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliyoitoa 22 Aprili, 2021 wakati akilihutubia Bunge la 12 aliposema: '***Tutawapima viongozi na watumishi kwa namna wanavyotimiza majukumu yao, hatutawaonea aibu viongozi na watumishi wazembe, wezi na wabadhirifu wa mali za umma. Tutaendeleza pia juhudi za kupambana na rushwa kwenye utumishi wa umma. Wajibu wa watumishi wa umma ni lazima uendane na haki zao*'**.** Katika kuendana na wakati, jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

***70. Mheshimiwa Spika***, maombi ya Ofisi ya Rais yatawezesha vyombo vinavyosaidia kwenye maamuzi ya nchi, usalama na kuimarisha vita dhidi ya rushwa. Hivyo, kupitisha Bajeti ya Ofisi hii ni kuchangia katika uimarishaji na

uwezeshaji wake vyombo hivyo na malengo yake kwa Taifa. Aidha, kupitisha bajeti hii ni njia ya kuimarisha na kuchangia kukuzwa kwa Maadili kwa viongozi wote na watumishi wa umma kwenye nchi hivyo kupata tija ya rasilimaliwatu na rasilimalifedha kwa kuwa na matumizi yenye tija ya rasilimali hizo kwa wakati wote. Kwa bajeti hii, Serikali itayapa kipaumbele maeneo ya usimamizi wa rasilimaliwatu na rasilimalifedha. Vilevile, bajeti itaiwezesha Serikali kupandisha vyeo watumishi; ubadilishwaji wa kada au muundo wa utumishi; kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi na kutoa ajira mpya.

***71. Mheshimiwa Spika**,* Serikali kwa ujumla inafanya maboresho ya kisekta na mtambuka, wajibu wa Ofisi ya Rais itakuwa ni kuhakikisha maboresho yanayofanywa katika nchi yetu hayana urudufu na yanaleta tija katika Utumishi wa Umma na kuchochea maendeleo. Aidha, Ofisi itahakikisha kunakuwepo na utawala bora ulio imara kuanzia ngazi ya juu ya uongozi hadi ngazi ya chini. Katika kuimarisha misingi ya utawala bora ya ushirikishwaji, uwazi na uwajibikaji, Ofisi ya Rais itahakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu maamuzi ya Serikali na kuweka imara mifumo ya mrejesho wa utoaji huduma.

***72. Mheshimiwa Spika**,* Kwa nchi yetu na kwa mujibu wa Hati idhini inayotoa mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, nawajibika kuwasilisha mapitio ya utekelezaji mipango na bajeti ya Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa. Hivyo, nalihakikishia Bunge lako tukufu kuwa Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Sita kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji

wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma kwa kufanyia mapitio ya michakato ya utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

***73. Mheshimiwa Spika,*** baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka 2022/23 na Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora sasa naomba kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi kwa mwaka 2023/24 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | **Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 32,157,384,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **32,157,384,000.00** |
| 2. | **Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 678,193,941,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 181,992,535,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **860,186,476,000.00** |
| 3. | **Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 10,813,016,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 1,950,000,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **12,763,016,000.00** |
| 4. | **Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 57,130,005,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 12,187,455,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **69,317,460,000.00** |
| 5. | **Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 10,139,298,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 3,572,517,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **13,711,815,000.00** |
| 6. | **Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 8,324,091,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 300,000,000.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **8,624,091,000.00** |
| 7. | **Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa** | | |
| | Matumizi ya Kawaida | Sh. | 3,897,811,000.00 |
| | Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 450,000,000.00 |
| | **Jumla Ndogo** | **Sh** | **4,347,811,000.00** |
| | | | |

***74. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu***, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2023/24, ni kama ifuatavyo:-

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Jumla kuu - Matumizi ya Kawaida | Sh. | 800,655,546,000.00 |
| | Jumla kuu - Matumizi ya Miradi ya Maendeleo | Sh. | 200,452,507,000.00 |
| | **Jumla Kuu kwa Mafungu Yote** | **Sh** | **1,001,108,053,000.00** |

***75. Mheshimiwa Spika na Wabunge wenzangu***, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

**Ahsanteni kwa kunisikiliza, naomba kutoa hoja**.

**WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI**: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante na hoja imeungwa mkono. Sasa namuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala Katiba na Sheria kuwasilisha taarifa ya kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa 2022/2023 pamoja na maoni ya kamati. *(Makofi)*

**MHE. FLORENT L. KYOMBO - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa nafasi ya pekee nimushukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha siku ya leo lakini pili nishukuru wajumbe wa Kamati ya Utawala Katiba na Sheria kwa kunichagua kuwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii. Naomba taarifa yetu kama ilivyowasilishwa iingie kwenye *Hansard* kama ilivyowaslishwa kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa utangulizi huo naomba kwa nafasi ya pekee niwaslilishe taarifa ya kamati ya bunge ya utawala katiba na Sheria kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2022/2023 pamoja na maoni ya kamati kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Mheshimiwa Naibu Spika, Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kifungu cha 6(2)(a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a)

cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kamati hii kwa kupitia Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

Mheshimiwa Spika, Mawanda ya Uchambuzi, katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni: -

(a) Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu;
(b) Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
(c) Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
(d) Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
(e) Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
(f) Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na
(g) Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo kama yanavyoonekana kwenye taarifa zetu ambazo tunazo kwenye vishikwambi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha

2022/2023; napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 22 na 23 Machi, 2023. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa bajeti zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Na. 20 Na Fungu Namba 30 – Ofisi Ya Rais, Ikulu Na Sekretarieti Ya Baraza La Mawaziri. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu Na. 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 29.8, kati ya fedha hizo bilioni 8.1 ilitengwa kwa ajili ya Mishahara na shilingi bilioni 21.7 ilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya bilioni 18.2 sawa na asilimia 61.1

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu Namba 30 -Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 741.2. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 577.2 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 573.4 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 3.7 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 164.0 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo shilingi bilioni 62.6 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 101.3 ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya shilingi bilioni 444.0 sawa na asilimia 60 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 47.6. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 39.5 sawa na asilimia 83.05 ya bajeti zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 18.0 ilitengwa

kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 21.4 ilitengwa kwa ajili ya Mishahara. Aidha, shilingi bilioni 8.0 sawa na asilimia 16 ya bajeti zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 36.0 sawa na asilimia 75.7 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 12.7, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 9.2 sawa na asilimia 72.7 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 6.5 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.7 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, bilioni 3.4 sawa na asilimia 27.3 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 2.8 ni fedha za ndani na shilingi milioni 650 ni fedha za nje. Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya shilingi bilioni 7.0 sawa na asilimia 55 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 inatekeleza miradi miwili, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa fedha za ndani na Mradi wa Kuimarisha Programu za Mapambano Dhidi ya Rushwa kwa fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya miradi ya maendeleo hususani mradi unaotekelezwa kwa fedha za ndani hadi kufikia Februari, 2023 ni mchakato ya kuwapata wakandarasi kuchukua muda mrefu hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kuandaa hati za malipo.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 8.7, kati ya fedha hizo bilioni 5.0 sawa na asilimia 58

zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 3.2 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 1.8 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 3.6 sawa na asilimia 42 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya shilingi bilioni 4.5 sawa na asilimia 52 ya fedha iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kuonekana kuwa Fungu hili limepata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni watumishi waliopaswa kuajiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kutoajiriwa wote na watumishi kuhamia kwenye taasisi zingine. Aidha, upungufu wa bajeti kwenye mradi wa maendeleo umesababishwa na ucheleweshaji wa kuanza kwa mradi hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kupata hati za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma. Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa shilingi bilioni 5.9, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia 95 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Ambapo bilioni 3.3 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.2 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi milioni 300 sawa na asilimia tano zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya shilingi bilioni 3.4 sawa na asilimia 57 ya fedha iliyoidhinishwa. Kamati ilielezwa kuwa mapokezi ya fedha hadi kufikia Machi, 2023 kwa miradi ya maendeleo Fungu hili lilipokea shilingi milioni 299 sawa na asilimia 99.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu Namba 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa; kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya shilingi

bilioni 4.9. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 3.5 sawa na asilimia 71.31 zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ambapo shilingi bilioni 1.5 zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi bilioni 2.0 zilitengwa kwa ajili ya mishahara. Aidha, shilingi bilioni 1.4 sawa na asilimia 28.6 zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya shilingi bilioni 2.4 sawa na asilimia 50.8 ya fedha iliyoidhinishwa. Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni matarajio ya ofisi hii kuwa na ajira mpya na upandishaji vyeo ambao hadi Februari, 2023 hawakupokea watumishi wapya wala Watumishi waliopandishiwa vyeo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba: -

a) Kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa shilingi bilioni 851.0 kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hii ilipokea Jumla ya shilingi bilioni 515.8 sawa na asilimia 60.6 ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

b) Taasisi tatu kati ya saba za Ofisi hii ndizo zilizofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa asilimia 66.6 hadi kufikia Februari, 2023.

c) Ofisi hii ingeweza kukusanya Maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anayekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha

kwa ujumla si wa kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023. Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Bora ni kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 1 na Jedwali Namba 2.

Mheshimiwa Naibu Spika, Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais; bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi yanayoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora. Naomba kurejea hiyo kwa msisitizo. Kutokana na hali hiyo Kamati inampongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa, usimamizi na uratibu wa shughuli za Utumishi wa Umma umeimarika zaidi sana katika misingi ya utawala Bora, hali

ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala bora Afrika na duniani kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo; kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Ofisi hii ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 181.0 kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo bilioni 164.0 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 30 Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, shilingi bilioni 3.4 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 33 Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa Umma na shilingi bilioni 8.0 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 32 Ofisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Shilingi bilioni 1.4 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 04 Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, bilioni 3.6 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 67 Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma na Milioni 300 ziliidhinishwa kwa Fungu Namba 94 Tume ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Mfuko wa Maendeleo *TASAF*. Mradi wa Kupanua Bwawa Dogo unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo *TASAF* ili Kijiji cha Magiri, Wilaya ya Uyui, Mkoa wa Tabora. Kamati ilielezwa kuwa gharama za mradi huu ni shilingi milioni 2.8 ambapo milioni 2.5 ni kwa ajili ya malipo ya ujira kwa wanufaika ambao wanalipwa shilingi 3,000 kwa siku kwa watekelezaji wa mradi ambao ni wanufaika 12 na shilingi 287.4 elfu ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 ukiwa umeshatumia milioni 1.0 na kuwa na bakaa ya shilingi milioni 1.8 ambayo itatumika kuwalipa walengwa kwa kuzingatia ratiba na taratibu za malipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kukagua mradi huu na kufanya mkutano wa wazi na wanufaika wa

*TASAF*, Kamati ilipokea malalamiko ya baadhi ya wanufaika na kubaini kuwa kaya nyingi hazikuridhika na uhakiki uliofanyika. Wanufaika wengi wamekosa sifa za kujiunga na Mradi wa *TASAF* kwa sababu ya kukosa vitambulisho vya Taifa *(NIDA)* licha ya kwamba wengi wao walishafanya maombi ya kupata vitambulisho hivyo muda mrefu. Hata hivyo wapo baadhi waliokata rufaa baada ya kukosa sifa za kujiunga na mradi lakini majibu ya rufaa zao yamechelewa kutoka. Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha Wanufaika wote waliokata rufaa majibu ya rufaa zao yatolewe kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Kisima cha maji unaotekelezwa TASAF katika Kijiji cha Magiri, Wilaya ya Uyui ambao unatekelezwa na wanufaika 7 kwa gharama ya Shilingi milioni 1.6 shilingi 180.3 elfu ni kwa ajili ya vifaa vya ujenzi na usafiri, shilingi 180 elfu ni kwa ajili ya ufundi na usimamizi na shilingi milioni 1.2 ni kwa ajili ya ujira wa Shilingi 3,000 kwa siku kwa wanufaika walengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa lengo la msingi la mradi huo ni kuwawezesha wanaufaika wa *TASAF* kupata kipato cha ziada cha shilingi 3,000 kwa siku nje ya mafao ya uwezeshaji ya kawaida wanayopewa na *TASAF* ili waweze kumudu gharama za maisha. Wakati wa ukaguzi, Kamati ilibaini ujenzi wa mradi haukuzingatia utalaam usanifu kwa kutokufunikwa kwa sehemu ya nondo, jambo linaloweza kupelekea kuoza kwa nondo hizo mapema na kuleta madhara kwa kisima na watumiaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kwa sababu hiyo, Kamati ilishauri ujenzi wa mradi husika uzingatie ubora kwa ajili ya usalama na ili mradi uweze kudumu. Pia Kamati ilishauri watalaam wa sekta ambako miradi inatekelezwa wahusishwe kutoa ushauri wa kitalaam katika utekelezaji ili miradi iwe miradi endelevu. Aidha, Kamati inashauri kwamba ni vyema miradi itakayobuniwa iweze kutumika kuwanufaisha

walengwa ambao ni kaya maskini ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuondokana na hali ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Barabara ya Mtaa unaotekelezwa na wanufaika wa *TASAF* Kata ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ni ujenzi wa barabara ya mtaa yenye urefu wa Kilometa 2.5 kwa gharama ya shilingi milioni 25.6 ambapo shilingi milioni 22.1 ni kwa ajili ya ujira kwa watekelezaji wa mradi ambao ni wanufaika 123 wa *TASAF* wanaolipwa shilingi 3,000 kwa siku na shilingi milioni 3.5 ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa na usafirishaji wa vifaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za bei Nafuu 198 unaotekelezwa na Taasisi ya *Watumishi Housing* Kisasa *Hiltop*, Njedengwa, Dodoma. Mradi huu ambao ni kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa umma ulianza kutekelezwa Agosti, 2017 na ulitakiwa kukamilika Mei, 2019 kwa gharama ya shilingi bilioni 7.2. Utekelezaji wa mradi huu unajumuisha ujenzi wa nyumba 198 pamoja na uwekaji wa miundombinu yote muhimu ikiwemo barabara, maji, umeme na madaraja. Bei za nyumba hizo zimegawanywa kwa makundi kutegemea na ukubwa wa nyumba yenyewe. Gharama za nyumba hizo ni kuanzia shilingi milioni 45.8 kwa nyumba ya gharama ndogo na nyumba yenye bei ya juu zaidi huuzwa kwa shilingi milioni 98.5 na malipo hufanyika kwa awamu au mkupuo kulingana na chaguo la mnunuzi. Kwa sasa jumla ya nyumba 196 zimeshajengwa na asilimia 94 ya nyumba hizo tayari zimeshapata wateja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuja na mradi huu wa nyumba za bei nafuu kwa ajili ya watumishi wa umma. Aidha, Kamati ilibaini changamoto kwenye usimamizi wa mradi huu

unaosababishwa na upungufu wa watumishi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza watumishi kwenye taasisi hii ili waweze kusimamia miradi zaidi ya 40 inayotekelezwa nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Makao Makuu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dodoma. Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya shilingi bilioni 22.3. Mradi unatekelezwa kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa jengo na awamu ya pili ni umaliziaji *(finishing)*. Awamu ya kwanza ilianza mwezi Mei, 2021 na ilitakiwa kukamilika Mei, 2022. Kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, mkandarasi wa mradi alipewa nyongeza ya muda wa miezi sita baada ya muda wa awali kumalizika bila ya kukamilika. Aidha, baada ya miezi sita kukamilika, mkandarasi aliongezewa muda tena wiki ishirini na moja hivyo basi, awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika Mwezi Mei, 2023. Hadi wakati wa ukaguzi mradi ulikuwa umefikia asilimia 60 ya awamu ya kwanza na jumla ya shilingi bilioni 6.5 zimeshalipwa kwa mkandarasi na mtalaam elekezi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilielezwa kuwa kwa sababu mradi umechelewa kwa muda wa mwaka mmoja kutokana na uwepo wa chemchemi ya maji katika eneo la ujenzi na hivyo kuhitajika kuwekwa tenki la maji ya chini. Licha ya sababu hiyo, Kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi huu uliosababisha kukwama kwa kuanza kutekelezwa kwa mradi wa awamu ya pili. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mradi unakamilika mapema na kwa kiwango stahiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa utekelezaji wa mradi ya maendeleo umeonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2023, fedha ilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni shilingi bilioni 140.6 sawa na asilimia 77.7 ya bajeti iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati; wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo 13. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano wa ushauri uliozingatiwa, unahusu Serikali kutengeneza kanzidata ya wanaofanyiwa usaili na kufaulu kwa lengo la kuwa na orodha ya Wataalam wenye sifa wasioajiriwa, ambao wanaweza kuajiriwa bila usaili mwingine iwapo itatokea nafasi ya ajira. Kufatia ushauri huo Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetengeneza kanzidata ya kieletroniki ya kuhifadhi orodha ya wasailiwa waliofaulu usaili na kukosa nafasi kutokana na uchache wa nafasi. Kanzidata hiyo itatumika kuajiri vijana pale nafasi za ajira zitakapotangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa bado kuna umuhimu kwa Serikali kujali ushauri unaotolewa na Kamati Bungeni. Kwani uzingatiaji wa ushauri wa Kamati unawezesha Serikali kukidhi matarajio ya wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; Kamati imetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata. Kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge, Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 785,255,545,500 ikiwa ni fedha za Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo shilingi 46,896,731,500 ni kwa ajili ya mishahara *(PE)* na shilingi 738,358,814,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo *(OC)*.

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2023/2024 imeongezeka kwa asilimia 17.18 ukilinganisha na mwaka wa fedha unaoisha ambapo bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa shilingi 670,086,770,000. Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya Kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye Jedwali Na. 3

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo; katika mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imeomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 196,452,507,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi 94,490,717,000 ni fedha za ndani na shilingi 101,961,790,000 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya maendeleo katika mwaka wa fedha 2023/2024, imeongezeka kwa shilingi

15,451,713,000 sawa na asilimia 8.53 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana katika Jedwali Na.4

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Hata hivyo, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba, bado kiwango cha fedha ambacho kinatengwa kwa kutumia fedha za nje ni kikubwa ukilinganisha na kile kilichotengwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati; baada ya maelezo haya, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarajio ya wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha;

(c) Upo umuhimu wa wakala wa ndege za Serikali kupunguziwa majukumu hasa ya umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)*, ili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ulete tija; *(Makofi)*

(d) Serikali ifanye tathmini ya uwiano wa watumishi wa umma mijini na vijijini, ili kuongeza ufanisi kwenye maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa watumishi; na

(e) Mradi wa *TASAF,* awamu ya tatu uwanufaishe walengwa, Serikali iboreshe malipo kuendana na kazi iliyofanyika kwenye mradi husika na ishughulikie malalamiko ya wanufaika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ushauri wa Kamati; kutokana na maoni yaliyobainishwa kutokana na uchambuzi, naomba kutoa ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kuzingatia ipasavyo ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa mipango, majukumu ya bajeti kwa madhumuni ya kukidhi matarajio ya wananchi;

(b) Serikali ihamishe umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania kutoka kwa Wakala wa Ndege ya Serikali kwenda kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *ATCL;*

(c) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yanayopangwa;

(d) Serikali iharakishe upatikanaji wa Vitambulisho vya Taifa ili kuwawezesha wananchi wenye sifa za kunufaika na Mradi wa *TASAF* wapate fursa hiyo;

(e) Serikali ione umuhimu wa kutumia matokeo ya Sensa ya Watu wa Makazi ya Mwaka 2020 kwenye kubaini wanufaika wanaostahili kuingia kwenye Mradi wa *TASAF;*

(f) Serikali iharakishe matokeo ya rufaa za waombaji wa kujiunga na Mradi wa *TASAF;*

(g) Serikali iendelee kuimarisha msingi wa utawala bora pamoja na kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika utumishi

wa umma sambamba na kuboresha mishahara na maslahi ya watumishi;

(h) Serikali iendelee kutoa ajira zaidi ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi katika Serikali. Aidha, Serikali itumie Kanzidata ya Wasailiwa waliofanya vizuri kwenye usaili na kukosa nafasi.

(i) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalum ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa; na

(j) Serikali iondoe mrundikano wa watumishi wa umma walio maeneo ya mijini na kuwahamishia sehemu zenye watumishi wachache hususani maeneo ya vijijini ambayo yana uhitaji zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hitimisho; napenda kumshukuru Mheshimiwa Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson, kukushukuru wewe binafsi pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu wa kutupatia nafasi ya kuwasilisha Taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao kwa maoni yao Ushauri na Ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyoainishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa George Boniface Simbachawene, kuendelea kuaminiwa na Rais na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na

Naibu Waziri wake Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete ambao wametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati. Aidha, Kamati inampongeza Mheshimiwa Jenista Joakim Mhagama, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu ambao wakati wa Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii, aliipa Kamati ushirikiano mkubwa kama Waziri wa Ofisi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Taasisi zake kwa ushirikiano waliyoipatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu Kiongozi; Ndugu Majura Mahendeka, Katibu Mkuu Ikulu; na Ndugu Juma Selemani Mkomi, Katibu Mkuu Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu wa Katiba ya Nchi. Aidha, niwashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, *ndc*. Mkurugenzi msadizi, Ndugu Gerarld Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndugu Frank Nkya, Ndugu Praisegod Lukio na Ndugu Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bibi Theresia Jacob kwa kuratibu Shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**19 APRILI, 2023**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2022/2023 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, kuhusu Utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika**, ili kuliwezesha Bunge kufuatilia taarifa hii ipasavyo, naomba kutambulisha sehemu nne za Taarifa hii ambazo ni:-

(a) Sehemu ya **Kwanza** inahusu maelezo ya jumla, inabainisha msingi na muundo wa Taarifa hii;

(b) Sehemu ya **Pili** inahusu uchambuzi wa Utekelezaji wa bajeti kwa kuangalia mwenendo wa upatikanaji wa fedha na uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati;

(c) Sehemu ya **Tatu** inahusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati;

(d) Sehemu ya **Nne** ni Hitimisho.

### 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa Kamati kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge. Kifungu cha 6 (2) (a) kikisomwa kwa pamoja na Kifungu cha 7(1)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge, zinatambua jukumu la Kamati hii kufanya uchambuzi huo. Aidha, Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Ofisi hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba kulitaarifu Bunge lako tukufu kuwa masharti hayo yamezingatiwa.

### 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi huo, Kamati ilipitia jumla ya mafungu saba (7) ambayo ni:-

a) **Fungu 20**: Ofisi ya Rais, Ikulu;

b) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;

c) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;

d) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

e) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

f) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; na

g) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

### 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwa msingi huo, ili kuwezesha ufuatiliaji mzuri wa wasilisho hili, Taarifa hii imejielekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

(a) Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(b) Taarifa ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023;

(c) Uzingatiaji wa Maazimio ya Bunge; na

(d) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

### 2.2 Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/2023

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ilizingatia Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kazi hiyo ilifanyika tarehe 22 na 23 Machi, 2023. Uchambuzi huo umejikita kwenye kulinganisha uwiano wa

fedha zilizoidhinishwa, fedha zilizopokelewa pamoja na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Uchambuzi huo ni kama ifuatavyo:-

2.2.1 **Fungu Na. 20 na Fungu Na. 30 – OFISI YA RAIS (IKULU) NA SEKRETARIETI YA BARAZA LA MAWAZIRI.**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 **Fungu Na. 20** - Ofisi ya Rais (Ikulu) iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 29,828,203,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 8,118,876,000** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 21,709,327,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (OC).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 18,225,488,831.32** sawa na **asilimia 61.10**. Kati ya fedha hizo **Sh. 5,412,584,000** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) sawa na **asilimia 66.67** na **Sh, 12,812,904,831.32** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) sawa na **asilimia 59.02**.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023 **Fungu Na. 30** -Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri iliidhinishiwa jumla ya **Sh. 741,299,267,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 577,206,673,000** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 573,461,500,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 3,745,173,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 164,092,594,000** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo **Sh. 62,698,000,000** ni fedha za ndani na **Sh. 101,394,594,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 444,071,919,686.5** sawa na **asilimia 60** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 312,933,489,223.76** sawa na **asilimia 54.22** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 131,138,430,462.74** sawa na **asilimia 80** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.2 Fungu Na. 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 47,611,581,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 39,541,381,000** sawa na **asilimia 83.05** ya bajeti zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 18,083,845,000** ilitengwa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 21,457,536,000** ilitengwa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 8,070,200,000** sawa na **asilimia 16.95** ya bajeti zilitengwa kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea jumla ya **Sh. 36,056,774,859.05** sawa na **asilimia 75.73** ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 30,099,223,414.89** sawa na **asilimia 76.1** zilipokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo **Sh. 15,920,545,306.11** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na **Sh. 14,178,678,108.78** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE). Aidha, **Sh. 5,957,551,444.16** sawa na **asilimia 73.8** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

### 2.2.3 Fungu Na. 33 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 12,730,049,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 9,260,049,000** sawa na **asilimia 72.7** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Sh. 6,542,825,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 2,717,224,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 3,470,000,000** sawa na **asilimia 27.3** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo **Sh. 2,820,000,000** ni fedha za Ndani na **Sh. 650,000,000** ni fedha za Nje.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 7,000,542,969.33** sawa na **asilimia 55** ya

fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 6,040,699,726.12** sawa na **asilimia 65** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 959,843,243.21** sawa na **asilimia 27.66** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, ambapo **Sh. 600,000,880** sawa na **asilimia 21.2** zilizopokelewa ni fedha za ndani na **Sh. 359,842,363.21** sawa na **asilimia 55.36** zilizopokelewa ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2022/2023 inatekeleza Miradi miwili, Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma **Mradi Na. 6389** kwa fedha za ndani na Mradi wa Kuimarisha Programu za Mapambano Dhidi ya Rushwa BSAAT (DFID) **Mradi Na. 6210** kwa fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya miradi ya maendeleo hususani mradi unaotekelezwa kwa fedha za ndani hadi kufikia Februari, 2023 ni michakato ya kuwapata Wakandarasi kuchukua muda mrefu hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kuandaa hati za malipo.

2.2.4 **Fungu Na. 67 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 8,721,849,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 5,063,849,000** sawa na **asilimia 58** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 3,231,577,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 1,832,272,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE), aidha, **Sh. 3,658,000,000** sawa na **asilimia 42** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 4,539,184,428.34** sawa na **asilimia 52** ya fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 2,785,409,812.34** sawa na **asilimia 55** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya

Kawaida ambapo **Sh. 952,983,314.24** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) sawa na **asilimia 52** na **Sh. 1,832,426,498.1** sawa na **asilimia 56.7** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida, aidha, **Sh. 1,753,774,616** sawa na **asilimia 48** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea kuonekana kuwa Fungu hili limepata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni Watumishi 43 walipaswa kuajiriwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 kutoajiriwa wote na Watumishi kuhamia kwenye taasisi zingine. Aidha, upungufu wa bajeti kwenye mradi wa maendeleo umesababishwa na ucheleweshaji wa kuanza kwa mradi hivyo kupelekea ucheleweshaji wa kupata hati za malipo.

2.2.5 **Fungu Na. 94 – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh. 5,981,824,000**, kati ya fedha hizo **Sh. 5,681,824,000** sawa na **asilimia 95** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 3,378,986,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 2,302,838,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE), aidha, **Sh. 300,000,000** sawa na **asilimia 5** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 3,433,268,711.18** sawa na **asilimia 57.4** ya fedha iliyoidhinishwa, kati ya fedha hizo **Sh. 3,433,268,711.18** sawa na **asilimia 60.4** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na hakuna fedha iliyopokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa mapokezi ya fedha hadi kufikia March, 2023 kwa miradi ya maendeleo Fungu hili lilipokea **Sh. 299,995,000** sawa na **asilimia 99.9** na **Sh.**

**4,097,324,957.17** sawa na **asilimia 68.4** kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

2.2.6 **Fungu Na. 04 – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Fungu hili liliidhinishiwa jumla ya **Sh.4,914,791,000**. Kati ya fedha hizo **Sh. 3,504,791,000** sawa na **asilimia 71.31** zilitengwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 1,500,000,000** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC) na **Sh. 2,004,791,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara (PE). Aidha, **Sh. 1,410,000,000** sawa na **asilimia 28.69** zilitengwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2023 Fungu hili lilipokea Jumla ya **Sh. 2,497,147,979.06** sawa na **asilimia 50.8** ya fedha iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo **Sh. 1,662,288,756.56** sawa na **asilimia 47.43** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo **Sh. 790,025,432** sawa na **asilimia 39.4** zilipokelewa kwa ajili ya Mishahara (PE) na **Sh. 872,264,324.56** sawa na **asilimia 58.15** zilipokelewa kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC). Aidha, **Sh. 834,858,222.50** sawa na **asilimia 59.21** zilipokelewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa kuwa sababu zilizopelekea Fungu hili kupata bajeti pungufu ya matarajio kwa ajili ya matumizi ya kawaida ni matarajio ya ofisi hii kuwa na ajira mpya na upandishaji vyeo ambao hadi Februari, 2023 hawakupokea Watumishi wapya wala Watumishi waliopandishiwa vyeo.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa upatikanaji wa fedha hizo unaonesha kwamba:

(a) kwa ujumla, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora iliidhinishiwa **Sh. 851,087,564,000**

kwa mwaka wa fedha 2022/2023, hadi kufikia Februari, 2023 Ofisi hii ilipokea Jumla ya **Sh. 515,824,327,464.78** sawa na **asilimia 60.6** ya bajeti iliyo idhinishiwa na Bunge.

(b) Taasisi tatu kati ya saba za Ofisi hii ndizo zilizofanikiwa kupata kiasi cha fedha ambacho kinaendana na uwiano wa upatikanaji wa fedha kwa **asilimia 66.6** hadi kufikia Februari, 2023.

(c) Ofisi hii ingeweza kukusanya Maduhuli kupitia taasisi zinazofanya biashara kama vile Wakala wa Ndege za Serikali anaekodisha ndege zake kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL).

**Mheshimiwa Spika**, kwa uchambuzi huo, Kamati ina maoni kwamba, mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa ujumla si wa kuridhisha. Kamati inaishauri Serikali ihakikishe kwamba fedha zote zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya taasisi zilizo chini ya Ofisi hii zinapatikana kabla ya kuisha kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

**Mheshimiwa Spika**, Mchanganuo wa fedha hizo kwa taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 1** na **Jedwali Na. 2**

**JEDWALI NA. 1: Mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 29,828,203,000 | 18,225,488,831.32 | 61.10 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 577,206,673,000 | 312,933,489,223.76 | 54.21 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 39,541,381,000 | 30,099,223,414.89 | 76.1 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 9,260,049,000 | 6,040,699,726.12 | 65 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 5,063,849,000 | 2,785,409,812.34 | 55 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya | 5,681,824,000 | 4,097,324,957.17 | 72.11 |

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| Utumishi wa Umma | | | |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 3,504,791,000 | 1,662,288,756.56 | 47.43 |
| **JUMLA KUU** | **670,086,770,000** | **375,843,924,722.16** | **56.08** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2023.*

**JEDWALI NA. 2: Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2022/2023**

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 164,092,594,000 | 131,138,430,462.74 | 80 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 8,070,200,000 | 5,957,551,444.16 | 73.8 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 3,470,000,000 | 959,843,243.21 | 27.66 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya | 3,658,000,000 | 1,753,774,616 | 48 |

| FUNGU | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | FEDHA YA MAENDELEO ILIYOPOKELEWA HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2023 | ASILIMIA YA MAPOKEZI |
|---|---|---|---|
| Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | | | |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 300,000,000 | 299,995,000 | 99.9 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 1,410,000,000 | 834,858,222.50 | 59.21 |
| **JUMLA KUU** | **181,000,794,000** | **140,944,452,988.61** | **77.86** |

***Chanzo**: Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2023.*

2.3 **Utekelezaji wa Mipango na Majukumu ya Ofisi ya Rais**

**Mheshimiwa Spika**, bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2022/2023 ililenga kufanikisha utekelezaji wa mipango na majukumu ya Ofisi ya Rais, Menjimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na taasisi zilizopo chini ya Ofisi hiyo. Ili kuliwezesha Bunge kujiridhisha na mwenendo wa Matumizi unayoakisi madhumuni ya kuidhinishwa kwa bajeti hiyo, Kamati ilichambua utekelezaji wa mipango na majukumu ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa utekelezaji wa bajeti umezingatia mipango na majukumu yaliyoombewa fedha. Aidha, Ofisi hii ilitumia fedha zilizopatikana kusimamia na kuimarisha misingi ya Utawala Bora.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo, Kamati inampongeza kwa dhati **Mhe. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Amiri Jeshi Mkuu** kwa usimamizi madhubuti wa Utawala Bora. Ni maoni ya Kamati

kuwa, usimamizi na uratibu wa shughuli za Utumishi wa Umma umeimarika zaidi sana katika misingi ya utawala Bora, hali ambayo imeendelea kuipandisha nchi yetu katika medani za utawala Bora Afrika na Duniani kote.

## 2.4 **Tathmini ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi hii ilitengewa jumla ya **Sh. 181,000,794,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo **Sh. 164,092,594,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 30** Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, **Sh. 3,470,000,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 33** Sekretarieti ya Maadili ya viongozi wa Umma, **Sh. 8,070,200,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 32** Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, **Sh. 1,410,000,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 04** Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, **Sh. 3,658,000,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 67** Sekretarieti ya Ajira Katika Utumishi wa Umma, **Sh. 300,000,000** ziliidhinishwa kwa **Fungo Na. 94** Tume ya Utumishi wa Umma.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea miradi mitatu inayosimamiwa na Wizara na kuchambua utekelezaji wa miradi hiyo kama ifuatavyo:-

### 2.4.1 **Mradi Na. 6220: Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)**

(a) ***Mradi wa Kupanua Bwawa Dogo (Lambo) unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili Kunusuru Kaya Maskini-Kijiji cha Magiri, Wilaya ya Uyui) – Tabora.***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa kuwa gharama za mradi huu ni **Sh. 2,807,400** ambapo **Sh. 2,520,000** ni kwa ajili ya malipo ya ujira wa mnufaika ambayo ni **Sh. 3000** kwa siku kwa watekelezaji wa mradi ambao ni wanufaika kumi na mbili (12), na **Sh. 287,400** ni kwa ajili ya ununuzi wa vifaa. Mradi huo

umekamilika kwa **asilimia 100** ukiwa umeshatumia **Sh. 1,007,000** na kuwa na bakaa ya **Sh. 1,800,000** ambayo itatumika kuwalipa walengwa kwa kuzingatia ratiba na taratibu za malipo. Licha ya kamati kuelezwa kuwa bwawa hilo (lambo) litakalotumika kunyweshea mifugo na kwa ajili ya bustani kwa wakazi wote wa Kijiji, lengo la msingi la mradi ni kuwawezesha wanaufaika wa TASAF kupata kipato cha ziada nje ya mafao ya uwezeshaji ya kawaida wanayolipwa ili waweze kumudu gharama za maisha. Aidha, kamati ilielezwa kuwa kufuatia kukamilika kwa mradi huo, mradi utakabidhiwa kwa serikali ya kijiji kwa ajili ya matumizi ya wanakijiji wote.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Kamati kukagua mradi huu na kufanya mkutano wa wazi na wanufaika wa TASAF, kamati ilipokea malalamiko ya baadhi ya wanufaika na kubaini kuwa kaya nyingi hazikuridhika na uhakiki uliofanyika, Wanufaika wengi wamekosa sifa za kujiunga na mradi wa TASAF kwa sababu ya kukosa vitambulisho vya Taifa (NIDA) licha ya kwamba wengi wao walishafanya maombi ya kupata vitambulisho hivyo muda mrefu, Hatahivyo wapo baadhi waliokata rufaa baada ya kukosa sifa za kujiunga na mradi lakini majibu ya rufaa zao yamechelewa kutoka. Kamati ilishauri Serikali kuhakikisha Wanufaika wote waliokata rufaa majibu ya rufaa zao yatolewe kwa wakati.

(b) **Mradi wa Kisima cha maji unaotekelezwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ili Kunusuru Kaya Maskini-Kijiji cha Magiri, Wilaya ya Uyui) – Tabora.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu unatekelezwa na wanufaika saba (7) wa TASAF kwa gharama ya **Sh. 1,620,000** ambapo **Sh. 180,300** ni kwa ajili ya vifaa vya ujenzi na usafiri, **Sh. 180,000** kwa ajili ya ufundi na usimamizi na **Sh. 1,260,000** ni kwa ajili ya ujira wa **Sh. 3000** kwa siku kwa wanufaika walengwa. Mradi ulipangwa kutekelezwa kwa muda wa miezi sita kuanzia Mwezi Novemba, 2022 hadi Aprili 2023. Hadi

wakati wa ukaguzi, mradi ulikuwa umekamilika kwa kisima kuchimbwa na kujengewa huku kukibaki kazi moja ya kujenga uzio wa miti kuzunguka kisima. Kamati ilielezwa kuwa mradi ulikuwa umeshatumia **Sh. 780,000**. Aidha, kamati ilielezwa kuwa kufuatia kukamilika kwa mradi huo, watekelezaji wake wataukabidhi mradi huo kwa serikali ya kijiji kupitia Kamati ya huduma za jamii kwa ajili ya matumizi ya kijiji kizima na uendelezaji wa mradi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa lengo la msingi la mradi huo ni kuwawezesha wanaufaika wa TASAF kupata kipato cha ziada cha **Sh. 3000** kwa siku nje ya mafao ya uwezeshaji ya kawaida wanayopewa na TASAF ili waweze kumudu gharama za maisha. Wakati wa ukaguzi, kamati ilibaini ujenzi wa mradi haukuzingatia utalaam katika usanifu kwa kutokufunikwa kwa sehemu ya nondo na ujenzi jambo linaloweza kupelekea kuoza kwa nondo hizo mapema na kuleta madhara kwenye kisima na watumiaji wake. Kwa sababu hiyo, kamati ilishauri ujenzi wa mradi husika uzingatie ubora kwa ajili ya usalama na ili mradi uweze kudumu. Pia kamati ilishauri watalaam wa sekta ambako miradi inatekelezwa wahusishwe kutoa ushauri wa kitalaam katika utekelezaji wa miradi ikiwemo mradi huu wa maji ya kisima. Aidha, kamati inashauri kwamba ni vyema miradi itakayobuniwa iweze kutumika kuwanufaisha walengwa ambao ni kaya maskini ili waweze kujikwamua kiuchumi na kuondokana na hali ya umaskini.

(c) **Mradi wa barabara ya Mtaa unaotekelezwa na Wanufaika wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)-Kata ya Ngokolo, Manispaa ya Shinyanga.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu ni ujenzi wa barabara ya mtaa yenye urefu wa Kilomita 2.5 kwa gharama ya **Sh. 25,661,000** ambapo **Sh. 22,140,000** ni kwa ajili ya ujira kwa watekelezaji wa mradi ambao ni wanufaika 123 wa TASAF wanaolipwa **Sh. 3000** kwa siku, na **Sh. 3,521,000** ni kwa ajili ya ununuzi na

usafirishaji wa vifaa. Licha ya barabara inayojengwa kuunganisha mitaa ya eneo hilo ili iweze kufikika kwa urahisi, lengo la msingi la mradi ni kutoa msaada wa ziada kwa wanufaika ili waweze kumudu gharama za maisha. Mradi unatarajia kutekelezwa kwa kipindi cha miezi sita kuanzia Novemba, 2022 hadi Aprili, 2023. Hadi wakati wa ukaguzi mwezi Machi, 2023; mradi ulikuwa umefikia asilimia 50. Aidha, jumla ya **Sh. 5,411,000** zilikuwa zimeshatumika ambapo **Sh. 1,890,000** ni kwa ajili ya malipo kwa walengwa na **Sh. 3,521,000** ni ununuzi wa vifaa. Bakaa ya **Sh. 20,250,000** iliyobakia itatumika kuwalipa walengwa ambazo zitaendelea kulipwa na Serikali kulingana na ratiba ya malipo.

2.4.2 **Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za bei Nafuu 198 unaotekelezwa na Taasisi ya Watumishi Housing Investment (WHI)-Kisasa Hiltop, Njedengwa, Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa nyumba 198 kwa ajili ya kuwauzia watumishi wa umma ulianza kutekelezwa Agosti, 2017 na ulitakiwa kukamilika Mei, 2019 kwa gharama ya **Sh. 7,215,490,743.63**. Utekelezaji wa mradi huu unajumuisha ujenzi wa nyumba 198 pamoja na uwekaji wa miundombinu yote muhimu ikiwemo barabara, maji, umeme na madaraja. Bei za nyumba hizo zimegawanywa kwa makundi kutegemea na ukubwa wa nyumba yenyewe. Gharama za nyumba hizo ni kuanzia **Sh. 45,800,000.00** kwa nyumba ya gharama ndogo na nyumba yenye bei ya juu Zaidi huuzwa kwa Sh. **98,500,000.00.** na malipo hufanyika kwa awamu au kwa mkupuo kulingana na chaguo la mnunuzi. Kwa sasa jumla ya nyumba 196 zimeshajengwa na asilimia 94 ya nyumba hizo tayari zimeshapata wateja.

**Mheshimiwa Spika,** kamati inapenda kuipongeza serikali kuja na mradi huu wa nyumba za bei nafuu kwa ajili ya watumishi wa umma. Aidha, kamati ilibaini changamoto kwenye usimamizi wa mradi huu unaosababishwa na upungufu wa Watumishi, kamati inaishauri Serikali kuongeza watumishi

kwenye taasisi hii ili waweze kusimamia miradi zaidi ya 40 inayotekelezwa nchini kote.

2.4.3 **Mradi Na. 6203: Ujenzi wa Makao Makuu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu unatekelezwa kwa gharama ya **Sh. 22,300,000,000.** Mradi unatekelezwa kwa awamu mbili (2) ambapo awamu ya kwanza inahusu ujenzi wa jengo na awamu ya pili ni umaliziaji (*finishing*). Awamu ya kwanza ilianza mwezi Mei, 2021 na ilitakiwa kukamilika Mwezi Mei, 2022. Kutokana na changamoto mbalimbali zilizojitokeza, mkandarasi wa mradi alipewa nyongeza ya muda wa miezi sita baada ya muda wa awali kumalizika bila ya kukamilisha kazi. Aidha, baada ya miezi sita kumalizika, mkandarasi aliongezewa muda tena wa wiki ishirini na moja hivyobasi, awamu ya kwanza inatarajiwa kukamilika Mwezi Mei, 2023. Hadi wakati wa ukaguzi, mradi ulikuwa umefikia asilimia 60 ya awamu ya kwanza na jumla ya **Sh. 6,560,000,000** zimeshalipwa kwa mkandarasi na mtalaam elekezi.

**Mheshimiwa Spika,** kamati ilielezwa kuwa kwa sasa mradi umechelewa kwa muda wa mwaka mmoja kutokana na uwepo wa chemchemi ya maji katika eneo la ujenzi, na hivyo kuhitajika kuwekwa tenki la maji ya chini. Licha ya sababu hiyo, kamati haikuridhika na kasi ya utekelezaji wa mradi huu uliosababisha kukwama kwa kuanza utekelezaji wa awamu ya pili ya umaliziaji (*finishing*). Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mradi unakamilika mapema na kwa viwango stahiki.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo umeonesha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2023, fedha zilizopokelewa kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ni **Sh. 140,644,460,988.61** sawa na **asilimia 77.7** ya bajeti iliyoidhinishwa.

## 2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Kamati ilitoa Maoni na Ushauri katika maeneo Kumi na Tatu (13). Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kwa kiasi kikubwa ushauri wa Kamati umezingatiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Mfano wa ushauri uliozingatiwa, unahusu Serikali kutengeneza kanzidata ya wanaofanyiwa usaili na kufaulu kwa lengo la kuwa na orodha ya Wataalam wenye sifa wasioajiriwa, ambao wanaweza kuajiriwa bila usaili mwingine iwapo itatokea nafasi za ajira, kufatia ushauri huo Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imetengeneza kanzidata ya kieletronik ya kuhifadhi orodha ya wasailiwa waliofaulu usaili na kukosa nafasi kutokana na uchache wa nafasi, kanzidata hiyo itatumika kuajiri vijana pale nafasi za ajira zitakapotangazwa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kuipongeza Serikali kwa kuzingatia sehemu kubwa ya ushauri uliotolewa, bado kuna umuhimu kwa Serikali kuujali ushauri unaotolewa na Kamati Bungeni. Kwani uzingatiaji wa ushauri wa Kamati unawezesha Serikali kukidhi matarajio ya Wananchi wanaowakilishwa Bungeni.

## 2.6 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni za Kudumu za Bunge zimetambua umuhimu wa uzoefu unaopatikana katika mwaka wa fedha unaoisha ili kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kama ilivyoelekezwa katika Kanuni ya 117 (2) ya Kanuni za Bunge. Kamati imezingatia umuhimu huo na masharti ya Kanuni za Bunge kwa

kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kama ifuatavyo:-

2.6.1 **Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika,** Katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zilizo chini yake inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh. 785,255,545,500 Ikiwa ni Fedha za Matumizi ya Kawaida, kati ya fedha hizo Sh. 46,896,731,500 ni kwa ajili ya mishahara (PE), na Sh. 738,358,814,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo (OC).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **asilimia 17.18** ukilinganisha na Mwaka wa Fedha unaoisha ambapo bajeti ya Matumizi ya kawaida ilikuwa **Sh. 670,086,770,000** Kamati imebaini kwamba, moja kati ya sababu ya ongezeko hili ni maoni ya Kamati kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na mahitaji halisi. Aidha, ongezeko hilo linaakisi mahitaji ya kifedha kulingana na sababu mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kupanda kwa bei ya bidhaa na huduma.

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinazoombwa zinatumika vizuri. Na ili kuhakikisha hili linatekelezwa ipasavyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inawasilisha mbele ya kamati taarifa mbalimbali za utekelezaji wa bajeti kwa mujibu wa Sheria. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 3**

**JEDWALI NA. 3: Mchanganuo wa Bajeti ya Matumizi ya Kawa 2022/2023 na Uwiano wa Makadirio ya Bajeti ya Matumizi ya Kawaida 2023/2024**

| FUNGU | FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA ILIYOTENGWA KWA MWAKA 2022/2023 | MAKADIRIO YA FEDHA YA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | ASILIMIA YA ONGEZEK O |
|---|---|---|---|
| **Fungu 20** – Ofisi ya Rais (Ikulu) | 29,828,203,000 | 32,157,384,000 | 7.8 |
| **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri | 577,206,673,000 | 674,342,692,000 | 16.82 |
| **Fungu 32** – Ofisi Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | 39,541,381,000 | 45,130,005,000 | 14.13 |
| **Fungu 33** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma | 9,260,049,000 | 10,813,016,000 | 16.77 |
| **Fungu 67** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma | 5,063,849,000 | 7,139,298,000 | 40.98 |
| **Fungu 94** – Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma | 5,681,824,000 | 8,324,091,000 | 46.50 |
| **Fungu 04** – Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa | 3,504,791,000 | 3,497,811,000 | -0.19 |
| **JUMLA KUU** | **670,086,770,000** | **785,255,545,500** | **17.18** |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2023.*

### 2.6.2 Uchambuzi wa Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Sh. 196,452,507,000** kwa ajili

ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Sh. 94,490,717,000** ni fedha za ndani, na **Sh. 101,961,790,000** ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika**, bajeti ya maendeleo katika Mwaka wa Fedha 2023/2024 imeongezeka kwa **Sh. 15,451,713,000** sawa na **asilimia 8.53** ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha unaoisha. Mchanganuo wa fedha hizo ni kama unavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 4**

**JEDWALI NA. 4 – Mchanganuo wa Bajeti ya Maendeleo 2023/2024**

| FUNGU | BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024 | |
|---|---|---|
| | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE |
| **Fungu 33** | 1,500,000,000 | 450,000,000 |
| **Fungu 67** | 3,572,517,000 | 0 |
| **Fungu 30** | 80,598,000,000 | 101,394,535,000 |
| **Fungu 04** | 450,000,000 | 0 |
| **Fungu 32** | 8,070,200,000 | 117,255,000 |
| **Fungu 94** | 300,000,000 | 0 |
| | **94,490,717,000** | **101,961,790,000** |
| **JUMLA KUU** | **196,452,507,000** | |

***Chanzo***: *Randama za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, 2023.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada za Serikali kuendelea kupanga bajeti ili kutekeleza miradi mingi zaidi kwa kutumia fedha za ndani. Hata hivyo, katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kwamba, bado kiwango cha fedha ambacho kinatengwa kwa kutumia fedha za nje ni kikubwa ukilinganisha na kile kilichotengwa kwa fedha za ndani.

**SEHEMU YA TATU**

## 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

### 3.1 Maoni

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba kukamilisha uchambuzi kwa kubainisha Maoni ya Kamati yanayojenga mtazamo ambao ni msingi wa Ushauri wa Kamati. Maoni hayo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti unahitaji kupewa nafasi stahiki ili kukidhi matarajio ya Wananchi;

(b) Kuna umuhimu wa kufanikisha upatikanaji wa kiasi chote cha fedha ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii, ili kutekeleza mipango iliyokusudiwa kwa mwaka wa fedha unaoisha; na

(c) Upo umuhimu wa wakala wa ndege za Serikali kupunguziwa majukumu hasa ya umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL), ili uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali ulete tija.

(d) Serikali ifanye tathmini ya uwiano wa Watumishi wa umma mijini na vijijini, ili kuongeza ufanisi kwenye maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa wa Watumishi.

(e) Ili Mradi wa TASAF awamu ya tatu uwanufaishe walengwa, Serikali iboreshe malipo kuendana na kazi iliofanyika kwenye mradi husika na ishughulikie malalamiko ya wanufaika kwa wakati.

### 3.2 Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika,** kwa Maoni niliyobainisha kutokana na uchambuzi, naomba kutoa Ushauri wa Kamatikama ifuatavyo:-

(a) Serikali iendelee kuzingatia ipasavyo, Ushauri unaotolewa Bungeni kuhusu utekelezaji wa Mipango, Majukumu na Bajeti kwa madhumuni ya kukidhi matarajio ya Wananchi;

(b) Serikali ihamishe umiliki wa ndege zilizokodishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania, kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali kwenda kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL);

(c) Serikali ihakikishe kuwa fedha inayoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii na Taasisi zake inapatikana ipasavyo ili kufanikisha utekelezaji wa majukumu yaliyopangwa;

(d) Serikali iharakishe upatikanaji wa vitambulisho vya Taifa ili kuwawezesha Wananchi wenye sifa za kunufaika na mradi wa TASAF wanapata fursa hiyo;

(e) Serikali ione umuhimu wa kutumia matokeo ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwenye kubaini wanufaika wanaostahili kuingia kwenye mradi wa TASAF.

(f) Serikali iharakishe matokeo ya rufaa za waombaji wa kujiunga na mradi wa TASAF.

(g) Serikali iendelee kuimarisha misingi ya Utawala Bora pamoja na Kuboresha mifumo ya utendaji kazi katika Utumishi wa Umma sambambana kuboresha mishahara na maslahi ya Watumishi;

(h) Serikali iendelee kutoa Ajira zaidi ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Watumishi. Aidha, Serikali itumie kanzidata ya wasailiwa waliofanya vizuri kwenye usaili na kukosa nafasi;

(i) Serikali iendelee kusimamia na kutoa mafunzo maalumu ya mara kwa mara kwa Watumishi wa Umma ili kuwezesha utendaji kazi unaozingatia weledi na ustadi mkubwa; na

(j) Serikali iondoe mrundikano wa Watumishi wa umma walio maeneo mijini na kuwahamishia sehemu zenye Watumishi wachache hususani maeneo ya vijijini ambayo yana uhitaji zaidi.

## SEHEMU YA NNE

## 4.0 HITIMISHO

### Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika**, napenda kukushukuru wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Uongozi wenu na kutupatia nafasi ya kuwasilisha taarifa hii. Napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ambao maoni, ushauri na ushirikiano wao umewezesha Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi wa hali ya juu na hatimaye kukamilika kwa taarifa hii. Naomba majina yao yaingizwe kwenye taarifa rasmi za Bunge kama yalivyowasilishwa.

1. Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb. – **Mwenyekiti**
2. Mhe. Florent Laurent Kyombo, Mb. – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Abdullah Ali Mwinyi, Mb.
4. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb.
5. Mhe. Wanu Hafidh Ameir, Mb.
6. Mhe. Edward Olelekaita Kisau, Mb.

7. Mhe. Boniphace Nyangindu Butondo, Mb.
8. Mhe. Dkt. Alice Karungi Kaijage, Mb.
9. Mhe. Khadija Shaaban Taya, Mb.
10. Mhe. Jonas Van Zeeland, Mb.
11. Mhe. Selemani Jumanne Zedi, Mb.
12. Mhe. Tumaini Bryceson Magessa, Mb.
13. Mhe. Salum Mohammed Shaafi, Mb.
14. Mhe. Yahya Omary Massare, Mb.
15. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza, Mb.
16. Mhe. Abeid Ighondo Ramadhani, Mb.
17. Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb.
18. Mhe. Hussein Nassor Amar, Mb.
19. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb.
20. Mhe. Omar Issa Kombo, Mb.

**Mheshimiwa Spika**, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mb) kwa kuendelea kuaminiwa na kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Naibu Waziri wake Mhe. Ridhiwani Kikwete ambae ametoa ushirikiano mkubwa kwa Kamati, Aidha, Kamati inampongeza Mhe. Jenista Joakim Mhagama, (Mb) – Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu ambae wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii aliipa Kamati ushirikiano mkubwa kama Waziri wa Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia niwashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na taasisi zake kwa ushirikiano walioupatia Kamati wakiongozwa na Makatibu Wakuu wa Ofisi hiyo Ndg. Juma Selemani Mkomi na Ndg Majura Mahendeka Katibu Mkuu Ikulu.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Nenelwa Mwihambi, *ndc* kwa kuratibu vema shughuli za Kamati na Bunge kwa mujibu

wa Katiba ya Nchi. Aidha, nawashukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto, *ndc* Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Gerald Magili na Makatibu wa Kamati hii Ndg. Frank Nkya, Ndg. Praisegod Lukio na Ndg. Ganjatuni Kilemile wakisaidiwa na Bi. Theresia Jacob, kwa kuratibu shughuli za Kamati na kufanikisha kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako tukufu likubali kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mb
**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA**
19 Aprili, 2023

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Sasa Waheshimiwa Wabunge tutaanza mjadala. Tunaanza na Mheshimiwa Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly Ntate, Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, Zacharia Paulo Issaay na Esther Matiko wajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kufungua dimba katika uchangiaji wa bajeti ya Ofisi ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye kimsingi ndiye Waziri kwenye Wizara hii kwa kazi kubwa ambayo anaendelea kuifanya na kazi hii anaifanya. Nimewahi kusoma maandiko matakatifu kutoka kwenye vitabu vyetu

vitukufu kwamba Mtume Muhammad *Swallallahu Alayhi Wasalaam* alifundishwa biashara na Bi Hadija ambaye ndiye alikuwa mke wake. Huyu ndiye aliyemfundisha bihashara pamoja na Utume wake lakini biashara hiyo alifundishwa na mwanamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna Bibi mmoja anaitwa Elizabeth ambaye ni Mama yake Yohana mbatizaji ndiye aliyegundua kwamba Bi. Mariamu, Mama yake Yesu ana ujauzito. Kwa hiyo utagundua kwamba mwanamke kwa nafasi hii ambayo tumemkabidhi Rais majukumu haya hatukumkabidhi kwa bahati mbaya ni kiumbe ambaye amebarikiwa kutoka kwa uumbaji wa Mwenyezi Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *theories* mbalimbali, wanazuoni wengi wanatanabaisha kwamba kitovu cha matumizi sahihi ya rasilimali ni rasilimali watu. Rasilimali watu katika nchi yetu tumeikasimisha katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inafanyika kazi nzuri sana na tunawapongeza sana. Sera zote za Utumishi wa Umma, Sheria lakini miongozo mbalimbali yote inasimamiwa na Ofisi hii ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika haya mambo yaweze kufanyika na kukamilika ni lazima kuhakikisha kwamba wakati wote haki za watumishi zinasimamiwa ipasavyo na hili Mheshimiwa Rais ameonyesha kwa vitendo haswa baada ya kuwapandisha madaraja watumishi wote kwa wakati, lakini kulipa malimbikizo yote ya pesa ambazo watumishi wa umma walikuwa wanadai. Hali kadhalika amebadilisha kada ya utumishi na hili amelifanya kwa kutoa Muongozo wa kupandisha madaraja kwa watumishi wapya ambao wapande madaraja kwa miaka minne na wale watumishi wa muda mrefu kwa miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatakiwa ifanye kazi katika maeneo kadhaa ambayo ningeomba kutoa ushauri. Eneo la kwanza ni maadili, katika idara zote zinazosimamia maadili ya utumishi wa umma ni vizuri sana zikazingatia misingi ya utumishi wa umma. Hapa nitatoa mfano kwamba, sisi tunapokea Ripoti ya CAG ambayo Bunge linaipokea na linajadili. Ningependa kuona na Sekretarieti hii ya Maadili ya Viongozi wa Umma na yenyewe ianze kufanya hivyo kupitia ile Tume ya Utumishi kwamba Tume ya Utumishi inaleta ripoti ndani ya Bunge, lakini kwa bahati mbaya sana ripoti ile hatuijadili.

Mheshimiwa Naibu Spika kwa hiyo ningependa kushauri kwamba ifike mahali sasa angalau na Tume ile ya Utumishi ikileta ripoti ndani ya Bunge, tuifanyie mjadala ili tuweze kuona ufanisi uko kwa kiwango gani katika maeneo yote ya utumishi wa umma? Tunaweza tukagundua upungufu katika utendaji, lakini pia kuangalia haki za watumishi na msawazo wa ujumla wa utumishi katika nyanja mbalimbali za utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuna mfumo ule wa Upimaji Utendaji Kazi kwa Watumishi *(OPRAS)* mfumo ule una changamoto. Sasa ni vizuri wakaja na mfumo bora zaidi ambao utakuwa unapima *quantity* na *quality*. Tunaweza tukasema ubora lakini pia na wingi wa kazi ambazo mtumishi mmoja anafanya na hapa tuwashirikishe vizuri watu wa *e–government*. Hii mifumo tunaizungumza tu, lakini ukienda kwenye uhalisia huoni namna inavyofanya kazi na ndiyo maana wakati mwingine inazua maswali mengi hata kutoka kupoteza imani hasa linapokuja suala la ajira. Kwa hiyo niombe sana kwamba tutumie *e–government* kuhakikisha kwamba tunaboresha mifumo iweze kusomana vizuri, tuwe na kanzidata ambayo inaweza ikajua mfanyakazi mmoja anafanya kazi kwa kiasi na mwingine anafanya kazi kwa kiasi gani. Pia na usambazaji mzima wa hao watumishi katika

halmashauri zetu, katika idara na katika mashirika kwa ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina jambo lingine ambalo ningetaka nishauri na hili ni jambo ambalo kwa kweli kama Taifa inabidi tuliangalie kwa umakini mkubwa sana, suala zima la ajira. Nitatoa tu mfano katika kada moja ya elimu, kama kuna mahali tumekosea ni pale tulipoua Tume ya Mipango. Tume ile ya Mipango ndiyo ilikuwa inaweza kupanga mipango yetu ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu. Tumeiunganisha Tume ya Mipango kwenye Wizara ya Fedha, sasa hivi ufanisi wake huuoni na huko mbele ya safari tutakwenda kukumbana na tatizo ambalo ndiyo hili naomba niliseme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwenye kada moja tu ya elimu; tunavyo Vyuo 35 vya Elimu hivi ni katika ngazi hii ya *diploma* na *certificate* ambavyo ni vya Serikali. Kila chuo kinadahili wanafunzi 400 kwa mwaka, kwa maana kwa vyuo 35, tunapata wanafunzi 14,000 wanadahiliwa kwenye ualimu kwa mwaka mmoja. Ukichukua na wanafunzi walioko kwenye vyuo binafsi vya elimu viko 23, hivi vinachukua wastani wa wanafunzi 11,000, ukichanganya unapata ni wanafunzi wastani wa 25,000 wanadahiliwa kila mwaka. Kwa hiyo kwa vyuo hivi vinavyochukua wanafunzi kwa miaka mitatu maana yake una wanafunzi 75,000 wanadahili sasa hivi wako kwenye vyuo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye Vyuo Vikuu *UDOM*, St Augustine pamoja na *University of* Dar es Salaam, *DUCE* na vinginevyo vina wanafunzi, mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa 56,183. Jumla yake ni wanafunzi 131,183 hawa wanadahiliwa, wanaandaliwa kwa ajili ya soko la elimu. Soko lenyewe halipo, ajira zilizotoka ni 21,000 elimu na afya ambazo ni wastani wa kwenye elimu ni 12,000, hawa wanafunzi tutawapeleka wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nishauri, hapa sasa ndiyo tunakuja kwenye Tume ya Mipango lakini pia eneo la utawala bora. Kuna umuhimu gani kuendelea kuzalisha walimu kama kwenye soko hatuwahitaji? Ifikie mahali tupunguze utitiri vya vyuo hivi vinavyotoa kada za elimu kama hatuna nafasi ya kweza kuajiri ili watoto wetu wasome masomo ambayo watakapokwenda kwenye soko wanaweza wakayafanyia kazi na ualimu kwasababu ni ambalo ni mahususi maana yake akishasoma hawezi akafanya kazi nje ya eneo hilo. Kwa hiyo niombe sana jambo hili tulifanyie kazi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Kengele ya pili hiyo.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, inakushukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly James Ntate, ajiandae Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii, leo Mheshimiwa Rais, nimeshamshukuru kwa niaba ya watumishi kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu. Leo niwapongeze Mheshimiwa Simbachawene kwa kuaminiwa kuwa mdau wa Utumishi wa Umma nchini, nikupongeze Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyokuwa naangalia sifa zao wote ni Wanasheria, kwa hiyo kuna makusudi na sababu kuwapeleka Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Waende wakarekebishe sheria, wakaangalie Kanuni na wakaangalie miongozo iliyopitwa na wakati ndani ya utumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nampongeza Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete nilimwambia hivi, kuna sheria ambazo zilitungwa kabla yeye hajazaliwa lakini bado ziko kwenye utumishi wa umma, tumezifanya nazo kama ni imani ya Dini kama ni Biblia na Qurani ambavyo huwa havibadiliki. Niwaombe wakazibadilishe. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nasema hivyo kwa sababu gani? Kuna *standing order* inayosema kwenda na nyaraka ya Serikali nje ya ofisi ni makosa, lakini leo hii tunatumiana hata kwenye vishikwambi hizo nyaraka za Serikali. Leo hii tunatumiana kwenye *e-mai,l* je, ukiambiwa umefanya kosa utatokea wapi? Wakati kuna *standing order* inayosema hivyo, ndiyo maana ya sheria ninazosema wakaziangalie ni za aina hiyo. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitaongelea ajira kazi kubwa ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma ni ajira, ni kuajiri watumishi ndani nchini, lakini leo TAMISEMI anaajiri, tukikaa Wizara ya Afya itaajiri, hizo ajira tunazi–*control* vipi? Huko nyuma tulishafanya, Wizara zikapewa mamlaka na idara za Serikali kuajiri. Shida tuliyopata Serikali ikaamua kuunda Sekretarieti ya Ajira na Katibu wake wa kwanza akiwa ni Daudi Xavier ambaye sasa hivi ni Naibu Katibu Mkuu, Utumishi wa Umma, ni kwa sababu waliona haiwezekani, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ndiyo iangalie ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya matatizo tunayopata kwamba wameajiri kwa upendeleo wamefanya nini? Ni kwa sababu hakuna ambaye ndiye anayesimamia. Kwa mfano Mama Jenista Mhagama akiwa Waziri wa Utumishi alituambia amefungua kanzidata tukakupongeza, hivi kama hiyo kanzidata ingekuwa inatunzwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na wao ndiyo wanaajiri, leo hii kulikwa na sababu ya kutangaza kazi hizi tulizotangaza? Tungerudi kwenye kanzidata tukaangalia wale walioomba, nafasi zikawa kidogo

wakabaki ndio wangeajiriwa, kwa sababu tayari walikuwa wameshafanya *interview*. Hii ingepunguza gharama ya Serikali za kurudia tena kwenye kuajiri. Hilo niwaombe Wanasheria wangu wawili hapo wakaliangalie upya, wasimame kwenye *instrument* yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna miundo inayokinzana, leo hii ukiangalia kwa *RAS* pale ndiyo anasimamia Halmashauri lakini niongelee kada ya sheria tu iwe mfano. Mwanasheria aliyeko kwa *RAS* ambaye kazi yake ni kusimamia wanasheria walio kwenye Halmashauri, yeye anaitwa Afisa Mkuu na analipwa mshahara wa kimadaraka lakini wenzake walio kwenye Halmashauri ni Wakuu wa Vitengo na wanalipwa mshahara wa kimadaraka siyo wa kimuundo, huyu analipwa kimuundo hawa kimadaraka. Sasa mtu anayelipwa mshahara wa kimuundo wa Afisa Mkuu atamsimamia ambaye ni Mkuu wa Kitengo analipwa marupurupu yote? Kazi tunaitegemea ipatikane sawa? Ndiyo maana mikataba mingine inapita ya kiajabu ajabu kwa sababu huyu mmeshamdogosha hawezi kumsimamia mtu ambaye anamzidi mshahara na cheo, hilo nalo mkaliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee faragha ya Viongozi. Viongozi wetu tunasema Mawaziri, Makatibu Wakuu, Wakurugenzi na ninyi Waheshimiwa Wabunge. Kwa nini inaonekana labda viongozi wa sasa hivi hawana maadili mazuri? Ni kwa sababu tumewaondolea haki yao ya faragha. Viongozi wetu, kuwa Waziri Mheshimiwa Jenista hakukutoi kwenye raha zako zingine. Zamani mlikuwa na faragha, mlikuwa na *Leaders Club*, mlikuwa na Mikoani sehemu za kukaa viongozi wenyewe kwa wenyewe. Kwa hiyo, pale ukikaa hata ukiburudika na bia moja ukadondoka wanakubeba viongozi wenzako na hautalisikia mtaani. Leo hamna pa kukaa mkafanya faragha zenu na hilo limeonekana kama hakuna maadili, lakini maadili ni yale yale, watu ni wale wale.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe *Leaders Club* ikarudi Menejimenti ya Utumishi wa Umma, hapa Dodoma mjenge *Leaders Club* ya Viongozi kwenda kupumzika baada ya saa za kazi, na hii inasababisha hata *document* za Serikali ku- *leak*. Kwa sababu zamani, ukienda *Leaders Club* unampelekea Katibu Mkuu *document* au Waziri aliyepo pemebeni ni Waziri mwenzake au Katibu Mkuu mwenzake, lakini leo tukikuletea Morena kuna simu zingine zina mita 200 zinavuta *document* unaikuta magazetini. Turudishe hizo faragha.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ndugu zangu niongelee Vyuo vyetu vilivyo chini ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hivi vyuo kila chuo kilianzishwa kwa maana yake. Chuo cha Uhazili Tabora kilikuwa ni kutoa Masekretari mahiri, wenye *stenography*, leo tunao? Kwa sababu chuo kile sasa tumekibadilisha, kumekuwa na miundo mingi pale, masomo mengi pale kimekuwa ni cha kibiashara. Pia iko wapi *IDM* Mzumbe ambapo watu walikuwa wakishakuwa Maafisa Wakuu mnapelekwa pale kufundishwa uongozi, kufundishwa uzalendo, kufundishwa maadili. Leo iko wapi? ndiyo maana tunaona maadili hayapo, watu wanateliwa hawajapelekwa mahali popopte kupikwa. *IDM* imebadilika leo ukitafuta historia yake iliyoianzisha haipo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Chuo cha Utumishi wa Umma, Magogoni kilikuwa ni chuo cha ku-*refresh* watumishi waliokazini! Leo hii tumeweka wanafunzi wanaotoka shuleni moja kwa moja, yale maadili yake yameondoka. Niwaombe muende mviangalie vyuo hivyo. Leo hii hatuna wa kuzalisha hata ma-*stenographer* wa kuja hapa Bungeni wa kwenda Mahakamani wa kwenda kwenye Taasisi za nje zinazokuja hapa. Hawapo hawazalishwi kwa sababu tayari vyuo tumeshavichanganya.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kengele ya pili.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga hoja mkono.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kwezi, jiandae Mheshimiwa Zacharia, jiandae Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba nichukue nafasi hii na mimi kuwa miongoni mwa wachangiaji wako wa leo.

Kwanza niseme kabisa bajeti hii naiunga mkono, mbili niwapongeze sana Waziri na Naibu Waziri pamoja na Mtendaji Mkuu na timu yake yote kwa kazi nzuri ambayo wanafanya katika Utumishi wetu wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo ambayo ninapenda kuyazungumzia lakini nisipogusa maslahi ya watumishi katika Jimbo la Kaliua na nchi nzima nitakuwa sijatenda haki kwa wananchi, nitakuwa sijatenda haki kwa watumishi wa umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo Wilaya, zipo Halmashauri, zipo *RAS*, zipo Wizara, mpaka sasa bado zinadai malimbikizo. Kwa hiyo, naomba ndugu zangu hawa wahakikishe kwanza malimbikizo ya mishahara yanalipwa kwa wakati, mbili wahakikishe yale madeni yote wanayodaiwa kwa mfano Kaliua kuna madeni mpaka sasa watumishi bado wanadai, madai ya uhamisho, madai ya likizo, madai ya matibabu Milioni karibu 170, wawape wale watumishi wanafanya kazi nzuri sana ya kuijenga Kaliua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi ambalo ningependa kulichangia kwanza niombe Wizara hii, ninapata kigugumizi ninapokuwa kwenyeJimbo langu. TAKUKURU

hawana Ofisi ya Wilaya, TAKUKURU wamepanga kwenye nyumba za watumishi, hivi huyu mtumishi anapo - *misbehave* TAKUKURU anamchukuliaje hatua wakati yeye ni mpangaji wake? Badala yake utamchukulia hatua leo, keshokutwa na yeye anakupandishia kodi unakuwa unahama hama. Kwa hiyo, ninakuomba Mheshimiwa Wakili Msomi, tena mko wawili wote hapo watani zangu. Niwaombe sana kwenye bajeti hii tafadhali sana Kaliua tunahitaji Ofisi ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, TAKUKURU wa Kaliua wakiongozwa na Ndugu Abdallah kazi wanafanya nzuri sana. Kwa hiyo, kama wanafanya kazi kwenye mazingira magumu hebu tupeni ofisi ili wafanye kazi kwa uzalendo wao kuokoa fedha za umma na mambo mengine mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda pia kushauri kwenye suala la wastaafu, wastaafu wetu jamani maisha asilimia 90 ya watumishi wa umma walioajiriwa yanaishia kazini. Unaingia kazini una miaka 18 pengine mpaka miaka 60 hii ni asilimia 90 ya maisha yake, sasa wanapostaafu nini kinatokea? Nje ya usumbufu wa mafao yao yote, usumbufu mkubwa wanaokuja kuupata mimi nasema ni kwenye *pension,* sijaona utumishi wamekaa chini wanasema, umestaafu ile *pension* wanakupa mshahara wako wa mwisho. Hivi kwa maisha yanavyozidi kubadilika mtu umestaafu ukabahatika kuishi miaka mia moja na, kama wazazi wangu wako Kaliua pale wana miaka mpaka mia moja, bado ile ile hela waliostaafu nayo ya *pension* haiongezeki.

Mheshimiwa Naibu Spika, *challenge* ya maisha haya tunakwenda hivi mpaka lini? Kwa hiyo, ni lazima tuangalie hawa wastaafu wetu angalau kwenye kile cheo alichostaafu nacho si kuna watumishi wanaendelea nacho? Kwa mfano, Wakurugenzi wana SSE kwa hiyo wale ambao wana hiyo na walistaafu kwenye *level* ile basi tutegemee watakapobadilika wa sasa na wale wastaafu *pension* zao ziweze kubadilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo la msingi jingine niliseme la *team work,* naomba mje mjifunze Kaliua. Kwa kweli kuna *teamwork* nzuri sana kuanzia Mkuu wangu wa Wilaya Rashid Chuachua, yuko vizuri. Niko Jimboni lakini kule akizunguka atamsema Mama Samia miradi mizuri sana, atamsema Mbunge Kwezi miradi mizuri sana, atawasema Madiwani tena wa Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu nataka niwaambie hawa viongozi nimefurahishwa sana na Utumishi kitendo mlichokifanya juzi cha *induction course* kwa Wakuu wa Wilaya, wafundisheni kwa sababu mtu anatoka sehemu hajui majukumu ya Mkuu wa Wilaya, hajui majukumu hata ya wale anaofanya nao kazi ana-*share* vipi, *team work* inakuwaje hapo? kwenye Sheria Namba 8 ya 2002, Kanuni za Septemba 2003 mmeongelea Kifungu cha 65 *teamwork*. Sasa *Public Servant* maeneo mengi unakuta wengine wanafeli kwa sababu utakuta Mkuu wa Wilaya fulani amekuwa kibaraka wa mgombea fulani, Mkurugenzi fulani anafeli sehemu fulani, sasa haya yanatuangusha, lakini mkishawaeleza kama mlivyowaelimisha juzi kwa kweli kile kitendo kinaendelea kutuimarisha. Nilitaka niwathibitishie Utawala Bora pale tupo vizuri, tunahitaji tu kwenye TAKUKURU mtupatie hiyo ofisi, tunahitaji na gari ya TAKUKURU ili wakina Abdallah na *team* yake waendele kufanya kazi vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo ningeweza kulisema Mheshimiwa Rais amefanya kazi kubwa sana hivi karibuni ya kuhakikisha mishahara inaongezeka. Mishahara imeongezeka kwenye mazingira ambayo vitu vingine vyote kulikuwa na mfumuko wa bei, watumishi hawajaona *impact* kubwa. Nataka niwashauri, mwaka huu mpaka sasa tunaongea ni mwezi Aprili hakuna *promotion* iliyofanyika mwaka huu. Sasa tunamaliza mwaka bajeti ilishatengwa kwamba ile mishahara yao ya *promotion* ilitengwa kuanzia Tarehe 01 Julai, sasa tunakwenda mpaka

Tarehe 30 Juni, hapa katikakati imebaki miezi minne, mnapokuja kutoa mnatoa *with effect* kwenye Tarehe ambayo mmetoa barua zenu za *promotion*, bila ku-*consider* kwamba hii bajeti ilikuwepo toka Tarehe 01 Mwezi Julai, naomba mlizingatie hili ili watumishi wa umma waneemeke na maslahi mbalimbali ya kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichangie pia kwenye eneo moja kubwa sana la *allocation* ya *human resource* na maadili, hapa ndiko kuna shida. Hivi *vetting* mnazifanyaje ndugu zangu? Yaani unafanya *vetting* leo mtumishi anateuliwa kesho, mambo hayakwenda vizuri, mwezi mmoja mnatengua. Hawa ina maana hamjafanya vizuri *vetting* si ndiyo hivyo? Sasa mimi nilitaka nishauri kwamba chunguzeni kwa kiasi cha kutosha na mtoe majibu kwa wakati. Mnaziumiza Halmashauri na *vetting* hizo, kuna Idara mtu anakaimu na kukaimu na kukaimu kibaya zaidi hamuwaambii kwa wakati kwamba huyu hafai, unakuja kukuta alishakaimu hata miaka miwili, miaka mitatu halafu unamletea mtu mwingine, matokeo yake kunakuwa na *conflict of interest*. Mtu alishajenga matumaini, alijenga na mambo mbalimbali haya hatuyafanyi, niwaombe sana Mawakili Wasomi zingatieni hizo sheria kwa kuhakikisha wananchi wetu wananufaika vizuri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwataja hawa wanaokaimu mimi nataka niongelee *crisis* kwenye suala la ajira. Ajira tumefanya vizuri na jana tumeshauri vizuri kweli, lakini hizi ajira mimi nataka muangalie na kwenye *private sector*. *Private sector* kuna miradi mikubwa inaendelea, pale Kaliua kumeanza mradi wa kukarabati ile reli ya kutoka Kaliua kwenda Mpanda na sasa kuna *lot* ya Tabora - Kaliua mpaka Kigoma. Watu ambao wanakuja mimi nilitegemea wananchi wa Kaliua, wananchi wa Urambo wananchi wa Ulyankhulu mule ambako mradi unapita, sasa wananchokifanya sasa hivi wanahama na watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Watumishi ametoka nao hapo Makutupora watani zangu Wagogo wame-*enjoy* wamenufaika tena tumewafundisha ujanja Wanyamwezi wakifika kule wanahama nao sasa wanaleta rundo kule. Wale Wanyamwezi wangu wanabaki benchi maana yake nini? Hivyo, katika kwenye hii miradi mfuatilie siwaambii huu ni utani, hata sasa hivi mkitaka m - *prove* nendeni pale kwa sababu wamesimika pale Zugimlole kuna stesheni pale, utakuta wamehama na watu zaidi ya 20 nikawa nauliza hawa? Eti hawa ni mafundi. Mafundi 30 halafu fundi mwenyewe kazi yake ni kubeba tofali wananchi wa Kinyamwezi kule hawana nguvu hizo? Wafipa hawana nguvu hizo? Waha hawana nguvu hizo? Siyo kweli. Kwa hiyo nataka niwaambie haya tukiyafanya tutajenga heshima ya Mama vizuri sana, tutaondoa malalamiko ambayo hayana tija vizuri sana.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sahani hii nilitaka niwashauri kitu kingine kuhusu uboreshaji wa miundo hii. Miundo inakaa kwa muda mrefu sana, mabadiliko yanaenda na sayansi na teknolojia, ninyi bado mnashangaa huku, shida ni nini kwanza? Kwa nini hamjiimarishi? Kibaya zaidi hapa kwenye uimarishaji wa Ikama nilitaka niseme hapa, Halmashauri kule tunawaomba kwamba mwaka huu Kaliua tunataka tuajiri watu 205 tukileta huku ninyi mnakuja kutupa chukua watu 15 hivi kweli tatizo litaisha. Ninachowaambia kwa mfano, mimi Kata zote za Jimbo la Kaliua hakuna Afisa Maendeleo ya Jamii kwenye Kata. Hayo maendeleo wananchi wanahamasihwaje? wamelima tumbaku vizuri sana, wangetegemea Afisa Maendeleo wa Jamii atapita kuwaelimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuliwaambia jamani Kata zetu ziko 13 zinahitaji hiki na hiki, bado mnatakiwa mchukue ushauri wangu. Baada ya kuyasema haya siwezi kuzuia bajeti yao hawa, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Zacharia Issaay ajiandae Esther Matiko, jiandae Omar Issa Kombo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza niungane na wenzangu wote kumshukuru Mwenyezi Mungu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote niipongeze Serikali kuna kazi nyingi sana zimefanyika katika Jimbo la Mbulu Mjini, kazi kubwa ambayo ilikuwa imeshindikana kwa muda mrefu. Aidha nichukue nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu kabla ya wakati huu kulikuwa na miradi ambayo ilishindikana kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue pia nafasi hii kuiopongeza Serikali kwa kazi kubwa iliyofanyika na naomba nichukue nafasi hii kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii. Kwanza Jimbo la Mbulu Mji Manyara kule lina sura mbili, kuna Vijiji na Mji. Eneo la vijiji ni Kata 10 eneo la Mji ni Kata Sita, katika hali kama hiyo kuna changamoto kubwa sana hasa kwenye upande wa watumishi. Wakati tunagawanyika mwaka 2015 Halmashauri ya Mbulu Mji ilipokea asilimia 40 ya watumishi, hadi tunapoongea sasa hivi hatujapata hata kujaza zile asilimia ambazo zilipungua kulingana na Mji kupokea asilimia 40 kwa 60. Kwa hiyo, tumeomba mara nyingi ajira za ujazaji ukiacha hizi ajira mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu ni mkubwa sana. Kwa mfano, kwenye eneo la Watumishi wa Kilimo wako Watatu badala ya 54. Katika hizo Kata za Vijijini kuna Vijiji 34. Katika Vijiji 34 vilivyoko watumishi hawa wa kilimo na mifugo walikuwa muhimu sana, kuna upungufu wa watumishi 54 wa kilimo na watumishi 52 wa mifugo, ukijumlisha ni watumishi 100.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilio changu ni kwamba nimeenda Wizara ya Utumishi mara nyingi, bahati mbaya

Mawaziri wamebadilika lakini ofisi ni ile ile. Nikitetea walau hizi nafasi za ujazaji zijazwe ili wananchi wangu wapate huduma bora kulingana na upungufu huu wa watumishi. Hizi ni kada mbili tu zina upungufu wa watumishi 100 sijaenda kwenye kada zingine. Mfano mwingine ni Vijiji na Mitaa tulizogawiwa 2014, kulikuwa na mahitaji ya Watendaji wa Vijiji na Mitaa zaidi ya 94 hadi sasa wamejaza nafasi za 30 tu na kila unapoenda unaahidiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu au hoja ya msingi zaidi ni kwamba hata yule aliyestaafu mshahara wake anapokea nani? Mheshimiwa Waziri kama alistaafu yuko kwenye mshahara na mshahara wake pengine ulikuwa unaweza kuajiri hata watumishi watatu, wanne, kwa maana ya yeye anaweza akawa anapokea zaidi ya Milioni Moja na watumishi wapya wanaoajiliwa kwa kada tofauti tofauti wanaweza kuajiliwa mpaka Watatu kwenye nafasi hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu hapo ni kwamba hatuangalii *data* zetu kwa umakini na maeneo gani yanaathirika sana. Ukizungumza Maafisa hawa ambao ni ngazi za Kata na Vijiji wakakosekana moja kwa moja uwezo wa utendaji wa Serikali na utoaji wa huduma kwa Serikali unapungua kwa asilimia kubwa sana. Kwa hiyo, nilikuwa naona wakati fulani kibali hiki siyo hisani unapoona mtumishi wako amestaafu na kinaombwa mwezi wa Machi kila mwaka kwenye bajeti lakini hakuna kinachotokea. Ninaomba Mheshimiwa Waziri eneo kama hili linahitaji kibali cha ajira mbadala na kama Halmashauri ina Kata 17 ina Vijiji 34 ina Mitaa 58 wananchi wa eneo la Mbulu Mji, eneo la Mji ni ndogo. Eneo hilo la Mji lilichanganywa pamoja na eneo la vijiji, lengo kubwa lilikuwa kwamba kutokana na jiografia ilivyo, na kwa kuwa Halmashauri iligawanywa kwa lengo la kupeleka huduma karibu na wananchi, basi tusiwapeleke wananchi wale wa upande wa Vijijini waende Jimbo la Mbulu Vijijini ili wapokee huduma. Kwa hiyo naomba sana

chonde chonde, nendeni kwenye *data* muangalie Halmashauri ya Mbulu Mji imeomba nafasi ngapi za ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo jingine naomba nichangie kwa upande huu wa wenzetu ambao wako katika eneo la TAKUKURU. TAKUKURU Wilaya ya Mbulu ina miaka zaidi ya 15 inapangisha jingo, TAKUKURU Wilaya ya Mbulu pia ina upungufu wa watumishi. Kwa hiyo kuna hoja nyingi za TAKUKURU katika Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Wilaya ya Mbulu hazifanyiwi kazi kwa wakati kulingana na wale watumishi walivyo wachache. Kama inawezekana hoja nyingi zinazokwama kwa ajili ya utekelezaji wa Maafisa, basi ngazi za Mkoa na ngazi zingine ziangalie namna ya kutatua tatizo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ndege za Serikali. Duniani kote hakuna Serikali inaweza ikafanya biashara ika – *perform* au ikafanya ufanisi zaidi, ushauri wangu kwenye eneo hili la ndege za Serikali hasa za *ATCL* kwa maana zile zinazokodishwa kwenda *ATCL* basi Serikali ibinafsishe ili yenyewe ipewe gawio ama ipewe sehemu ya hisa, kwa sababu ni eneo ambalo limelalamikiwa sana na taarifa za *CAG,* kwamba zinaonesha zinaipa Serikali gharama kubwa na hakuna mafanikio zaidi. Kwa nini nazungumza hivi? Ninazungumza hivi kwa sababu ukiacha ndege za Viongozi wa Serikali hizi ndege zingine zote kwa kukodisha huwezi kupata mrejesho wa mafanikio ya mapato na ufanisi wa kiuchumi kwa maana ya uzalishaji. Kwa hiyo, eneo hili linahitaji zaidi sana lipate utaratibu wa kukodishwa ama wa kubinafsishwa kwa utaratibu wa wazi wa Serikali kusubiri gawio ama sehemu ya faida iliyotarajia kutoka mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni eneo la ajira. Vijana wengi wanatoka vijijini, wanakuja huku Makao Makuu ya Nchi kufanya usaili, kule wanakotoka wanakopa, wanapokuja huku wanapata gharama kubwa, ushauri wangu katika eneo hili Serikali iangalie utaratibu wa

kuwezesha Sekretarieti ya Ajira kufanya usaili kikanda ili kupunguza gharama kubwa ambayo watoto wa wananchi na vijana wetu hawa wanapata gharama kubwa na kadri wananvyokuja huwa wanakosa kwa sababu nafasi tunazopata ni chache na hizo nafasi chache wanapokuja wengi baadae inageuka kuwa kilio.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna wakati tulipitisha hapa Bungeni kikokotoo kwa Watumishi wa Umma. Wastaafu wamelalamikia sana eneo hili. Hata kama hatusikii, tuliona kuwa ni muhimu, Maazimio ya Bunge siyo Msahafu. Tutazame upya kilio cha wale wengi ambao ni Watumishi wa Umma, walishaitumikia nchi hii, na sasa wanalia kule. Hawa ni watumishi, waliitumikia nchi hii kwa uzalendo mkubwa sana, wanacholalamikia ni umri wa Mtanzania umeshuka. Kwa kuwa umri wa Mtanzania unashuka, na kikokotoo kile kinakuwa kidogo. Nadhani tuna jukumu kubwa la kutazama kama Bunge na kama Serikali, ili tuone hao watumishi na wastaafu wanachokizungumza katika ile hali ya uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na muda, naomba nizungumzie pia eneo lingine la *TASAF*.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, ni kengele ya pili hiyo.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Naibu Spika,…

**NAIBU SPIKA:** Ni kengele ya pili hiyo. Ukiwa na mengine, mwandikie Waziri.

Mheshimiwa Matiko, halafu Mheshimiwa Omar Issa Kombo, Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, wajiandae

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuweza kunipatia nafasi kuchangia kwenye hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Nina hoja kadhaa, kama nne hivi, lakini nitaenda kuzichangia kwa kadiri nitakavyoweza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taifa lolote lile ili liweze kuendelea lazima liwe na usimamizi madhubuti wa rasilimali watu kuhakikisha kwamba wanatenda kazi kwa ufanisi ili kuweza kuleta tija. Hata Waziri wakati anawasilisha hapa ameonesha bayana kwamba, tukiwa na rasilimali watu za kutosha basi uchumi wa nchi yetu utasonga kwenda kwenye uchumi wa kati. Tumekuwa kama Taifa kwa kweli, tukishuhudia wimbi kubwa la upungufu wa rasilimali watu. Maana tusipokuwa na rasilimali watu wa kutosha wenye uwezo, wenye weledi na waadilifu, tutaendelea kushuhudia utolewaji hafifu wa huduma za kijamii, ubadhirifu wa fedha za umma na mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiyo wana mamlaka yote ya kutoa vibali na kuhakikisha kwamba Watanzania wenye sifa wanaajiriwa, ili kuwepo na ufanisi kwenye taasisi zetu. Nitaenda kuainisha upungufu uliopo hasa kwenye sekta ya afya, sekta ya elimu na Serikali kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu wa rasilimali watu kwenye sekta ya afya ni mkubwa sana. Watanzania sasa hivi tupo milioni 61,700,000 na kitu kwa mujibu wa sensa ambayo imepita. Tuna upungufu wa zaidi ya wafanyakazi 82,000 kwenye sekta ya afya. Nilikuwa napitia Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, *page* 134. Inasema: "Kuongezeka kwa watumishi wa sekta ya afya kutoka 86,000 mwaka 2015 kufikia 100,000 mwaka 2020", ambapo tumeongeza watumishi 18,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani kwa miaka mitano, kama Taifa, na upungufu tulionao kabisa mmeona *it is a statement* kuweka kwenye Ilani ya Uchaguzi kwamba mmeweza kuajiri watu 18,000! Kwa maana nyingine, tangu tupate Uhuru mnaandika mmeajiri watu 100,000 kwenye sekta ya afya. Kweli! Tuko milioni 61, *if you take the ratio* hapo, ina maana mtumishi wa afya bila kujali *category* aliyonayo, anatakiwa kuhudumia Watanzania 600,000. *Are we serious?* Halafu tutegemee tuwe na Watanzania ambao watahudumiwa wawe na afya njema, wafanye kazi ya utendaji kwenye uchumi wa nchi na kuweza kuchechemua uchumi wa nchi yetu? *You are not serious. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami naona kwa sababu hata Wizara zikija hapa zinasema, kuweza kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi, wanakuwa wamewekwa kwenye *comfort zone*. Sasa ukiwekewa kwamba uajiri watu 18,000, au 20,000 au 30,000 kwa miaka mitano, tayari wamekuwa kwenye *comfort zone*. Ndiyo maana hata wakiomba vibali vya kuajiri uta-*relax* tu, Ukiangalia ilani yenyewe imekupa idadi ndogo ya watu. Hatuwezi kufika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija kwenye sekta ya elimu, ndiyo kabisa. Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa Mwaka 2021/2022, mpaka 2025/2026 umesema kabisa kwenye sekta ya elimu, shule za msingi…

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nataka kumpa Taarifa mwongeaji. Kwanza nampongeza kwa kuisoma Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Tumegundua kwamba anaisoma na anaielewa vizuri. Nimwambie tu, tulishaajiri 7,000, na sasa hivi tumetangaza 21. Kwa hiyo, tumeshaipita ilani na tunaendelea kuajiri. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Nicheke kidogo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipokuwa naapa hapa, napewa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kama nyenzo kuhakikisha Serikali iliyopo madarakani na chama ambacho kimepewa madaraka na wananchi wanatekeleza na kuleta maendeleo kwa Watanzania. Sasa dada yangu Munde uwe unasoma kwa kina, unachukua na *figure* nyingine unalinganisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia upungufu wa wafanyakazi kwenye sekta ya afya na elimu, ni zaidi ya 223,000. Mnazungumzia kuajiri 7,000, umeajiri 20,000, kweli! Tutachukua miaka mingapi kuweza kuajiri hao wote wakati watu wanakua? Yaani leo miaka 62 ya Uhuru, mme-*document* hapa, watu 100,000. Ungetakiwa tu ukae chini. Ngoja niendelee. *(Makofi/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Ehe.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, wamesema kwa elimu, shule ya msingi, *ratio* ni mwalimu mmoja wanafunzi 50; Mpango wa Tatu wa Maendeleo. Kwa sekondari *ratio* ni mwalimu mmoja afundishe wanafunzi walau 20. Ukiangalia jinsi wanavyotoa ajira hizi, na ambapo nashukuru kwenye elimu sasa hivi, maana nimepitia hapa, ile miaka mitano hamkuajiri kabisa kwenye sekta ya elimu. Sasa hivi walau wametangaza 21,200 na 13 kwenye elimu, lakini bado.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia upungufu tulionao kwenye sekta ya elimu ambao ni 223,000, ukiangalia na uwiano, ina maana unazungumzia shule ya msingi, *on average* ni kwamba mwalimu mmoja kwa wanafunzi 120, na kuna nyingine mpaka 200 au 300. Maana unakuta shule ina wanafunzi 1,000 au 2,000 lakini walimu watatu au wanne. Sasa ukiangalia hiyo *ratio* ni mwalimu mmoja kwa wanafunzi 400. Tutafika kweli! Yaani leo tutegemee wanafunzi wa shule za umma wafaulu kama za binafsi! *We will be joking. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani leo utegemee mwanafunzi wa shule ya umma afaulu! Anapewa mtihani wa kujipima sawa na anaopewa Nicole wangu? *Never on earth.* Hatuwatendei haki Watanzania hawa. Tujitoe, tuajiri kama Taifa, kama ambavyo tunatoa matrilioni kujenga barabara na mambo mengine, tuwekeze kwenye rasilimali watu. Tanzania ndiyo nchi pekee ambayo iko nyuma, inaenda sijui sayansi ipi ya kutothamini rasilimali watu? *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, muda wangu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Matiko ukae. Taarifa.

**TAARIFA**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nadhani Mheshimiwa Mbunge anaposimama angepongeza juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita ambazo zimejionesha katika kushughulikia tatizo la rasilimali watu nchini. Ninachotaka kumwambia ni kwamba, utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ni utekelezaji wa miaka mitano, hapa tulipofika ni kama tunaelekea tu nusu ya safari. Hata hivyo, ameona juhudi

nyingine tofauti tofauti za kuhakikisha kwamba, tatizo la rasilimali watu nchini linatatuliwa ikiwa ni pamoja na kuanzisha mfumo wa kufanya tafiti na kuangalia uwiano mzima wa watumishi tulionao ili waweze kutoa…. *(Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Hebu, upande huu kaeni kimya. Upande huu kaeni kimya.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, mnakataa maamuzi ya Kiti!

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo, unakataa maamuzi ya Kiti Mheshimiwa Ester Bulaya! Nikusomee Kanuni ya kupinga maamuzi ya Kiti?

Kaa kimya, kaa kimya. Usilete mambo ya kujua humu ndani, kwanza huna unachokijua.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** *(Hapa hakutumia kipaza sauti)*

**NAIBU SPIKA:** Wala usinijibu mimi. Nikikusomea kanuni hapa utatoka na hutarudi tena mpaka miaka mitatu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri endelea.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE NA URATIBU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana *commitment* ya Serikali yetu kuhakikisha inatatua tatizo la

watumishi, imeanzisha mfumo wa *Human Resource Assessment,* ili kujua ukubwa wa tatizo na kupitia ajira na mikakati mingine tuweze kutatua tatizo hilo. Kwa hiyo, Serikali haijakaa kimya, imefanya juhudi kubwa na itaendelea kutekeleza mipango mbalimbali kutatua tatizo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei taarifa yake. Hapa tupo Wabunge tunaishauri Serikali. Mchukue mawazo yetu myafanyie kazi, mweze kuboresha hapo mlipo, maana mnajikongoja, muende kwa kasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Raslimali watu ndio kitu muhimu cha kuchechemua uchumi wa nchi. Mtajenga miundombinu; na hapa kwenye Ripoti ya CAG ameainisha kwamba, amepitia akaona kwenye Halmashauri 16 kuna vituo vya afya, kuna zahanati zimekamilika za Shilingi bilioni 4.93 zimeshindwa kufanya kazi kwa sababu ya upungufu wa Watumishi wa Umma hawapo. *Then* tuna-*advise* mnasimama kupoteza muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, mwaka wa fedha 2021/2022…

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti wa Kamati inayohusika, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe Taarifa Mheshimiwa mchangiaji kwamba, ni kweli kuna upungufu wa watumishi wa sekta ya afya na elimu, lakini upungufu umeonekana kutokana na kuongezeka

kwa ujenzi wa shule za msingi, ujenzi wa vituo vya afya na ujenzi wa zahanati. Ujenzi wa vituo hivi umekwenda kuonesha upungufu wa watumishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasi kama Bunge, ukipitia Taarifa ya Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naye Mbunge akiwa mmojawapo, tulipitisha maagizo ya kuiomba Serikali iongeze wafanyakazi na Serikali imetekeleza na hayo yanafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa hiyo. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunafurahi sana majengo kujengwa, lakini inaonesha mlikuwa hamna mpango. Kwa sababu, ukijenga majengo ni lazima yaende sambamba na kuajiri rasilimali watu. Hatuwezi kujenga majengo tunaacha popo wanakaa, halafu tunakaa tuna-*relax* hapa wakati hela za umma zinatumika bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuwe na *value for money.* Mathalani mwaka 2021/2022 tu tuliidhinisha bajeti ya kuajiri watumishi 10,800 kwenye Serikali Kuu. Vibali viliombwa vya watumishi 20,000, lakini vikaidhinishwa 7,000 tu, na bajeti tumepitisha hapa kwa watumishi wote. Kwa hiyo, unaona hawatoi uzito kwenye kuhakikisha kuna rasilimali watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nihame hapo, maana naona viti havitulii.

**MBUNGE FULANI:** Endelea!

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ukaimishaji wa watumishi wa umma kinyume cha sheria na kanuni ambazo zinasema usizidi miezi sita. Kwa mujibu wa Ripoti ya *CAG,* kuna watumishi 258; kwenye taasisi 40 tu walizopitia, wanakaimishwa nafasi kati ya muda wa miezi sita mpaka 108. Yaani unamkaimisha mtu kwa miezi 108, *you are saying about nine years,* hujamwona kama ana sifa ili umthibitishe awe mfanyakazi kamili, na kama hana sifa umweke pembeni mteue mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi mimi ukinikaimisha kwa miaka tisa, kwanza nakuwa hata siwezi kufanya kazi kwa ufanisi, kwa sababu, sina mamlaka kamili, umenikaimisha tu. Kwanza pia, unanipa majukumu mengi, nina kanafasi kangu kengine huku, na huku umenikaimisha. Miaka tisa unamkaimisha mtu, miaka tisa! Hii siyo sawa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kengele ya kwanza hiyo. *(Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, dakika mbili, wamesimama wengi sana, dakika mbili, tunalisaidia Taifa hapa. *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Omar Issa Kombo.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni wakati wangu sasa, anatumia muda wangu Mheshimiwa Esther. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Omar Issa Kombo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Alice Kaijage.

**MHE. OMAR ISSA KOMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuchangia hotuba hii ya Ofisi ya Rais. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia mpaka muda huu nikiwa bado nina neema yake ya uhai na afya njema. Vilevile nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri na timu yao yote Wizarani kwa kuandaa hotuba nzuri kabisa na kuiwasilisha kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wetu, Mama yetu Jemadari Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ya maendeleo anayoendelea kuifanya katika Taifa letu. Mama ameonesha uwezo mkubwa sana na kwa kweli anastahili pongezi. Tunapompongeza, hatumpongezi kwa bahati mbaya, ni kwa mazuri na makubwa tunayoyaona katika nchi yetu ambayo anaendelea kuyatekeleza mama huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia hotuba hii kwenye taasisi ya *TASAF*. Nitagusia kidogo tu. Naipongeza Serikali kwa kuendelea kuutekeleza mradi huu kwenye jamii yetu. Nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kukubali kuendeleza mradi huu. Tunafahamu kwamba mradi huu umeanza awamu kwa awamu, ulianza na Mheshimiwa Hayati Benjamin Mkapa, wakaja viongozi wengine wakauendeleza. Sasa kitendo cha Mheshimiwa Rais Samia kukubali kuuendeleza mradi huu, kwa kweli, anastahili pongezi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, naipongeza *TASAF,* imekuwa ikifanya kazi nzuri sana. Pia kuna maeneo naomba niishauri Serikali ili iangalie katika *program* hii ya *TASAF*. Kwa mfano, kwenye vigezo vya kuwatambua wanufaika;

malalamiko yamekuwa mengi kwa wananchi wetu kwamba, kuna baadhi ya wananchi wana sifa za kuingia kwenye mpango huu, lakini kwa kweli bado wanaendelea kuachwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iangalie vigezo. Kwa mfano, tunapoangalia kigezo cha umasikini, tukiangalia kwamba mtu akipata nyumba tayari eti anaonekana kwamba, sio masikini. Tuangalie hiyo nyumba ameipataje? Kuna mazingira tofauti ya kuipata nyumba. Wakati mwingine mtu anajengewa na wahisani. Hatuwezi kusema kwamba huyu siyo masikini tena. Au wakati mwingine familia ilikuwa na baba, baba amefariki, anapofariki familia hii inarudi katika ukwasi wa maisha. Kwa hiyo, kigezo cha nyumba hakiwezi kutumika kama ni kigezo cha mtu kutoingizwa kwenye Mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, tuangalie vilevile ruzuku inayotolewa. Naipongeza *TASAF* imeandaa program za kutoa ajira za muda. Lengo la ajira hizi ni kuwawezesha wananchi kujimudu katika vile vipindi vigumu. Pia tuangalie: Je, unapokwenda kumlipa mtu Shilingi 3,000/= kwa siku, hivi jamani kweli! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, azma ya Serikali ni njema na malengo ni mema, lakini kulingana na kupanda kwa gharama za tuangalie namna ya kuboresha. Shilingi 3,000 sasa hivi kumpa mtu kwa kweli haiwezi kwenda kumsaidia kama vile ambavyo Mheshimiwa Rais amekusudia kuwasaidia wananchi wake. Kwa hiyo, tuangalie ikiwezekana tuongeze angalau iwe shilingi 5,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile muda wanaoutumia katika hizi ajira za muda. Wanakwenda wanufaika wanaanza saa 01:00 mpaka saa 09:00, analipwa shilingi 3,000, kulingana na ukubwa wa kazi na muda anaoutumia. Muda huo anaoutumia ina maana tayari hapa hatumsaidii. Ni vema

tukaweka muda mchache ili aweze kufanya kazi nyingine za kumwingizia kipato. Nadhani hii itakuwa ni njia sahihi ya kuweza kumsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile miradi ambayo tutakwenda kuifanyia kazi, tuwachagulie zile kazi nyepesi. Kama tunavyofahamu kwamba, wanufaika wengi wa *TASAF* hali zao ni duni, wengi wao ni akina mama. Kwa mfano, katika jimbo langu tunakwenda kutekeleza mradi huu wa ajira za muda kwenye masuala ya zege. Mama unambebesha saruji, wengine wanaangukanayo, ni jambo ambalo kwa kweli Mheshimiwa Waziri, ni lazima tuliangalie kwa kina. Ni vyema tukawatafutia zile kazi nyepesi ambazo wanazimudu, lakini vilevile muda wanaoutumia uwe mchache ili waweze kwenda kufanya shughuli nyingine za kujiingizia kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kikwazo kingine ni suala la vitambulisho vya *NIDA*. Mara nyingi Wabunge tumekuwa tukipiga kelele kuhusu tatizo la vitambulisho vya *NIDA*. Tokea Wizara hii iko kwenye Kamati ya USEMI tumekuwa tukishauri mara kwa mara kwamba, Wizara ikutane na Wizara ya Mambo ya Ndani, wakae kwa pamoja waangalie namna ya kutatua au kama haiwezekani basi, kigezo cha kitambulisho cha *NIDA* kiondolewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao Wenyeviti wa Serikali za Mitaa na Masheha, akishathibitishwa na Sheha basi aweze kuingizwa kwenye Mpango, lakini suala la kuweka kitambulisho cha *NIDA* kama ni kigezo, na huku tayari kuna vikwazo vya kupata hicho kitambulisho cha *NIDA,* hapa itakuwa hatuwatendei haki wananchi. Naomba sana Mheshimiwa Waziri akutane na Wizara inayohusika ili tuangalie namna ya kutatua changamoto hii ya vitambulisho vya *NIDA* ili wananchi waweze kupata haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwa haraka kulingana na muda, nije kwenye *program* ya kuendeleza miundombinu ya miradi ya kijamii. Tumeelezwa hapa kwamba kuna miradi 550 tayari iko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji. Naomba kuwe na utaratibu mzuri wa kugawanya miradi hii, kwa sababu kuna baadhi ya Shehia, mfano kwenye jimbo langu Shehia ya Mjini Wingwi, Mapofu, wamepeleka barua za maombi ya miradi kama hii, lakini hadi leo ukiangalia, miradi inapelekwa sehemu moja au sehemu chache, wakati wananchi wanaohitaji miradi hii ni wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili mkalifanyie kazi. Kwa zile Shehia ambazo tayari wameshapeleka barua zao za maombi basi na huko kuangaliwe namna ya kufanyiwa kazi. Wananchi wote tunahitaji hizi huduma, keki hii ya Taifa tuweze kuifaidi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine, nije kwenye upelekaji kwenye rufaa. Tumeelezwa kwamba, bado kuna malalamiko ya rufaa yanaendelea kufanyiwa kazi na ni muda sasa. Kwenye majimbo yetu wananchi wanakuwa wakitulalamikia kwamba rufaa imekuwa ni muda mrefu, watu wanatolewa bila utaratibu. Hebu niombe hizi rufaa ziende kwa haraka ili kama anastahili kuingizwa kwenye mpango aendelezwe kwenye mpango.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kusikitisha zaidi ni kwamba kuna wananchi tayari wameshafanya kazi karibu miezi miwili, lakini wanafikia mahali wanaondolewa kwenye mpango na kile walichofanyia kazi bado hawajalipwa. Niiombe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi iende ikafanyie kazi hizi rufaa. Hawa wananchi kama wanastahili kupata hizi haki waendelee kuzipata, lakini kama hawastahili vilevile kuandaliwe utaratibu mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la vikundi, kutolewa elimu kwa wanufaika. Tumeambiwa kuna vikundi kadhaa vimeundwa, lakini ukifuatilia kwa kweli bado wananchi hawa elimu ya kuibua miradi ni ndogo. Tutumie maafisa wetu wa huduma za jamii, lakini vilevile tutumie wataalam wetu ili waweze kuwasaidia wanufaika hawa waweze kuibua miradi kulingana na mazingira wanayoishi ili mradi huu wa *TASAF* uweze kukidhi yale malengo ambayo Mheshimiwa Rais ameyakusudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo machache, nishukuru sana, naunga mkono hotuba hii. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Alice Karungi Kaijage, jiandae Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Mwenyezi Mungu. Pia, naendelea kuipongeza Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kujali huu utumishi wa Umma, maana mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Tumeona jinsi ambavyo Serikali imeendelea – japo kuwa ana keki ndogo – lakini imeendelea kujali utumishi wa Umma ukilinganisha na ambavyo ilikuwa hapo nyuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mawaziri wetu, Mheshimiwa Simbachawene, pamoja na Mheshimiwa Ridhiwani. Nampongeza pia Mheshimiwa Jenista Mhagama, wakati tunajadili bajeti yetu hiii tulishirikiana naye vizuri kwa sababu wakati huo yeye ndio alikuwa Waziri wa Wizara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii Wizara imeendelea kufanya kazi zake ambazo ni za msingi kwa maana ya kusimamia utumishi wa Umma, utendaji kazi bora, pia kuhakikisha stahiki za wafanyakazi zinasimamiwa sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hii ni Wizara ambayo ina-*deal* na rasilimali watu, rasilimali watu ukiisimamia vizuri ndiyo inaweza kusimamia rasilimali nyingine; rasilimali ardhi, madini, maji n.k. Na haya malalamiko yote ambayo tunayaona, kama kuna usimamizi mzuri wa rasilimali watu hatutakuja kuyaona. Ubadhirifu hatutakuja kuuona. Kwa hiyo, ni muhimu sana kusimamia rasilimali watu, kwa hiyo Wizara hii inafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini nasema hivyo; nikienda kwenye Fungu 32. Fungu hili limekuja na mifumo mingi, mifumo hii ndiyo kwanza inaanza, kuna mfumo ambao tunauita wa Utendaji Kazi katika Utumishi wa Umma. Mfumo huu ni kama ule ambao ulikuwa *OPRAS* siku za nyuma. Ule ulikuwa unaamua, mnakaa watumishi mnajikusanya mnajijazia. Na mwajiri anakuwa anakutazama unafananaje anakujazia. Lakini sasa hivi kuna mfumo huu umekuja unasimamia utendaji kazi wa utumishi wa Umma na mwingine unasimamia utendaji kazi wa taasisi za Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu mpaka sasa hivi umefanya majaribio kwenye taasisi 11 za Umma na umefanya kazi nzuri sana. Na sasa hivi mfumo huu utakuwa unaangalia ubora na wingi *(workload)*. Kwa hiyo, *automatically* inakwenda kwenye mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa wakati unamjazia mtumishi utapunguza upendeleo na unyanyasaji, *whether* unampenda au humpendi lakini zile *grades* zimekuja kwenye mfumo. Kwa hiyo, hii itatoa moyo kwa watumishi sasa hivi, watakuwa na ari. Kwa hiyo, itakuwa na usimamizi mzuri na

wafanyakazi watafanya kazi kwa moyo na hakutakuwa na uonevu kama ambavyo nimesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri mifumo hii ndiyo kwanza inaanza, ina nia njema, naomba mamlaka mtandao iongezewe bajeti kuwe na fedha za kutosha kuhakikisha usimamizi wa mfumo huu. Ni mwema, lakini kama hautasimamiwa vizuri, hautakuwa na ulinzi, ina maana ile tija haitaonekana; ndiyo ushauri wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mfumo mwingine unaitwa wa Taarifa za Utumishi na Mishahara. Mfumo huu ni mzuri sana kwa sababu tunakumbuka zamani, mchakato wa mshahara ulikuwa unachukua hata siku 14, lakini sasa hivi mchakato wa mshahara siku moja tu umesambaa kote, umefika kwa siku moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, unaweza kuona mifumo hii ina nia njema ya kuboresha maslahi ya watumishi ili wafanye kazi kwa bidi ili kulinda utumishi katika sehemu nyingine mbalimbali, kutoa tija. Ukimpa mtumishi mshahara wake kwa wakati unamtia morali, unamtia moyo, anafanya kazi kwa ufanisi. Kwa hiyo, mifumo hii tusiidharau. Nimeijadili kwa sababu imeanza kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mfumo mpaka sasa hivi umeshaunganishwa kwenye taasisi 433 kati ya taasisi 522 tulizonazo kwenye utumishi wa Umma. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi ambavyo Serikali inakazana. Nashauri kwamba mifumo hii isimamiwe kwa udhibiti mkubwa sana na pesa ziongezwe, iimarishwe, isambazwe kote. Huu mfumo pia, kwa mfano…

**TAARIFA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Taarifa.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa anayechangia. Hapo awali tulishauri Bunge hili kwa habari ya kuondokana na Mfumo wa *OPRAS,* na Serikali sikivu ya Awamu ya Sita ilisikia, ikaenda kwenye mifumo hii mipya, *PEPMIS* na *iLMIS* ambayo kimsingi imeanza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kumuunga mkono mzungumzaji, anazungumza jambo jema sana kwa Taifa letu. Ninashauri ni muhimu sasa Wizara ya Utumishi ianzishe kitengo maalum kitakachoratibu uendeshaji wa mifumo hii nchi nzima. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kaijage, taarifa.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naipokea taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kueleza jinsi ambavyo Mfumo huu wa Taarifa za Utumishi na Mishahara unavyofanya kazi vizuri. Sasa hivi ulivyoanza kufanya kazi kwenye taasisi hizi ambazo zimeshaunganishwa ukifika umri wako wa kustaafu *automatically* mfumo huu unatoa jina lako kwenye mshahara, unalihamishia kwenye mifuko ya pensheni. Kwa hiyo, itapunguza zile taratibu za mtu kuendelea kulipwa mshahara wakati alishatoka kwenye umri wa kustahili mshahara, na itapunguza udanganyaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo huu umeunganishwa na taasisi mbalimbali; *NIDA, RITA* na mifuko mingine ya hifadhi ya jamii. Kwa hiyo, umeanza sasa hivi, tutaona baadaye *effect* yake. Sasa hivi ukifika muda wako wa kustaafu, umri wa kustaafu, kwa sababu *RITA* imeunganishwa na mfumo huu, *automatically* jina lako linahama, hupati tena mshahara, linahamia kwenye pensheni kwa hiyo, nipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuomba kwamba mifumo hii iwezeshwe ili iweze kufanya kazi kwa tija na izalishe vizuri na watu waweze kuona umuhimu wake na hivyo, watumishi wakifanya kazi wawe wanajua kwamba mwisho wa siku watakuwa na utulivu na watakuwa hawana wasiwasi juu ya mafao yao na stahiki zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Mfumo mwingine unaoitwa wa Tathmini ya Mahitaji ya Watumishi wa Umma. Sasa huu ni mfumo muhimu sana kwa sababu ndiyo ambao utakuwa unaonesha watumishi wako wangapi, wako sehemu gani, kuna upungufu wa watumishi kiasi gani, kuna wingi wa watumishi kiasi gani. Kwa hiyo, utakuwa unarahisisha Serikali kufahamu kwamba yamkini vituo viko sawa, vina *level* sawa, kwa mfano labda vya hospitali, kituo fulani kinahitaji watumishi 500, kingine watumishi 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ukija kuangalia kwenye *workload* na idadi ya mtu ambaye ameona mgonjwa unagundua kwamba katika kituo fulani, japo kinafanana na kingine, lakini wana madaktari 50, wengine wana 100 lakini hawa wana wagonjwa wachache, kwa hiyo, kutakuwa kuna urahisi wa kuhamisha watumishi kutoka sehemu fulani kwenda sehemu nyingine kulingana na jinsi ambavyo mfumo unaonesha idadi, uwezo na ubora na *workload* anayotumia yule mtu kutibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mfumo huu utapunguza malalamiko mengi ambayo Wabunge wengi wamechangia. Unakuta sehemu fulani kuna watumishi wengi, sehemu nyingine kuna watumishi wachache lakini vituo vinafanana. Lakini ukiangalia katika uhaliasia *workload* aliyonayo mtumishi mmoja na yule mwingine ni tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mfumo huu ni mzuri sana, utabaini idadi ya uhalisia wa uhitaji wa wafanyakazi, utakuwa bayana. Nimeona niseme hivi vitu;

nimeshazungumzia mambo mengi kuhusu wafanyakazi na kuwatetea, lakini naomba niwaoneshe, kwa sababu niko kwenye Kamati hii, mambo yanayokuja mbeleni yatakuwa mazuri. Ila tunachokiomba; Serikali iongeze bajeti ya *e-Government* ili mifumo hii isimamiwe vizuri iweze kuwa na tija baadaye. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, ni kengele ya pili.

**MHE. DKT. ALICE K. KAIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika bajeti hii ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa niwapongeze Mheshimiwa Waziri na msaidizi wake kwa hotuba nzuri waliyoitoa. Lakini pia nimpongeze mtangulizi wake aliyekuwepo, Mheshimiwa Jenista, kwa kuyachukua mengi tuliyoyachangia katika Bunge la Bajeti lililopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yako baadhi ambayo hayajafanyiwa kazi. Sasa nilitaka kipindi tunaendelea kwanza nipongeze nafasi nyingi sana za ajira ambazo zimetoka, hasa hizi nafasi 21,200. Tumpongeze Mheshimiwa Rais kwa nafasi hizo, walau zinapunguza joto ingawa joto bado ni kubwa, lakini *at least* zinapunguza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati nachangia bajeti hii ya Utumishi *specifically* niliongelea

jambo moja linalohusu watoto waliomaliza katika vyuo vya maliasili lakini wakanyimwa ajira kwa sababu umri wao umevuka miaka 25. Nililisema hapa na ninaomba nilirudie kwa sababu ni kama halikufanyiwa kazi na bado halijafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati tunapewa majibu humu ndani tuliambiwa sheria za Jeshi haziruhusu kuajiri mtu aliyevuka miaka 25. Nikasema sawa. Lakini vijana hawa wengi ambao tunasema wametoka kwenye vyuo vyao wamekuwa *trained* Kijeshi na tayari wanavyo vyeti. Sasa unaposema huwezi kumuajiri wakati ana cheti na umem-*train* Kijeshi na yuko mtaani, sidhani kama ni *fair. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe, kwa sababu vyuo hivi ni vya Serikali, wazazi wamelipia kuwapeleka watoto wao wakaenda kusoma pale, tunaomba Serikali itumie busara ione vijana hawa ambao hawakuajiriwa kati ya 2015 mpaka 2022 waone jinsi ya kusaidiwa ili na wao jasho lao walilolitoa kujifunza mafunzo haya ya Kijeshi waone kwamba kuna sehemu wanakwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuendelea kuwaacha mtaani ni kuwaonea. Maana mtu amesomeshwa na mzazi kwa ada ya milioni nne mpaka nane, leo anamaliza pale unamwacha mtaani unamwambia umri umevuka, na hakukataa kujiajiri, ni kwa sababu hatukuwa na nafasi za kuwaajiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini huku tunapotoka kila siku tunalalamika tembo wanatoka wanajeruhi wananchi, wanafanya nini. Hawa vijana wako mtaani, tuone jinsi ya kuwachukua kwa sababu bado nafasi za kuwaajiri zipo; hilo ndiyo ninaomba. Mlichukue hivyo, Serikali ilione ili iweze kutusaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu wa mwaka jana niliongelea pia habari ya nafasi zinazotoka kwa kigezo cha JKT. Wote ni mashahidi; kambi zetu tulizonazo za ku-*hold* watoto katika JKT hazitoshi wala haziwezi kuenea watoto wote walio mtaani. Lakini inashangaza kwamba nafasi bado zinatoka kwa kigezo cha kwamba mtu awe amepita JKT. Na humu ndani tulisema na Serikali ikasema imesikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao mfano; nafasi za Uhamiaji zilizotoka ilikuwa ni miaka 18 mpaka 25 kigezo cha kwanza, kinachofuata, awe amehitimu JKT. Lakini ni vijana wangapi wamekuwa *denied* nafasi ya kwenda JKT? Unamnyima kwenda JKT, wakati wa kutafuta ajira umetangaza ajira unamwambia awe ametoka JKT. Inaumiza kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili naomba niliseme kwa niaba ya vijana walioko mtaani. Tumeona habari za Uhamiaji, tumeona nafasi za Magereza. Leo nilikuwa nasoma kwenye *website* ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania, Jeshi ambalo tunasema kwamba labda ndiyo *basic;* hakuna hiyo *condition* ya kwamba mtu awe ametoka JKT. Wameandika tu miaka 18 mpaka 25, awe Mtanzania aliyemaliza kidato cha nne, wao hawaweki kigezo cha JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaomba haya Majeshi mengine ambayo yanafuata hapa wajaribu kuona, mpe nafasi huyu Mtanzania aje kwenye *interview*. Kama anafeli afeli kwa kigezo hicho cha kufeli baadaye mrudishe nyumbani, kuliko kum-*deny* kabisa hata nafasi ya kufanya *interview*. Watoto hawa wanaonewa, naomba hilo liangaliwe ili tuweze kuwasaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine ambalo nataka niliongelee. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, jana ametutolea ufafanuzi mzuri sana

hapa kuhusu hizi ajira, maana simu zimeelemewa huku; meseji ni nyingi, watu bado wanaendelea kutuma, pamoja na ufafanuzi wako wa jana meseji zinaendelea; wazazi, watoto na kila mmoja anaendelea kutuma. Lakini ninaomba nitoe *suggestion* moja; kuna mtu aliyeongea jana hapa kuhusu *allocation* ya hizi nafasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndugu zangu, wote hapa tulikwenda kuomba kura kwa wananchi. Wakati tunaomba kura kwa wananchi tuliinadi Ilani ya CCM. Ilani ya CCM imeweka *specific* kabisa kwamba tunataka kutengeneza ajira milioni nane. Ni aibu kwa Mbunge ninayesimama hapa leo, sijui hata watu ambao katika hizo nafasi 21,000 zilizotoka, leo hata jimboni kwangu naulizwa wametoka watu wangapi, sijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wewe ni Mbunge mwenzetu, unawawakilisha wananchi, na humu ndani hakuna mtu anayegombea kwamba hizi nafasi anazipeleka kwenye familia yake. Lakini tunachoomba ni kwamba pale tunaposhauri mawazo yetu ni mawazo ya wananchi, tunawasikiliza wananchi huko mtaani wanavyosema. Wanatoa mawazo kwamba kwa nini hata hizi nafasi zisigawanywe kwa kila jimbo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kama mnatugawia pesa sawa ya miradi ya barabara, mnatugawia pesa sawa miradi ya maji, mbona kwenye ajira kunakuwa na kigugumizi? Tukigusia tu ajira mnaanza kusema ubaguzi. Tunachotaka ni kwamba nafasi zimetoka 21,200, hatutaki kumpangia Waziri nafasi zile amuweke nani au afanye nini, tunachotaka iwekwe *equality. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimepiga hesabu, nafasi 21,200, ukigawanya kwa halmashauri 184 za nchi hii wote wako sawa, kila halmashauri iko sawa, hakuna halmashauri

kubwa wala ndogo hapa. Nawawakilisha wananchi na Wabunge wenzangu wanawakilisha wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukigawanya maana yake kila halmashauri itapewa nafasi 115 katika ajira hizi. Twende kwenye ile *system* yetu, *system* si unai-*feed* tu? Iwe ni *system* ya *JAVA* au kama ni *C++ programming,* unai-*feed information,* ielekeze, kwamba *choose* watu 140 kutoka wilaya hii itakupa, *choose* watu 140 kutoka wilaya nyingine watakuwepo pale, mkabidhi Waziri wa TAMISEMI mwambie watu wako 21,200 hawa hapa. Yeye awapange anavyotaka, lakini ajira hizi zisambae nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haiwezekani sisi tunakaa hapa tunawawakilisha wananchi unatoka hapa wananchi kila mtu anatuma meseji, wewe unakuwa unamwambia mfumo. Wakati unaomba kura ulimwambia tutawasaidia kupata ajira, tutaleta maendeleo, leo unamwambia mfumo. Hiyo haikubaliki, tusaidiane. Najua bado *deadline* haijafika, mnaweza kwenda kwenye mfumo – Utumishi mko hapa – tukakubaliana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri zaidi tunaye Mheshimiwa Bashe ni mfano tosha hapa kwenye Mradi wa *BBT*. Waliomba nchi nzima lakini kila wilaya imepata, tumeona, na yakatoka matangazo. Hakuna malalamiko tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wanaouliza tunawaambia kwamba nafasi ya pili ya *BBT* inakuja, subiri. Iko wazi inaonekana. Ajira hazipo lakini zikitoka chache tukawaambia wilayani kwetu tumepata ajira 50, subirini raundi ijayo, wananchi wanaelewa na wanaelewa hali ilivyo. Kuliko unakwenda sehemu mtu anakuuliza huna hata jibu la kumpa. Ninaomba hilo tulizingatie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuna kitu nimekuwa najiuliza. Ajira tunazoziona hapa; ualimu, huduma ya afya, hivi ajira za *TRA* huwa mnazitangazia wapi; ajira za *BoT* mnazitangazia wapi? *We want to see them.* Ajira za *TANESCO* mnazitangazia wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka hata zile ajira kubwa tuone watoto wa maskini wakienda huko kwa sababu wamesoma. Kelele zilizoko huko ni kwamba wanahisi zile ajira ni za watoto wa viongozi, siyo za kwao. Tuone zikitangazwa wazi, huo mfumo uwekwe kwa uwazi kama ni kugawanya tugawanye *equally,* nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatutaki tuone watu wa *TRA* ukienda unakuta watu wa kabila fulani tu na watu wa eneo fulani. Tunataka uende ukute Muha, Mhaya, Mchagga, ukute nchi nzima tumeenea kule, *that is what we want*. Kwa sababu hii ni keki ya Taifa, tuigawane *equally* ili kila mmoja aweze kupata haki ya kutumika katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa kumalizia, ninachoomba, taasisi hii ya Sekretarieti ya Ajira, tulikuwa tunaomba kama inawezekana ajira zote zipitie huko, tui-*empower* hii Sekretarieti ya Ajira. Kwa sababu ndiyo usalama wa Taifa letu wenyewe ulipo, tuwaajiri watu tunaowajua watachujwa kwa vigezo wataonekana kwa *merits* na *qualifications* zao ili iweze kutusaidia hata kuulinda usalama wa nchi hii. Siyo sasa kila taasisi inaachiwa inaajiri yenyewe tukitoka hapo baadaye tunakuja tunataja mfumo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo, nishukuru sana kwa nafasi. Lakini pia tuzidi kuangalia, tuzidi kumuomba Mheshimiwa Rais atusaidie ajira nyingine ziweze kuongezeka kwa sababu kweli kiuhalisia madarasa ni mengi, vituo vya afya ni vingi, watumishi wanahitajika na bado wengi wako mtaani.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza, nashukuru sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru kwa michango. Niendelee kuwakumbusha nidhamu kwenye Bunge. Hakuna Mbunge anayekatazwa kuchangia wazo lake na ushauri anaotaka kuutoa ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Esther Matiko amechangia na Serikali imejibu. Ni wajibu wa Serikali kujibu, ni wajibu wa Serikali kumwambia mambo inayofanya. Unapochangia kwa njia za kejeli za kuonesha kuna mapungufu hakuna yanayofanywa, hayo yanasababisha Serikali isimame na itoe miongozo na taarifa. *(Makofi)*

Kwa sababu mnapeleka *wrong signals* kwa watu kuwa hakuna kinachofanywa wakati mambo yanafanywa na yanaonekana kwenye majimbo yenu na kwenye maeneo yenu. *(Makofi)*

Shule hizi za kata sasa hivi ndizo zinapasisha watoto kwa kiwango kikubwa sana; kwa hiyo, tunaipongeza sana Serikali, kwa hayo madogo yaliyopo kimafanikio yanapatikana. *(Makofi)*

Hatuwezi kujifananisha sisi na Marekani au Uingereza. Huko wanazo changamoto zao vilevile. Lakini unapoanza mzozo wa kutaka kufanya mnayochangia ninyi mnajua zaidi mnafanya kosa la kinidhamu ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Hapa msione nimesimama mkasema wewe Zungu mtu wetu, hapana, mimi siyo Zungu nikisimama hapa, nikikaa hapa ni mamlaka. Mnaiona siwa hiyo, ndiyo mamlaka yaliyopo hapa, nikishashuka hapa sina mamlaka. Kwa hiyo nitoe tahadhari. *(Makofi)*

Mbunge kubishana na Kiti kwa mujibu wa Kanuni ya 84 ni kosa kubwa sana na Mbunge kujifanya wewe mjanja wa maneno au kuonesha Bunge kuwa una mdomo, utaumia. Kwa hiyo, nimekusamehe kwa sababu ya Mwezi wa Ramadhani tu. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, jioni tutakuwa na Mheshimiwa Issa Mtemvu, Mheshimiwa Michael Kembaki, Mheshimiwa Yustina Rahhi na Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga.

Nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa Kumi jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. David M. Kihenzile) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Katibu.

**NDG. PILI OMARI – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na uchangiaji, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Wachangiaji watakao anza ni kama ifuatavyo: -

Tutaanza na Mheshimiwa Issa Mtemvu akifuatiwa na Mheshimiwa Michael Kembaki wakati huo Mheshimiwa Yustina Rahhi anajiandaa.

**MHE. ISSA J. MTEMVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kwa mchana huu nianze kuchangia kwenye Wizara hii, Fungu 67; lakini kabla nitoe pongezi sana kwa hotuba nzuri iliyowasilishwa na kaka yangu Simbachawene. Najua ni kwa msaada mzuri wa mdogo wangu Ridhiwani Kikwete, na ninatambua bila shaka watendaji kwenye Wizara hii ya Ofisi ya Rais Utumishi wako vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika zangu najua ni kumi nimeziweka hapa ili yale ambayo ninayoweza kujaliwa kuyatimiza. Kabla, hii dakika moja lazima niseme vizuri juu ya kazi kubwa ambayo inafanywa na Mheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Sita Dkt. Samia Suluhu Hassan. Kila mmoja anayesimama hapa anajaribu kueleza ni jinsi gani Mheshimiwa Rais anafanya kazi, hatuwezi kumaliza kwa dakika moja. Nakumbuka, na ninawasilisha leo; wananchi wangu wa Jimbo la Kibamba, yupo mzee mmoja mstaafu wiki moja iliyopita aliniandikia barua, akaniambia naomba peleka wazo langu Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mama anafanya kazi kubwa, ndiye Rais wetu wa kwanza mwanamke, kwa nini tusifikie sarafu yetu ya nchi ikabeba sura ya Mama Samia Suluhu Hassan? Najua tuliwekeana utaratibu na marais wetu huyu ni wa sita, marais wawili tu ndio wanaoonekana, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Rais wa Awamu ya Pili Ali Hassan Mwinyi. Tufikie maamuzi Rais wetu wa kwanza mwanamke kwenye Jamhuri ya Muungano wa Tanzania naye aingie kwenye sarafu ya fedha zetu, haya si maneno yangu ni maneno ya wananchi wangu toka jimbo la Kibamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitachangia maeneo mawili mpaka matatu muda ukiniruhusu kwa haraka. Eneo la kwanza ni eneo ambalo linahusu utumishi kwa ujumla wake lakini katika idara nataka nizungumze kidogo idara ya uhasibu pamoja na fedha. Kumekuwa na changamoto sana, na nimewahi kuuliza swali la msingi hapa kama mwaka na nusu uliopita juu ya idara hii. Inaonekana idara ya fedha na uhasibu ndicho kiini cha hati safi na hati chafu. Wakuu wa ofisi, kwa maana ya *accounting officers* wanapopata hati safi wanasifiwa lakini inapopatikana chafu hawa ndio wanaoshikwa; hawa wahasibu na wakaguzi wa fedha walioandaa hesabu, lakini kuna jambo huku ambalo ndilo linasababisha ambalo leo likieleweka tena inawezekana ikalisaidia Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idara hii mara nyingi katika sekritarieti za mikoa na wizara zetu na hizi tunaita idara zinazojitegemea, zote hizi zina wahasibu wakuu; lakini pia kuna vitengo. Sasa wakuu wa vitengo wana changamoto sana. Kwanza wanakuwa hawawi *involved* vizuri kwenye menejimenti, hilo la kwanza; lakini la pili hawa wote wanakuwa ni ma *chief accountants*. Ukiwa na tofauti na wakuu wa idara, kwa mfano idara ya rasilimali watu, tuna wakurugenzi wa utawala na rasilimali watu lakini ziada wana wasaidizi, mkurugenzi utawala, mkurugenzi rasilimali watu, wamegawanyika wawili, wasaidizi hao, lakini unaenda mipango, Mkurugenzi wa Mipango ana wasaidizi, mkurugenzi upande fulani, mkurugenzi upande fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapokwenda kwa uhasibu unakuta mhasibu mkuu peke yake; anahangaika na mambo ya malipo, kama *payment* anahangaika na mambo ya *revenue* kama mapato, ni jambo gumu na kubwa sana. Mkumbuke tulikotoka tulikuwa tunatumia *manual* hata kwenye kufunga hesabu, lakini leo unapofunga hesabu Tanzania ndivyo wanavyofunga hesabu Marekani na Uingereza, kwa *standard* moja. Sasa kwa nini tunaona kazi

zao hizi ni ndogo? Kwa hiyo ni vizuri tupandishe hadhi kwenye hizi ziwe idara, muwape wawe wakurugenzi wa fedha na utawala lakini pia wawe na wakurugenzi wasaidizi upande wa fedha na upande wa utawala. Kwa kufanya hivyo tutapunguza sana na kwa kiwango kikubwa hoja za ukaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani mhasibu mkuu yupo peke yake na anafanya kazi peke yake, niliona hilo niliweke hivyo. Na, hata kama hatutaki kwenda kuibadilisha kuwa idara basi mhasibu mkuu kimuundo awe na wasaidiizi. Kuwe na mhasibu mkuu msaidizi kimuundo kwenye upande mmoja wa mapato na upande mmoja wa matumizi. Ikiwa hivyo tutasaidiwa sana kwenye kufunga hesabu vizuri na kuondoa hoja ya ukaguzi. Niliona hilo niliweke katika sura hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kuhusu ajira *portal,* limesemwa na wengine. Mimi mwanzo nilikuwa na mawazo, tuliko toka zamani ilikuwa kila taasisi *accounting officer* anaweza kuajiri lakini tukaja kwenye huu mfumo mzuri tukajua utatusaidia. Hata hivyo nje kuna manung'uniko mengi sana juu ya jambo ambalo mimi nilijua *garbage inn garbage out;* kwamba tunachokiingiza *process* mle iwe ni *fair* na nje pia tutakutana na jambo zuri, lakini leo mambo ya hovyo tu bado yanatokea kaka yangu Simbachawene. Tunaitegemea ajira *portal* lakini ukiichungulia, amesema Engineer Chiwelesa, unaona kabila limesimama pale, unaliona kabisa. Si hivyo tu unaona ukanda, na inatokea kwenye ajira portal tunayoiamini lakini ziada inatokea sura za viongozi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unamwona Mheshimiwa Simbachawene moja kwa moja kwenye matokeo ya wale wanaoajiriwa, unamwona Mheshimiwa Kikwete moja kwa moja, natolea mifano tu. Hii haiwezi kusaidia. Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na wakurugenzi ndio sura ya ajira inayotembea. Mimi sitaki tuondoke kwenye ajira *portal bali* tui-*strengthen.* Waheshimiwa Wabunge wengi wametoa

ushauri, na mimi ni mmoja wapo, kwamba ikibidi twende kwenye majimbo ili mimi wale wanaonitumia *message* na kadhalika niwaone. Hata kama wataenda kufanya kazi Mbeya, Sumbawanga lakini hawa wanatokea Wilaya ya Ubungo, hiyo itatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kwa haraka. Nimeona hapa, liko jambo la idara ya kumbukumbu na nyaraka za Taifa, nimesoma nikafurahi sana. Humu ndani wenzetu wanatuambia ni kama mradi na fedha walizozipata wamejaribu kutafuta nyaraka kwa kuhoji familia na watu, walimu, waasisi wetu, wanatamkwa waasisi wawili humu. Anatamkwa mhasisi wetu Karume kwa upande wa Zanzibar na Mwalimu Julius Kambarage Nyerere kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa ujumla ndio waasisi wetu. Lakini changamoto ya humu maandishi yanaonesha historia zao zimetafutwa hata kabla ya uhuru tangu wanasoma na Sekondari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vizazi vya mwisho vya kujua historia ya nchi yetu ni sisi. Tukiondoka sisi wajukuu na watoto wetu hawatajua tena kwenye hili, na ndiyo maana wanaenda kwa kuchoka, watajua watu wawili lakini sio kweli. Uhuru wanchi hii umepatikana na wazee wetu tunawajua. Nakutajia na majukumu yao, Kasela Bantu hakuna mtu asiye mjua. Huyu ndiye mwaka 1954 aliyeshawishi kikao cha *TANU* kifanyike ili kuanzishwa kutoka *Tanganyika African Association TAA*, iliyoanzishwa 1929-1954. Kuna Abulwahid Sykes tangu mwaka 1929 alikuwa na *TAA* hadi 1954. Yeye ndiye aliachia kiti akamwachia Mwalimu Julius Nyerere tangu *TAA* kuanzishwa hadi *TANU*. Kuna Alhaj Zuberi Mwinshehe Manga Mtemvu katibu Mkuu wa Kwanza wa *TANU,* kwa nini tunaacha haya? Vilevile kuna mzee Dothan Azizi, Waheshimiwa Wabunge lazima niwaambie, huyu ndiye aliyetoa *land rover* yake ikatembea kwa ajili ya kutafuta kura za *TANU*. Si hivyo tu, pia kuna akina Mzee Rupia, Bibi Titi Mohammed; na juzi nilimfurahia sana Mheshimiwa

Mchengerwa, na akina mama mmeanza kukubali na kukumbuka kwamba huyu ndiye mama wa Taifa sasa, lakini walisahaulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo naomba Mheshimiwa Waziri ukija utuambie, hizi nyaraka zenu juu ya wengine wote ambao walisababisha hao wakafahamika. Mimi nataka niwaambie tu wala si *success story* kama ndugu yangu *Chief* Kunambi anavyosema, lakini nikikumbuka sana, Mwalimu Nyerere anatoka Pugu alikaa pale mnaita Aggrey kwenye nyumba ya Mwinshehe Manga Mtemvu, babu huyo, akiwa anakunywa kahawa na kadhalika, kwenda Kariakoo Shimoni. Hii nchi lazima watu hawa wafahamike na kutambulika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti,lakini mwisho sana kwa umuhimu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Watumishi mmewafurahisha, mmeanzisha *PEPMIS* na *PIPMIS,* mifumo miwili; ya watumishi na ya *public institutions* itawasaidia sasa hivi kuna hali mbaya sana. Mimi huwa sipendi kuongelea kwingine kwenye nchi hii. Wilaya ya Ubungo tunayotokea leo kunawazuia sana watumishi ndiyo maana mmeziona *issue* za mkaguzi wa nje, mambo ya hovyo sana; lakini maana yake kuna watu wameishi mle muda mrefu. Nendeni mkaangalie muone walio *overstay* muwatoe, si lazima niwataje majina kama Wabunge wengine wanavyofanya hapa, sihitaji kutaja jina la mtu mle ndani kwenye taasisi mimi ninayoiongoza, Halmashauri ya Wilaya ya Ubungo. Nendeni mkaone shida iko wapi ili muweze kutusafishia mazingira hayo Mheshimiwa Simbachawene.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi naunga mkono hoja iliyopo mezani, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Issa Mtemvu kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Michael Mwita

Kembaki wakati huo Mheshimiwa Yustina Arcadius Rahhi anajiandaa.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nipende kutoa pongezi kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya ya kuongoza Wizara hii muhimu katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa niseme kidogo kuhusiana na kazi kubwa ambayo inafanywa na viongozi wetu wa kitaifa. Wakati nikiwa mdogo mama ndiye alikuwa tegemeo kubwa katika familia, alikuwa akienda kusenya kuni akiuza ndipo tunapata riziki ya kula. Familia ilikuwa inategemea jitihada za mama, kusomesha, kula na kila kitu. Leo hii wana Tarime tunaona jitihada kubwa za mama yetu mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kulijenga Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapozungumza tayari soko ambalo lilikuwa ni tatizo kubwa katika mji wetu wa Tarime tayari limejengwa liko katika asilimia 75 ili liweze kukamilika wapate sehemu ya kufanyia biashara. Vilevile kubwa zaidi ni ule mradi mkubwa wa maji kutoka Ziwa Victoria. Mji wetu tulikuwa tunapata shida kubwa sana. Maji tuliyokuwa tunatumia yamechanganyikana na tope, magonjwa ya bilharzia na Magonjwa ya kuhara yalikuwa ni sehemu ya Maisha yetu. Sasa mradi huu wa maji utakuwa ni ukombozi wa wana Tarime. Kwa hiyo nichukue nafasi hii kumpongeza Rais wetu kwa kutupa fedha za kutosha kwa ajili ya kuleta maji katika mji wetu wa Tarime.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuwapongeza mawaziri wote kwa kazi nzuri wanazozifanya, lakini niwaombe

wasiwe wanakwenda kwenye majimbo yetu kimya kimya, na wakati mwingine wanakwenda bila kutoa hata taarifa kwa Wabunge. Ni matarajio ya wananchi kuona Mawaziri wakizungumza nao na kueleza mambo makubwa ambayo Serikali imefanya kupitia kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine Mawaziri wanaenda pale kinyemela kinyemela, unashtukia tu anaenda kwenye ofisi ya Mkuu wa Wilaya, wananchi wanaambulia kuona misafara na vimuli muli vinapita. Tungependa waweze kufanya mikutano, waweze kuzungumza matendo makubwa ambayo yanafanyika kupitia Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa sana kwa upande wa madarasa, vituo vya afya na kujenga hospitali. Kwa mfano, kwa kipindi cha kuanzia 2021 mpaka sasa hivi kumejengwa hospitali zaidi ya kumi za rufaa za mikoa. Vile vile hospitali 102, vituo vya afya 487 na Zahanati 1,198. Upanuzi wa vituo hivi, na madarasa unahitaji wafanya kazi ambao wanahitajika kufanya kazi katika vituo hivyo, zahanati hizi pamoja na shule ambazo zimejengwa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini takribani wafanyakazi watumishi waliopo katika Serikali yetu ni takribani laki saba ambayo kwa ujumla kila Mbunge anayesimama anaongelea kuhusu upungufu wa watumishi katika majimbo yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushauri jambo moja. Kila mwaka wahitimu wanahitimu katika vyuo vyetu, na wahitimu hao wanapotoka katika vyuo vyetu wanaenda kufanya shughuli ambazo haziendani na kazi walizosomea. Kwa mfano mtu amesomea udaktari ameenda kufanya kazi ya kupiga debe stendi; sasa amefanya kazi ya kupiga debe ndani ya miaka sita mfululizo. Kwa mfano ajira zilizotoka hivi juzi akaajiriwa mpiga debe ambaye amefanya kazi kwa miaka sita akaenda kutibu mgonjwa. Kama tunavyojua mtu

akikaa muda mrefu bila kuendeleza taaluma yake kile anachokifanya kinaingia kichwani mwake na anaendelea kukifanya. Ni nini tunategemea basi? Hatima yake ni kwamba hatutegemei atoe huduma iliyo bora, hata kauli atakayokuwa anatoa haitakuwa kauli ya taaluma aliyoisomea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile ningependa kusema hili. Ukiangalia sasa hivi wale wanao ajiriwa *loan board* inaenda kuwadai walipe mikopo, na ukiangalia mishahara yao *especially* wale wanao ajiriwa katika sekta binafsi unakuta mtu anapata mshahara wa laki tatu, mshahara wa laki nne, anadaiwa alipe makato yote pamoja na mkopo huu wa *loan board*. Hii inapelekea apate kitu kidogo sana ambacho hakiwezi kustahimilisha maisha yake ya kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa nishauri kuwepo utaratibu, sera madhubuti iandaliwe, ambayo itaruhusu wahitimu wote walio hitimu waweze kwenda kujitolea katika sehemu zao walikotoka. Kama ni madaktari waende kwenye hospitali, zahanati na vituo vya afya vilivyo katika maeneo yao. Hii itapunguza gharama za maisha kwa sababu atakuwa anatoka nyumbani anaenda kufanya kazi. Lakini vile vile wakati anajitolea Serikali ipange utaratibu mzuri waweze kuwalipia mikopo hiyo kidogo kidogo kwa sababu wanafanya kazi, ili atakapokuwa wameajiriwa *at least* ipunguze makali ya makato ambayo huwa wanakatwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujitolea kunajenga mtu aweze kupata uzoefu, ajenge na kuwa na uzalendo wa nchi yake na pia kujitolea ni tendo la upendo. Kwa hiyo tutakuwa tumejenga uzalendo katika nchi yetu, kwamba watu wakimaliza elimu yao vyuoni watakwenda kujitolea, kwa hivyo tutakuwa na watumishi wengi, jambo ambalo litapunguza uhaba wa madaktari, walimu na watumishi katika idara zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba, hili nilishalisema, lakini ninarudia kusema kwa sababu ninaona kwanza huduma zinazotolewa katika taasisi na idara zetu za Serikali wakati mwingine zinakuwa ni chini ya kiwango kwa sababu watu waliotoka pale ni wametoka *direct* kutoka kupiga debe, kuendesha boda boda, wakulima na ile fani ambayo waliisomea hata imesha yeyuko kutoka kwenye akili zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa Serikali ichukue hili kwa *u-serious* ili iweze kulifanyia kazi na tuondokane na tatizo la upungufu wa watumishi katika idara zetu. Lakini vile vile itasaidia kujenga uzalendo na vijana wetu kupata ujuzi wa kufanya shughuli zao kikamilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,ukiangalia katika Sekta ya elimu, kwa mfano kwa mwaka 2020, utafiti uliofanywa na taasisi isiyo ya kiserikali ya *BEST* ilibainisha kwamba kuna upungufu wa watumishi katika idara ya elimu zaidi ya 50,993, hiyo ni miaka hiyo kabla ya madarasa hayo kujengwa na shule kupanuliwa. Kwa hiyo sasa hivi kutakuwa na uhitaji mkubwa wa watumishi katika sekta ya elimu pamoja na sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kuondokana na tatizo hili, ambalo ni kubwa na ni sugu katika nchi yetu. Najua kwamba si Tanzania peke yake, ni nchi nyingi, ningependa sana Serikali kupitia Wizara hii wafanye mchakato wa kuandaa sera ya kuhakikisha kwamba wale wahitimu wanaotoka katika Vyuo vyetu wanapata nafasi ya kujitolea katika maeneo yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti….

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKTITI:** Mheshimiwa Kembaki, ahsante sana na muda wako umekwisha.

**MHE. MICHAEL M. KEMBAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Nilimwita Mheshimiwa Yustina Rahhi wakati huo Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga anajiandaa.

**MHE. YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora. Ukiangalia majukumu ya Msingi ya Wizara hii ni kutengeneza Miundo, Sera na Nyaraka ambazo ni rafiki zinazotoa hamasa kwa watumishi wetu. Hata hivyo, kuna Miundo ya Utumishi ya muda mrefu, Muundo wa toka mwaka 2002 na miundo mingine. Hii miundo imebaki kuwanyanyasa watumishi au kuwa *threat* kwa watumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu watumishi wa umma kila mmoja anaajiriwa kwa muundo wake. Kwa mfano, watumishi wanaoajiriwa kwenye wa Muundo Mwandamizi, nitoe mfano kama Maafisa Kilimo, anaajiriwa kama *Agriculture Field Officer* au Afisa Kilimo Mwandamizi ana mahali pake akifikia *bar,* kwa mfano *TGS G* hawezi kuendelea ndio mwisho wa muundo wake. Mtumishi huyo akienda kujiendeleza akasoma, pengine ametoka *diploma* ameenda *degree,* badala ya kupata *promotion* sasa kama alikuwa *TGS G* atoke pale aende *H* muundo unamrudisha mpaka pale kwenye *TGS D*. Sasa *TGS D* mpaka kwenda *TGS E* anahitaji miaka mitatu, kama kweli muundo utampandisha *smoothly.* Akitoka *D* kwenda *E* miaka mitatu, akitoka *D* kwenda hiyo *G* yake miaka mitatu mingine. Sasa mpaka kwenda kumvusha mpaka kwenye *H* ni miaka tisa mpaka 12. Hivi Muundo huu ni rafiki kwa wafanyakazi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa unam-*frustrate* mfanyakazi ambaye tayari alishajiendeleza mwenyewe na anajiendeleza kwa ajili ya kutoa huduma bora. Iko hivyo hivyo hata kwa watumishi wa Afya. *Ma-nurse* wetu wanaosoma *RNDA* au *train nurse* darasa la saba amehamasishwa ameenda kusoma *form four* amemaliza, ameenda kuchukua *diploma,* wanapopata *diploma* akirudi kwenye utumishi, muundo ule una-*frustrate* wanashindwa kwenda mbele na wenzao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu cha kushangaza, sijui kwa nini tunatenga watumishi? Muundo huu ukienda kwa Walimu, Mwalimu mwenye *diploma* akienda kusoma *degree,* yeye anahama moja kwa moja na ule muundo wa watu wenye *degree*, hakuna kinachomrudisha nyuma kama maeneo mengine. Sasa ifike muda basi niiombe Wizara hebu wa-*review* hii miundo. Miundo ambayo sio rafiki kwa watumishi, miundo inayokandamiza watumishi na kuwa-*frustrate*. Kama sasa hivi sio hitaji, umefika muda sasa ku-*review* na kuachana nayo na kuangalia namna nyingine ya ku-*motivate* mtu ambaye ameamua kujiendeleza, ukitegemea sasa hivi dunia inaenda na teknolojia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, lakini inakuwa mbaya zaidi kama mtumishi wa Idara tofauti ameenda kusomea kitu tofauti, hapo ndipo unammaliza kabisa. Kwa mfano, Mwalimu, yeye toka mwanzo wito wake ulikuwa unamtuma labda kusomea kitu kingine Afisa Utumishi au Mwanasheria, akajiendeleza yeye mwenyewe, maana huko nyuma atakuwa alisaidiwa na wazazi, pengine fursa ilikuwa ni kwenda Chuo cha Elimu na fursa ya kupata utumishi ilikuwa ni hiyo, lakini atakapokuwa mkubwa na mshahara wake amejiendeleza na pengine halmashauri imempa nafasi ya kuwa labda Mwanasheria, anarudishwa kwenye muundo ule wa kuanza wa *degree,* lakini hata ile *personal salary* yake inafutwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshawahi kuona mtumishi anapunguziwa mshahara, anaenda kuanza kwenye mshahara wa chini. Hii miundo mingine naomba sasa ufike muda tu-*review,* tuone ni namna gani ambapo watumishi sasa wawe na furaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hili muundo wa hivi karibuni wa Halmashauri sijui *restructuring* maana nilishawahi kuuliza huko nyuma kama swali. Pengine nia ni njema halmashauri kwa ajili ya kubana matumizi imebadilisha muundo, ilikuwa na idara 13 na vitengo, sasa hivi imebana zile idara zimebaki idara tisa. Kwa maana hiyo kuna Idara zimeunganishwa kama za Kilimo na Vitengo vingine kama vya Uchaguzi vimefutwa, Idara kama ya Fedha imekuwa kitengo, *can you imagine* idara ya fedha ndio mkono wa Mkurugenzi pale. Sasa pengine sio shida, sijui kama kuna utafiti wa kutosha uliofanywa kuunganisha Idara za Kilimo na Mifugo pamoja na zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa *stress* zinatoka kwamba mtumishi ambaye alishawahi kuwa Mkuu wa Idara sasa unampoeleka chini ya Mkuu wa Idara nyingine, *it is enough torture to him (psychological torture*) yaani hawezi kuwa *happy* kufanya kazi chini ya idara nyingine. Vile vile na ufanisi utakuwa chini, kwa sababu taaluma ya kilimo ni tofauti na taaluma ya mifugo. Haiwezekani mtu wa mifugo ukimpa asimamie kilimo kwa vyovyote vile atakuwa *bias.* Niombe wafanye *review. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu tatizo ni kwamba, kama tulikuwa tunabana matumizi, hawa Wakuu wa Idara na Vitengo ambao vitengo vyao vimefutwa kwa mfano Afisa Uchaguzi, huwezi kumnyang'anya mshahara wake na stahiki zake za Mkuu wa Idara, ataendelea kubaki nayo. Kwa hiyo, ataendelea kupata mshahara wa Mkuu wa Idara na zile stahili ambapo hakuzifanyia kazi na huwezi kumwacha pale kwa sababu atakuwa hayuko *happy*. Sasa sijui

wamejipangaje kumjengea *job satisfaction* huyu mtu aweze kuwa *happy* sasa kuendelea? Kama alikuwa ni Mwalimu, utamrudisha kwenye chaki, alishakuwa Mkuu wa Idara, fikiria ukimrudisha kwenye chaki, ni kweli ataenda kufanya utumishi vizuri? Napendekeza, pengine ikibidi kwa hawa watumishi ambao idara zao zimefutwa labda wapelekwe kwa *RS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nataka kusema kuhusu watumishi wa Sekretarieti ya Mkoa wanavyopatikana. Watumishi hawa *RS* (Sekretarieti ya Mkoa) kazi yao kubwa ni kusimamia watumishi pamoja na Wakuu wa Idara katika halmashauri. Hata hivyo, hebu ona unamwajiri mtu kijana aliyetoka chuo unamweka pale kwenye Sekretarieti ya Mkoa. Anatoka huko anaenda kusimamia miradi ya halmashauri. Kama ni *Engineer* wa Umwagiliaji anakuja yule *technician* wa umwagiliaji aliyeko kule kwenye halmashauri ana *knowledge* kumshinda yeye. Ndio maana wakija wakubwa, akija Waziri Mkuu au Waziri mwingine kukagua miradi anakuja kukuta miradi mingine iko chini ya kiwango na lazima ina mapungufu. Sasa jiulize kama *RS* (Sekretarieti ya Mkoa) ilikuwepo pale walitoa ushauri gani huko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza wa-*review* utaratibu wa kupata Sekretarieti ya Mkoa kwa sababu wao ni wasimamizi wa miradi yote ya halmashauri pamoja na Wakuu wa Idara, wafanyiwe kama wanavyofanyiwa Wakuu wa Idara, wawe na *experience* ya kufanya kazi kwa miaka sita kama Wakuu wa Idara na wafanyiwe *vetting,* halafu wapate *promotion* ya kwenda Mkoani. Hii itawa-*motivate* pia watumishi wetu wengine kwenye halmashauri wajue kwamba watumishi wakifanya vizuri kuna *promotion* ya kwenda Mkoani. Hiyo itasaidia sana, naomba hilo waliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza na kusema ukweli nampongeza na Mama, kipindi hiki ndipo tumepata nafasi za ajira kuliko kipindi kingine chochote. Nashukuru kwamba ajira

nyingi zimekwenda kwa Walimu pamoja na watumishi wa afya, lakini kuna Wizara tunazisahau…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Yustina Rahhi kwa mchango wako, unaweza kuunga mkono hoja kama ulidhamiria. *(Kicheko)*

**MHE: YUSTINA A. RAHHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Muda wako ulikuwa umeisha, lakini ulivyoanza kumpongeza Mama nikasema nikuongeze sekunde kadhaa, tunakushuru.

Tunaendelea na Mheshimiwa Benaya Luika Kapinga, wakati huo Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge anajiandaa.

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kutoa mchango wangu katika Wizara hii nyeti. Kwanza kabisa nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na Naibu wake. Najua ni wachapa kazi, kwa hiyo niwapongeze sana. Vile vile niwapongeze wataalam ambao wako katika Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais mwaka jana alirudisha furaha kwa watumishi waliokuwa wameondolewa kazini kwa kusema ile asilimia tano irejeshwe kwa watumishi ambao awali ilionekana hawana haki ya kulipwa chochote. Jambo hili limerudisha furaha kubwa kwa watumishi ndani ya Tanzania hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wale wameanza kulipwa, baadhi yao wamelipwa, lakini bado kuna watumishi hawajalipwa. Kwa hiyo niiombe Serikali ifanye jambo hili haraka kama agizo lilivyotolewa ili ile furaha ambayo watumishi walianza kuwa nayo iendelee na iwepo, isije sasa ikaonekana jambo hili limesemwa halafu watumishi wanaendelea kusononeka, wanarudisha masikitiko na masononeko kwa Serikali yao ambayo inawapenda sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie suala la ajira. Amezungumza vizuri sana mwenzangu Mheshimiwa Ezra hapa. Ikumbukwe na ifahamike sisi hapa hatusemi maneno yetu wenyewe, yale yote tunayoyazungumza ni maneno ya wale waliotutuma kuja hapa Bungeni. Kule kwenye maeneo yetu ndiko wanakoenda hao watumishi wanaoajiriwa kwa mtindo ule ambao Waziri wa TAMISEMI jana alizungumza hapa. Ni utaratibu mzuri, lakini ule utaratibu una manung'uniko huko kwenye majimbo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, manung'uniko ni mengi sana. Baadhi ya wananchi wanasema ajira hizi zinatolewa upande fulani na wanataja. Naogopa tu kusema hapa, kwa sababu wanawaona mtu fulani kwa jina na majina yanafahamika. Unaona Walimu wameletwa labda 10, katika 10 wale nane majina yanafanana ni ya maeneo fulani. Kwa hiyo, wananchi wanasema kwamba ajira hizi zinatolewa kwa ukanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno yale wanatupatia sisi kama wawakilishi wao. Sasa kwa sababu tunakuwa hatuna takwimu, hatuna *data* pale za kusema kwenye jimbo langu mimi hapa, kwenye halmashauri yangu hii mimi wametoka watumishi wa ngapi? Kwa hiyo, hapa ndio namuunga mkono Mheshimiwa Ezra kwamba idadi ile ikigawanywa kwa halmashauri zote pengine sisi tutakuwa na majibu mazuri kwa wale wananchi tofauti na ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana jambo hili watusikilize, hatuna nia mbaya na Serikali yetu, tunaipenda sana, najua Serikali zinaongea, Serikali inazungumza, wafanye mawasiliano watusikilize. Kwanza, watoe kwa wale waliokuwa wanajitolea, lakini pili kwa kila jimbo, kwa kila halmashauri basi kuwe na idadi fulani ambayo mimi Mbunge nikienda kuongea nasema hapa bwana kuna orodha ya watu hawa ametoka katika halmashauri hii, itakuwa imekaa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nilikuwa nataka niongelee suala la ujibuji wa barua. Watumishi wetu hawa wanaandika barua pengine wanakuwa na vikwazo na matatizo fulani kwenye idara husika au eneo fulani analofanyia kazi. Anakuwa amesimamishwa au ana jambo tatizo fulani anaambiwa aandike barua. Anaandika barua, mwisho wa siku anakata rufaa, ipo kwenye Wizara ya Mheshimiwa Waziri, majibu yale hayarudi, inachukua muda mrefu sana watu kujibiwa majibu. Sasa sijajua hiki kitengo hakina watu wa kutosha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama shida ni hiyo, basi waongezewe watu. Mpaka leo nina watu 18 wamepeleka barua toka mwaka 2022. Wale walioondoshwa kwa vyeti *fake* wamepeleka barua katika Ofisi ya Mheshimiwa Waziri, lakini mpaka leo hawajajibiwa. Sasa kutojibiwa inakuwa kero kwa Serikali, inakuwa kero kwa Mbunge, inakuwa kero kwa Serikali iliyoko pale eneo husika kwa maana ya wilaya na halmashauri, kila siku watu wanahudhuria ofisini hapo. Niombe sana Mheshimiwa Waziri aimarishe hiki kitengo, kijibu zile barua, kama ndio iwe ndio, kama hapana iwe hapana ili lile suala liwe limefungwa. Tofauti na ilivyo sasa kila leo simu, kila leo *message,* kila leo ofisini, tunakuwa hatujaimarisha utawala bora katika nchi yetu. Naomba sana hili tulifanyie kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la wastaafu na pensheni; wastaafu wetu hawa wamelihudumia Taifa hili kwa uadilifu mkubwa sana. Wanafika sehemu wanastaafu, wengine wanalipwa kwa muda, lakini watu wengine wanapata shida sana kupata mafao yao. Hata hivyo, wanaweza kuwa wamepata mafao, kuja kupata yale mafao ya mwezi hawapati. Vilevile hawapati saa nyingine si kwa sababu yake yeye kuna kitu kinaitwa tozo. Sasa hii tozo mimi nimeifuatilia, haimhusu yule mtumishi aliyefanya kazi akamaliza muda wake, amekwenda pale ale pensheni yake anaambiwa bwana Serikali, sijui taasisi fulani haikulipa hii tozo. Sasa hii tozo inamhusu nini huyu mtumishi? Jambo hili linaumiza sana, jambo hili halikubaliki.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Matiko, taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tu kumpa taarifa msemaji anayechangia kuhusiana na kadhia wanayoipata wastaafu. Ni kweli alivyosema yaani imekuwa kero. Kwa mfano, mstaafu amepandishwa cheo, alikuwa na cheo fulani amepanda kwenda ngazi fulani ambayo mshahara umepanda, lakini anapostaafu analipwa kikokotoo cha mshahara wa awali sio ambao amepanda cheo. Akiuliza anaambiwa Serikali haikuleta hayo makato. Inatakiwa ulipe kwanza yaani achukue hela pembeni alipe hiyo tozo ya Serikali ili aweze kupewa mafao yakeo. Kwa hiyo, imekuwa ni kero wastaafu wanateseka sana, wengine mpaka wanaweza kufa kabla hawajapata mafao yao.

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Benaya Kapinga unapokea taarifa?

**MHE. BENAYA L. KAPINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipokea taarifa hii tena kwa mikono miwili na ndio ilikuwa hoja yangu ya pili kwamba pamoja na ile ya tozo ambayo nilikuwa naisemea kwamba, hii tozo ni ama taasisi aliyokuwa anaifanyia kazi ama Serikali ilichelewa kupeleka kwenye Mfuko husika. Huyu mtumishi yeye makato yake yalishakwenda, lakini Serikali au taasisi fulani imechelewa kupeleka ile tozo, gharama yake sasa inamrudia mtumishi. Hili jambo si sawa wala sio haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watumishi sasa hivi katika halmashauri yangu wanahangaika na hilo, hawalipwi mafao yao wana miaka mitano. Hawalipwi pensheni yao ya mwezi kwa sababu tu halmashauri haikupeleka tozo, kwa sababu tu Idara ya Elimu wakati huo haikupeleka tozo. Sasa hii tozo jamani, Serikali si wanaongea? Kwa nini wasizungumze huyu mwananchi raia wa kawaida apate haki yake, aendelee kula. Ameshafika miaka 60, miaka yenyewe ya kuishi mwisho 70, sasa atapata lini hela yake? Kwa kweli jambo hili si zuri na si sawa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ndilo hilo alilosema Mheshimiwa Esther kwamba tunachelewa kuwapandisha vyeo hawa watumishi au anapata barua halafu mshahara hauingii miezi mitano au mitatu. Mwisho wa siku anakuja kupata mshahara wa mwezi mmoja, *calculation* inayokuja kufanyika inafanyika ile ya kule nyuma sio ile stahiki yake na analipwa hicho, mtumishi huyo anaendelea kuhangaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri, najua yeye ni mchapakazi kweli kweli na ndio maana Mheshimiwa Rais anamwamini na anaendelea kumwamini, naomba hili jambo wakati huu yupo liishe. Vile vile na watumishi kama wananisikia wawasaidie Waheshimiwa Mawaziri hapa, wasikae tu sisi tunasema hapa, tunawasema hawa, wao kule wanafurahia wanafanya mambo yao kama

inavyofanyika siku zote. Si jambo jema, wafanyeni kazi kizalendo, waisaidie nchi hii, wamsaidie Mheshimiwa Rais wa Nchi hii kuondoa kero katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kulisemea ni suala la Sekretarieti ya Ajira. Tulianza vizuri ilikuwa inaenda vizuri na ilikuwa inafanya kazi vizuri. Najua lengo la Serikali ni kuleta umoja ndani ya nchi yetu. Haya mambo tunayosema ukanda fulani ili yasijitokeze, lakini sasa hivi zimeibuka baadhi ya tasisi zinataka zenyewe sasa ziajiri zenyewe. Jambo hili sio jema tutarudi kule kule ambako tunafikiri sasa ukanda ule ndio utaendelea zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalikuwepo maneno *TRA* wamejaa watu wa ukanda fulani, Bandari wamejaa watu wa ukanda fulani wakati fulani, lakini hapa katikati yalipungua sana. Kwa hiyo, niombe tuiboreshe Sekretarieti ya Ajira, badala ya kufikiri kurudisha tena kule hizi taasisi zikawa zinaajiri zenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Benaya Liuka Kapinga kwa mchango wako.

Nilimwita Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge, wakati huo Mheshimiwa Ramadhan Londo na Mheshimiwa Fransis Kumba Ndulane, pamoja na Mheshimiwa Kasalali Mageni wanajiandaa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nikianza kwa kumpongeza mwenye Ofisi yake kwa maana ya Mheshimiwa Rais. Pia, niwapongeze wanaomsaidia kwa maana ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Kaka yangu Mheshimiwa

Simbachawene, tuna imani kubwa naye, Waziri *senior* na mjomba wangu Ridhiwani Kikwete tuna imani naye, ni mweledi katika eneo ambalo Mheshimiwa Rais amekupa majukumu hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile, nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipompongeza mtangulizi wa Mheshimiwa Simbachawene, Dada yangu Jenista Mhagama amefanya kazi ambayo imeacha *legacy* katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niungane na wenzangu ambao kwa kweli tunaikumbusha Serikali kuwafikiria wale ambao waliondolewa katika Utumishi wa Umma kwa sababu zisizokuwa na ulazima wowote, Mheshimiwa Jenista Mhagama amefanya kazi kubwa asilimia kubwa wamerudi, kwa sababu kauli ya Mheshimiwa Rais anasema kazi iendelee ninaomba Mheshimiwa Simbachawene endeleza pale ambapo Mheshimiwa Jenista ameachia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wachache ambao wamebaki wakiwemo wale ambao walikuwa na *qualification* za Darasa la Saba naomba Mheshimiwa Waziri shughulikia warudi katika Utumishi wa Umma kwa sababu ilikuwa ni haki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo mimi nianze na ajira. Wachangiaji wengi wamezungumzia katika mfumo ule wa *Central Government* kwa maana ya ajira ambazo zinafanywa na Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma. Nianze na ajira ambazo zinafanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambazo kimsingi zimekasimiwa na Sekretariati ya Ajira katika Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira ambazo zinafanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ni za kisheria lakini sheria hiyo inawataka watu wa Sekretariati ya Ajira wasimamie mchakato wa mwenendo huu, lakini mimi nieleze masikitiko

yangu kwamba usimamizi wa mchakato wa ajira unaofanywa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa unatuondolea imani sisi tunaotoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, bado tunahisi kwamba kuna viashiria vya ubaguzi, kuna viashiria vya upendeleo na kuna viashiria vya kuonea watu wa Mamlaka za Serikali husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na *case study* kutoka katika Halmashauri yangu ya Wilaya ya Kilwa, michakato kadhaa ya ajira imefanyika, karibu mitatu nyuma kutoka sasa lakini hata wale wenye sifa za msingi wanaotoka katika Halmashauri za Wilaya ya Kilwa wamekosa kupata ajira kwa kisingoizio tu kwamba hawakufaulu mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna jambo la kufanyia kazi Serikali na nitoe wito au ushauri kwa Serikali kwamba hebu tukachunguze ajira tatu zilizofanywa kwa mfululizo katika Halmashauri ya Kilwa kama zili-*base on merit,* kama sheria zilizingatiwa na kama weredi ulitumika katika mchakato wa ajira huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kusikitisha zaidi ni kwamba watumishi wale ambao ni wakazi na wazawa wa Halmashauri wanapokuja katika mitihani ya *practical* wanafanya vizuri lakini inapokuja katika *theory* wanaonekana wamefeli, watumishi wanotoka nje ya Kilwa wanapokuja kwenye *theory* wanafanya vizuri kulikoni? Hii kama ni bahati mbaya kwa nini iwe ni bahati mbaya au *by accident* wa ajira tatu mfululizo hata mmoja hapati, hata wale watumishi ambao wamekuwa wakijitolea pale kwa mfano, hata kada ya madereva tu wanakosa ajira sifa za msingi wanazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la kufanyia kazi Serikali. Nimetoa ushauri kwamba likafanyiwe kazi kabla sisi Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa maana mimi Diwani mmojawapo wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa na Madiwani wenzangu  hatujachukua hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika stahiki za Watumishi. Hapa nitazumzia watumishi waliopo katika Utumishi wa Umma na Wastaafu. Pamoja na juhudi ambazo Serikali imeendelea kuzifanya lakini bado katika eneo la matibabu, masomo likizo malimbikizo ya mishahara na *disturbance allowance* kwa wastaafu bado imekuwa ni kizungumkuti katika kuhakikisha kwamba watumishi hawa wanapata stahiki zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe mfano kwa kadhia ambayo imekuwa ikiwakumba wastaafu. Ninayo orodha ya wastaafu waliostaafu katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa tangu mwaka 2018 mpaka leo, ninasikitika kusema kwamba hawajalipwa mafao yao ya kustaafu kulikoni? Nikiwataja kwa uchache wao hapa angalau kwa mfano tu, kuna Mwalimu Mstaafu Omari Mcheula kuna Mwalimu Mstaafu Khadija Bungurumo kuna Mwalimu Mstaafu Salma Kaisi tangu 2018 mpaka leo hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha wakati wengine hebu tuuvae uhusika, *just imagine* kwamba ni wewe ndiyo umetumikia nchi hii kwa weledi kwa mapenzi makubwa tangu 2018 umestaafu mpaka leo hujalipwa, hii ni kadhia lazima Serikali ifanye jambo hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo niseme tu kwamba Mifuko ya Pensheni na hapo kwa upeke yake nauzungumzia mfuko wa *PSSSF* umekuwa ukichelewesha mafao ya watumishi wastaafu, hebu Serikali ichukue hatua katika eneo hili. Mstaafu anastaafu miaka mitano nyuma anakaa tu anahangaikia tu, hili kwa kweli ni jambo ambalo linasikitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo nije katika suala la madaraja. Ninashukuru Serikali ya Awamu ya Sita imeweza kupandisha madaraja watumishi lakini kitu ambacho ninaomba kuikumbusha Serikali ni kwamba zoezi

hili halikufanyika kwa umakini tulioutarajia. Kilichofanyika ni kwamba watumishi ambao pengine kwa miaka mitano na kidogo hivi hawakupandishwa vyeo wakapandishwa kwa mkupuo, tafsiri yake ni kwamba kwenye eneo la utumishi wa umma tunakosa ile dhana ya *seniority,* mtumishi ambaye alikuwa wa kwanza kuajiriwa anajikuta yuko daraja moja na aliyefuatia kuajiriwa, hii itakuja kuleta athari kwenye utaratibu wa kustaafu na kwenye taratibu za mafao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri pamoja na kwamba Serikali imefanyia kazi eneo hili, ushauri wangu ni kwamba ikafanye *review* ya taratibu zote za upandishaji wa madaraja ili kila mtumishi akae kwenye daraja lake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nizungumie suala la motisha kwa Walimu. Huko nyuma tulikuwa na kitu ambacho kwa Walimu kilikuwa kinaitwa *teaching allowance* haitolewi kwa nini Serikali imeondoa *teaching allowance,* nadhani Serikali ambayo ilikuwepo wakati huo iliweka *teaching allowance* kwa Walimu kwa kuzingatia uzito wa jukumu la kazi ya ualimu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nikumbushe tu kwamba mwalimu pamoja na kufundisha, ambapo watu wengi tunadhani kwamba kazi yake ni kufundisha tu, ana kazi kubwa ya kuandaa mpango mzima wa ufundishaji wa mwaka au muhula mzima ambao kiualimu unaitwa *scheme of work,* lakini mwalimu anajukumu la kuandaa *lesson plan,* mwalimu ana jukumu la kuandaa *teaching aid,* utaona walimu kama watatu hivi wanacheza wanaandaa midoli, midoli hivi ndiyo kazi ya Mwalimu na anaifanya nje ya muda wa kazi. Walimu wana kazi ya kuandaa *lesson plan* na sasa hivi wameongezewa kitu kinachoitwa *KPI*. Hii *load* kubwa yote kwa nini Mwalimu asilipwe *teaching allowance* wakati watumishi wengine wanalipwa kitu kinachoitwa *responsibility allowance, ration allowance, on call allowance* kwa nini Mwalimu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nalizungumza hili kwa masikitiko makubw,a tutunze heshima ya Walimu katika nchi hii, viongozi wengi wakubwa katika nchi hili wamekuwa ni walimu, kwanini hatumheshimu Mwalimu?*(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wengi wakubwa katika nchi hii wamekuwa ni walimu, Baba wa Taifa ni Mwalimu, Mzee Alli Hassan Mwinyi ni Mwalimu, Hayati Magufuli ni Mwalimu, Waziri Mkuu wa sasa hivi Kassim Majaliwa ni Mwalimu, kwa nini hatutunzi heshima ya Walimu? Spika wa Bunge ni Mwalimu, tutunze heshima ya walimu kwa kuhakikisha kwamba walimu tunawatendea haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakumbushwa hapa kwamba Waziri wa nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu ni Mwalimu, pia nakumbushwa kwamba Waziri wa Elimu ni Mwalimu, nakumbushwa pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu mwingine ni mwalimu, sasa Ndugu zangu ni kwa nini hatuwatendei haki walimu, rudisheni *teaching allowance* kwa walimu. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya masuala ya kwamba *performance* na nini na nini hayana mpango wowote, muwezeshe mwalimu, toa motisha kwa walimu, elimu itapanda katika nchi hii.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa masikitiko makubwa, nimesahau hata Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani, ndugu yangu Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini ni mwalimu. *(Kicheko/Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ally Kassinge muda wako ulikuwa umekwisha lakini kwa mamlaka niliyonayo nakuongeza dakika nyingine moja ili uweze kumalizia na pengine ufahamu pia na Kiongozi wa Muhimili huu pia ni mwalimu.*(Makofi)*

**MHE. ALLY M. KASSINGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri wa bure na wa nia njema, hatuzungumzi kwa namna ya kufurahisha Bunge lakini ni ushauri wa bure na wa nia njema, hebu tutunze hali ya mwalimu katika nchi hii, turudishe *teaching allowance* kwa walimu. Ufaulu utaongezeka kwa kumwezesha na kumpa motisha Mwalimu na siyo vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwa kuniongezea muda na wewe utawekwa katika alama ya kumbukumbu kwamba ulimwongezea muda Mbunge anayechangia hotuba hii kwa kuhakikisha kwamba walimu wanapewa fursa ya kusikilizwa na haya yakifanyika tutakuweka katika kumbukumbu, wekeni alama Mheshimiwa Simbachawene, Mheshimiwa Waziri wa Elimu wekeni alama kwa kuhakikisha kwamba mnarudisha motisha kwa kwa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Mohamed Kassinge kwa mchango wako. Nilimtaja Mheshimiwa Ramadhani Ighondo Abeid wakati huo Mheshimiwa Ndulane na Mheshimiwa Mageni wanajiandaa.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia katika mjadala wetu huu muhimu wa Wizara ya Utumishi na Utawala Bora.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa naomba tumsikilize Mheshimiwa Mbunge anachangia, tusikilizane.

**MHE. ABEI R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nianze kwanza kwa kuwapongeza Watendaji wa Wizara hii kwa kuanza na Mheshimiwa Waziri ambaye kwanza amepewa majukumu haya kwa muda mfupi uliopita, nadhani haizidi hata mwenzi mmoja lakini anaonekana kuyamudu vizuri majukumu yake na hata hotuba yake ilikuwa nzuri pamoja na Naibu wake pia ni kijana mwenzetu tuna imani naye, kwa hiyo tunawatakia kila la kheri kwenye utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Katibu Mkuu wa Wizara naye ni kijana mwenzetu, tunaamini kwamba kwa upya wao huo, tunatarajia mambo mengi mazuri yanaenda kutekelezeka kwa maana ya kwamba utakuwa ni utumishi usiozingatia mazoea, siyo utumishi unaofanya kazi kwa mazoea, tunataka *creativity* tunataka tunaone mambo mapya tunayoyazungumza hapa yanafanyiwa kazi na tunataka tuone mabadiliko, waboreshe utumishi, waboreshe utendaji katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na jambo kubwa moja ambalo lilikuwa kwenye moyo wangu kuhusu mafao kwa wastaafu hasa hasa kwenye eneo la kikokotoo. Ninamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ambae aliridhia kikokotoo hiki kutoka kwenye asilimia 25 kwenda kwenye asilimia 33. Jambo hili bado lina manung'uniko kwenye eneo la utekelezaji, watumishi hasa wastaafu bado wana malalamiko kwenye kiwango wanachopewa cha mafao lakini pia kumekuwa na usumbufu mkubwa baada ya kuunganisha ile mifuko ya jamii liliyokuwa mitano kwenda kwenye mfuko mmoja uliobaki, hivi sasa kumekuwa na malalamiko mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtumishi anakwenda pale ile *filling system* ya taarifa zake ni mbovu, anaambiwa wewe ulikuwa *LAPF* sisi *PSSF* hatuna taarifa zako, anakwenda anaambiwa nenda rudi, hivi na ni watu wazima wazee tunaotarajia waheshimike na wahudumiwe ipasavyo, ninaomba tuhakikishe tunaboresha huduma kwa wastaafu hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kile kiwango ambacho kiliridhiwa walipokaa waajiri, Serikali pamoja na kile Chama cha Wafanyakazi kwamba iwe asilimia 33 bado jambo hili watumishi hawajaridhika nalo walio wengi. Naomba niwe *very sincere* nizungumze kile kulichopo moyoni mwangu na sisi tuko kwa wananchi, tunaishi na wananchi hawa wanaostaafu ndiyo wanarudi wanakuwa wapigakura wetu na tuna watarajia waje watupigie kura 2025 watampigia kura Mheshimiwa Samia watatupia kura na sisi wote tulioko hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana jambo lirudiwe tena liende kwenye majadiliano liangaliwe upya, yale malalamiko mapungufu taliyopo yakafanyiwe kazi, wastaafu wanapata taabu, naomba lifanyiwe kazi mapungufu yaliyopo yatatuliwe ili wastaafu hawa nao waweze kunufaika na waweze kuishi vizuri maisha yao ya ustaafu.*(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni hili jambo la ajira ambalo tumekuwa tukulizungumza sana hapa Bungeni ambao ni mjadala mkubwa hivi sasa. Kwenye eneo la ajira hapa tuna wataalam bobezi hapa, wakiwemo walimu wetu waliotufundisha vyuo vikuu, walitufundisha kuajiri kwa kuzingatia sifa kwa kuondokana mambo ya nepotism, tuzingatie bureaucratic systems, kwa kuajiri kupitia nepotism mambo ya udugu, kufahamiana huyu ni mtoto wa fulani, huu ni ushamba, huu ni utumishi wa kishamba, mtu mshamba ambae hajastaarabika ataenda kumuangalia ndugu yake*

*badala ya kuzingatia sifa.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakemea kabisa wale wanaoajiri watu kwa kuangalia nyuso badala ya kuangalia sifa walizonazo, hili tutaliepuka endapo tutaenda kuondokana na kufanya *interview* kwa *face to face* huu utaratibu uliopo hivi sasa wa kuwakusanya Watanzania kutoka Mtwara, kutoka Katavi kutoka Mwanza huko Kagera, kutoka sijui wapi Ukerewe, kuwalete Dodoma kuja kufanya *interview* ni mambo ya kishamba haya *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuende sasa kwenye kuzingatia TEHAMA, sasa hivi wenzetu wanaajiri kwa kutumia kompyuta. Kama watoto walienda Vyuo Vikuu kwa ku-*apply* kwenye kompyuta huko vijijini mwao, kwa nini wasifanye hizi *interview* au wasi-*apply* kazi kwa kupitia kompyuta hukohuko waliko kwenye maeneo yao tuepuke gharama, tuepuke usumbufu, tuwasaidie Watanzania hawa masikini wanaotaka kujikomboa kwa kutumia vyeti vyao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu utaratibu wa kuajiri hivi sasa naomba tuzingatie kompyuta, tu-*computerize* mifumo yetu. Tunaweza kufanya *interview* kwenye Mikoa yetu ukawa ni utaratibu ambao uko *fair,* ukam-*accommodate* kila mtu, tena kwa kuzingatia sifa zao. Kama tuliwaita vyuoni kwa kutumia kompyuta tena hukohuko kwenye vijiji wanakotoka kwa nini leo tunapotaka kuwaajiri tunashindwa kutumia kompyuta, kwa nini hatuaminiani shida iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwenye eneo la ajira hizi kelele hazitaisha endapo tutaendelea na ule ukale wa utaratibu tunaoutumia kwenye ajira. Malalamiko yataendela kuwepo, tutaendela kulaumiana bila sababu. Kwa hiyo, ninashauri hapa pamoja na kutumia hizi TEHAMA pia tuunde timu ya kushauri. Tunao wataalam, tunao watu bobezi Maprofesa wasomi wazuri, kwa nini hatutaki kutumia

watu hawa watushauri ipasavyo ili tuweze kuboresha utumishi, tuweze kupata watumishi wazuri wanaoweza kwenda kukutumikia ipasavyo kwenye utumishi wetu.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa...

**MHE. ABEI R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kuhusu watumishi. Tuna vijana wanatembea na bahasha mitaani mpaka wanachoka, viatu yaani wanatembea kama vile vichaa, hata nguo wanashindwa kufua, hawana sabuni hawana nini, lakini tunalalamika tunao upungufu wa watumishi tatizo liko wapi? Kwa nini tunashindwa kuajiri watumishi wanaotosha wakatumikia watu wetu kule vijijini?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ramadhani Ighondo muda wako umekwisha.

**MHE. ABEID R. IGHONDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naunga mkono hoja ninaomba tuajiri watu wakatumikie nchi, vijana wasomi wapo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge. Nilimuita Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane. Wakati huo Mheshimiwa Kasalali Mageni na Profesa Kitila Mkumbo wakiwa wanajiandaa.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwanza, napende kumpongeza Mheshimiwa Rais pamoja na Wizara yetu hii kwa kazi kubwa ambayo wameifanya katika kipindi cha siku hizi za karibuni, kwa kuzingatia utawala bora katika nchi yetu, hasa kwenye ile misingi ya utawala bora ambayo ni haki na usawa, ukweli

na uwazi, ushirikishwaji, uhuru na misingi ya kidemokrasia, kufuata sheria pamoja na kusimamia maslahi ya wengi hapa nchini. *(Makofi)*

*Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuanza kuchangia kwenye suala la mafunzo kwa Maafisa Utumishi. Maafisa Utumishi wetu wengi wamekariri Standing Orders au zile Kanuni za Utumishi wa Umma. Wengi ni mambumbumbu katika Sheria Mama katika Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini.* **[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakuta Maafisa Utumishi wengi wanashindwa ku-*cope* na mazingira na wakati mwingine wanajikuta wanakosea na kuwanyima baadhi ya watumishi wetu haki zao kwa sababu wamekariri tu mambo fulani ambayo yapo kwenye Kanuni za Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimpelekea Afisa Utumishi kwenye sheria mama, Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini, unakuta hajui. Kwa hiyo, napenda kusisitiza, naiomba Serikali iwekeze kwenye kutoa mafunzo kwa hawa Maafisa Utumishi ili waweze kutenda haki kwa watumishi wetu ambao wanatumikia Taifa letu katika ngazi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hili, unakuta kuna baadhi ya Halmashauri, Mkurugenzi anajiamulia tu. Unaweza ukakuta Mkurugenzi kila baada ya miezi sita anahamisha watendaji kata bila ya kuzingatia taratibu na haki zao ambazo wanazostahili. Unakuta Mtendaji Kata leo amehamishiwa kata hii, baada ya miezi sita anahamishiwa kata nyingine, halipwi *disturbance allowance,* halipwi haki yake yoyote. Shida ni kwamba kanuni na sheria na taratibu, hawa Maafisa Utumishi wanashindwa kuwaelekeza hawa Maafisa Masuuli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la upungufu wa watumishi. Bado kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi, japokuwa Serikali imejitahidi kwa miaka ya hivi karibuni, na hivi karibuni wametangaza hizo ajira 21,200, lakini bado tatizo ni kubwa. Tatizo limekuwa kubwa zaidi hasa kwa Halmashauri zetu za Wilaya. Watumishi wengi wakiajiriwa, unakuta wakishapata tu uthibitisho kazini, wanahama kutoka kwenye Halmashauri zetu za Wilaya zenye vijiji vingi, kwenda Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali katika eneo hili ijitahidi kudhibiti taratibu za uhamisho ili wakishaajiriwa waendelee kubaki kule kwenye vijiji vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda kwenye zahanati na shule, utakuta walimu ni wachache; manesi, utakuta ni mmoja tu, na ndio huyo huyo, hakuna *Clinical Officer,* hakuna daktari. Kwa hiyo, ni shida juu ya shida. Pamoja na kwamba tumeongeza miundombinu ya madarasa, maabara na zahanati, lakini unakuta zahanati hizo zimebaki zikiwa hazina watumishi wa kutosha, na mwisho wa siku wananchi wanakosa huduma muhimu katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niseme, Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Ally Kassinge, Mbunge wa Kilwa amezungumza hapa kwa uchungu kabisa na kwa hisia kubwa. Naye alikuwa Mwalimu siku zilizopita. Anajua vizuri katika masuala ya ualimu. Upungufu wa Walimu umesababisha hasa kwenye masomo ya sayansi, walimu wamefikia hatua wanapangiwa vipindi kati ya 35 mpaka 64 kule kwenye Halmashauri yetu ya Wilaya ya Kilwa, lakini *standard* ni vipindi 24 mpaka 30. Kwa hiyo, unaweza ukaona hali halisi ilivyo. Kwa hiyo, Walimu wanafanya kazi katika mazingira magumu na mwisho wa siku maisha yao yamekuwa magumu vile vile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna madai mbalimbali ya walimu. Yamekuwa aidha yakichelewa kulipwa na wakati mwingine hayalipwi kabisa na wanapigwa danadana tu. Unakuta madai ya tangu mwaka 2015 mpaka leo bado hayajalipwa. Hata yakilipwa, mtu anadai Shilingi 500,000/= analipwa Sh. 180,000/=, anaambiwa hii utalipwa baadaye na ndiyo imetoka hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nyumba kwa watumishi nayo ni changamoto kubwa. Hii imelazimu sasa watumishi wengi wanaolazimika kukaa maeneo ya mbali yenye nyumba zinazostahili ambazo ziko mbali na vituo vyao vya ajira. Kwa hiyo, naomba Serikali iliangalie jambo hilo ili kuboresha hasa kwenye sSekta hii ya elimu na sekta ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuzungumzia suala la wathibiti ubora. Mwaka 2022 nilizungumza juu ya changamoto iliyopo kwa watumishi hawa muhimu wathibiti ubora, wamekuwa wakifanya kazi kubwa katika mazingira magumu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, mwaka 2014 nilishawahi kusema, ulitoka waraka ambao unahusu viwango vya mishahara pamoja na viwango vya posho za madaraka kwa viongozi wa elimu, lakini yale mabadiliko ambayo yalitolewa kulingana na waraka ule wa mwaka 2014, yameweza kutumika tu kwa wale ambao wako kwenye kada ya elimu yenyewe; walimu wakuu, waratibu wa elimu, Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa, lakini hawa Wathibiti Ubora wa Wilaya na wa Kanda hawajaweza kubadilishiwa. Pamoja na kuzungumza mwaka 2022 mpaka leo hii, hawajabadilishiwa miundo yao, hawajabadilishiwa posho zao, hawalipwi stahiki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba iwalipe stahiki zao pamoja na *arrears* zake ili waweze kufanya kazi kwa bidii na kwa umahiri ili tuweze

kupata elimu iliyo bora. Kwa sababu unaweza ukafundisha darasani, lakini kama hakuna *assurance* kwenye elimu, ni kazi bure. Utakuta hiyo elimu haifuatiliwi, kama kuna uzembe haufatiliwi, au kuna kulegalega katika kufuatilia mambo kama hayo. Kwa hiyo, kwa ujumla napenda hilo nalo lizangatiwe ili basi hawa wathibiti ubora nao waweze kusaidiwa na kuweza kupata haki zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la wastaafu. Wenzangu wamezungumza sana kwa kirefu, nami labda nizungumze kwa kifupi tu. Wastaafu wamekuwa wakichelewa sana kupewa haki zao. Naomba hao wazee wetu wapewe kipaumbele. Katika mwaka wa fedha unaokuja watengewe bajeti inayotosha kulipa haki zao za mizigo na haki nyingine ili hatimaye pale wanapostaafu, walipwe mara moja na waweze kwenda kurudi katika maeneo yao ambayo wanatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ndulane kwa mchango wako. Nilimwita Mheshimiwa Kasalali Mageni, na wakati huo mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa ni Mheshimiwa Profesa Kitila Alexander Mkumbo.

**MHE. KASALALI E. MAGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa uzima na afya. Pia nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kutupatia nafasi za ajiri zaidi ya 21,000 ni jambo jema na ni jambo la kupewa heshima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nitumie nafasi hii kumpongeza sana Waziri, kaka yangu Mheshimiwa Simbachawene kwa nafasi hii aliyopewa na kwa kazi nzuri

ambayo amekuwa akiifanya katika Wizara mbalimbali alizopita na ninaamini Wizara hii imepata mtu sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Naibu wa Waziri Mheshimiwa Ridhiwani Kikwete, amekuwa ni msaada na kiongozi wa kujituma. Hongera sana Mheshimiwa Naibu Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wengine walivyotangulia kumpongeza Mheshimiwa Jenista Mhagama, Seneta, Waziri mzoefu, mwenye heshima, na anayejituma kufanya kazi yake vizuri; Mheshimiwa Waziri, hongera sana kwa njia uliyoiacha kwenye Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kabla sijaenda mbali, naunga mkono bajeti, kwa sababu naamini watu ninaoenda kuwashauri, watanisikiliza na watafanyia kazi ushauri wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla sijachangia, nataka nitoe takwimu halisi za upungufu wa watumishi kwenye Jimbo la Sumve. Jimbo la Sumve hivi ninavyozungumza ni moja ya majimbo ambayo yako vijijini kwa asilimia mia moja. Ni majimbo ambayo yanakumbana na watumishi kupangiwa kazi na kuanza kuomba uhamisho siku wameanza kazi. Majimbo haya yanatakiwa yaangaliwe kwa jicho la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Sumve ninavyozungumza sasa hivi, tuna upungufu wa walimu wa shule za msingi zaidi ya 1,311, lakini walimu wa shule za sekondari zaidi ya 318. Kwenye Jimbo la Sumve, kuna shule kama Nyang'ingi, shule nzima ina walimu watano. Kuna shule kama Bukala, shule nzima ina walimu saba. Hali ya upatikanaji ya watumishi ni mbaya kwenye maeneo ya vijijini. Serikali bado ina kazi kubwa ya kufanya kwenye sekta hii ya utumishi. Bado tuna upungufu mkubwa wa watumishi, kwa hiyo tunaomba Wizara iliangalie hili kwa jicho la pili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nichangie kama ambavyo wengi wamesema kuhusu mfumo wetu wa ajira. Niliwahi kusema hapa na wengine wamesema. Tunalo tatizo kubwa sasa hivi kwenye nchi yetu la wananchi kupoteza imani na mfumo wetu wa ajira Serikalini; na Wabunge wote wamesema humu. Tunazo meseji mpaka zimejaa kwenye simu, za watu kuomba tuwasaidie kupata kazi Serikalini. Watu wamehamisha imani kwa Wabunge, wameondoa imani kwenye Mfumo wa Serikali wa Ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi tunaowaongoza, wana akili na wanajiongeza. Wanajiongeza kutokana na wanayoyaona. Mfumo wetu wa ajira umekuwa ni mfumo wenye usiri mkubwa sana. Watu wanaomba kwenye Tume ya Ajira; sijui kuna kitu kinaitwa sijui kanzidata na *story* nyingine nyingi. Watu wanamwambia mtu ameomba, aliyekosa amewekwa kwenye kanzidata, mwingine amepewa ajira. Baadaye tena ajira ile ile hawatumii tena kanzidata kumpa ajira huyu waliyemweka, wanatangaza tena ajira nyingine kwenye jambo lile lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wamefika wakati wamegundua kwamba mfumo wa ajira ni wa dili. Sasa kama kweli mfumo wa ajira ni wa dili, ni hatari sana. Tutakuwa tunapokea Ripoti za CAG hapa, watu wametushangaza, kwa sababu wameingia kwa dili. Kwa hiyo, lazima mfumo huu wa ajira tuuangalie kwa namna nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatari kubwa sasa hivi, leo naongea kwa Wizara ya Utumishi, lakini imani ya wananchi mpaka kwenye mfumo wa ajira kwenye majeshi ni ndogo sana. Yaani wananchi wanatupa ujumbe kwamba huko tuna askari wa dili. Sasa nchi kama tunataka hivi ni lazima tujifikirie, yaani kuna kitu kwenye mfumo wa ajira wananchi wameshaondoa imani. Serikali lazima ijitazame na ijiangalie mara mbili. Wananchi bado hawatuamini. Sasa tunafanyaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliwahi kushauri hapa, ajira zikishushwa chini ni rahisi zaidi watu kuwa na imani. Maana watu wamesema hapa, hata ajira hizi kuna maeneo, mimi Mbunge wa Sumve nikikwambia ni wangapi wameajiriwa Sumve, siwezi kusema, maana sijui. Kwa sababu mambo haya yanafanyika juu juu tu. Sasa lazima ifike wakati uwazi uongezeke ili kuwe na mambo yanayoeleweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira hii siyo kwamba tunafanyia tu siasa. Mfano, leo tunasema kuna mfumo ambao TAMISEMI wamesema hapa, ajira wataangalia watu wa 2015, wengine hawawaangalii. Mtu wa 2015 leo ana miaka minane hafanyi kazi yoyote. Hawana *database* ya watu wanaojitolea. Watu wanaojitolea wanachukuliwa kama vile hamna wanachokifanya. Sasa kama Serikali yetu haina *database* ya watu wanaofundisha watoto wetu, inafanya kazi gani? Yaani sisi tumepeleka watoto shuleni, ninyi hamjui wanafundishwa na nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanajitolea huko, wanajiandikisha Walimu Wakuu, kila mwezi wanapeleka ripoti ya watu walioko kwenye shule, kwamba nina walimu kiasi kadhaa. Kumbe tunafanya *formality,* ni mazoea tu, mambo ya kishikaji. Lazima tufike wakati vitu vya msingi tulivyokubaliana vifuatwe. Watu wamejitolea na mnawajua, taarifa za watu wanaojitolea zinajulikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali, hizi nafasi zilizotolewa 21,000 tusiwe na haraka nazo sana, ni nyingi sana, tuzitengenezee mfumo mzuri ili watu wote wapate wanaostahili na zije kuwa na tija. Kwani tuna haraka gani? Kwani lazima tuajiri sasa hivi, si Rais ameshatupa. Hebu tulieni, tusikilizeni tuwaambie, kwamba watu wanaojitolea wanajulikana. *Story* ya kwamba hawajulikani, ni kuidhalilisha Serikali. Walimu Wakuu wanajua hawa watu, na ripoti za kila mwezi kwa Maafisa Elimu zinapelekwa. Leo mnasimama

hapa mnatuambia hamuwajui, mnafanya kazi gani sasa hapa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufike wakati tusimamishe hii ajira ya watu 21,000, tushauriane humu, wote ni watu wazima, tumetumwa na wananchi, tukubaliane nani anaajiriwa, na kwa sifa ipi? Kwa sababu tukiendelea na utaratibu huu, tutaendelea kuwa na watu tu tunaajiri, tunaajiri kwa ajili ya kujifurahisha, lakini watu bora tunawaacha nje, lakini na wananchi wanakosa imani na mfumo wetu wa ajira. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nishauri jambo lingine. Kuna jambo hapa linaitwa kikotoo. Serikali iwape watu fedha zao. Mtu amefanya kazi kwa muda mrefu, amepokea mshahara wake, mlikuwa hamumtunzii, ilikuwa hamhusiki chochote na mshahara wake, leo anastaafu zinakuja *story* kwamba hawezi kutunza hela yake. Wapeni watu hela zao. Wapeni watu hela zao wapambane nazo huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya huko. Kweli kabisa! Humu tunaweza tukakaa tukawa tunafikiri hali ni nzuri; kuhusu wastaafu, wastaafu masikini ni wazee wetu, nasi ni wastaafu watarajiwa, hawariziki na hela yao kutunziwa. Wakitunziwa, hatujui mtu kesho na keshokutwa hayupo, inalipwaje? Tufike wakati mtu apewa hela yake, amefanya kazi kwa heshima kwenye nchi hii, aende akafanye kazi yake vizuri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**TAARIFA**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kasalali Mageni, kuna taarifa kutoka kwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Ndalichako.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (KAZI, AJIRA, VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nilikuwa naomba nimpe taarifa kaka yangu, Mheshimiwa Kasalali Mageni ambaye ninamheshimu sana, na anachangia mchango mzuri, lakini naomba tu hili jambo lisije likapotoshwa kwamba Serikali inaona watu hawawezi kutunza fedha zao. Fedha ambazo mtu analipwa za mkupuo; na nilishafanya semina hata kwa Wabunge; anapata fedha nyingi kuliko hata zile ambazo amechangia katika miaka yake yote ya utumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokizungumzia mafao ya mkupuo, ni ile pensheni ambayo mtu anaipata ambayo makisio ya umri wa kuishi baada ya kustaafu tumekadiria ni miaka 12 na nusu. Kwa hiyo, tunafanya makisio ya fedha yote ta mtu kustaafu halafu katika fedha ile ndiyo tunampa mkupuo wa asilimia 33. Ni tofauti na kile ambacho mtu anakuwa amechangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona tu kaka yangu amechangia vizuri, nimpe hiyo taarifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa taarifa, na muda wa mchangiaji umekwisha.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Ninakuongezea dakika moja na nusu ili uweze kuhitimisha hoja yako Mheshimiwa.

**MHE. KASALALI E. MAGENI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwanza namshukuru Mheshimiwa Waziri,

Mwalimu wangu, nimepokea taarifa yako. Ila nataka tu kusema, hao wanaolalamika siyo kwamba vichwa vyao vimekatwa, wanaona kwamba jambo hili siyo sawa. Nasi kazi yetu ni kuwaambia kwamba wale wastaafu wanalalamika. Wanapolalamika, ni kwetu. Sasa kama mtu anapewa hela nyingi zaidi halafu bado analalamika, sijui, labda wastaafu wetu wana hali ngumu sana za kufikiri; lakini kama ni kweli zile walizotutumikia mpaka nchi yetu imefika hapa, ukweli ni kwamba wanalalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuone namna ya kuwapa hela zao wachukue wakapambane nazo. Tusiwakadirie umri wa kuishi, kila mmoja Mungu ndio anakadiria umri wetu wa kuishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na ninamshukuru Mwalimu wangu wa *Measurement and Evaluation,* Profesa, nakuheshimu sana, lakini wananchi wanasema kwamba hawaridhiki, wanaomba mbadilishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. *(Kicheko/Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nilimwita Profesa Kitila Mkumbo.

**MHE. PROFESA KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa nafasi hii, na kwa kweli nianze mchango wangu kwa kukupongeza, unaendesha kikao vizuri sana. Upo vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nichukue nafasi hii kwa kweli kupongeza sana hatua ya Serikali na Mheshimiwa Rais kutoa kibali cha ajira 21,000. Jambo hili siyo la kupongeza tu kwa maana ya utaratibu wa kawaida. Katika kipindi ambacho dunia nzima ina changamoto ya kiuchumi, katika kipindi ambacho kuna nchi tunavyozungumza leo zimeshindwa kulipa mishahara ya watumishi, katika nchi

ambazo zimeshindwa kulipa mishahara ya Waheshimiwa Wabunge, lakini sisi siyo kwamba tunalipa tu mishahara, tunaajiri watumishi wapya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili haliwezi kupita bila kuzungumziwa vizuri. Ni jambo kubwa, na ni jambo jema. Tunatambua kwamba idadi ya ajira hizi siyo kwamba zinakidhi, lakini lazima kila hatua tuone kwamba ni hatua na sisi kama Wabunge lazima tupongeze na kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na tukishashukuru tunajenga hoja ya kuongezewa zaidi kwa hiyo hilo ni jambo muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika hoja hiyohiyo, viongozi hufanya mambo manne; hujenga, huboresha, hufanya mambo mapya na hurekebisha pale ambapo walipoishia wenzao hapakukaa vizuri. Namimi nataka nichukue nafasi hii, hata hili la kuajiri ni hatua kubwa ya Mheshimiwa Rais ya kurekebisha kwa sababu miaka mitano, sita, saba nchi hii ilikuwa haiajari watumishi. Hawa waliyotoka vyuo vikuu wanafahamu, miaka ya tisini, miaka kumi Serikali iliacha kuajiri watumishi hasa katika vyuo vikuu kwa kitendo hiki ni hatua nzuri ya kurekebisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika muktadha huohuo nataka niombe Serikali warekebishe mambo mengine mengi lakini hasa matatu katika utumishi wa umma, na nataka kuzungumzia utumishi katika vyuo vikuu; kwa sababu pia kwenye Jimbo la Ubungo pale kuna Chuo Kikuu cha Kwanza Tanzania (Chuo Kikuu cha Dar es salaam) ambapo nimewahi kupata bahati ya kukitumikia; kwa sababu kufanya kazi chuo kikuu kama Profesa ni bahati kubwa na mshukuru Mungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa chuo kikuu kwa walimu ni uhuru wa kitaaluma *(academic freedom)*. Yaani mwalimu chuo kikuu lazima anapokaa pale awe na uhuru wa

kufundisha na kufanya utafiti na kusambaza maarifa bila woga wa kufikili kwamba hataingiliwa, ataonewa, atashughulikiwa, atabaguliwa au atanyanyaswa; huu ni msingi ambao unaongoza vyuo Vikuu Vyote Duniani. Ni kwa sababu vyuo vikuu duniani vinakuwa na sheria zake; na sisi tungekuwa na sheria ya vyuo vikuu, kila chuo kingekuwa na sheria yake. Hata hivyo mwaka 2005 Bunge likatunga Sheria linaitwa *Universities Act,* Sheria Na. 07 ya Mwaka 2005, lengo ni kulinda uhuru wa kitaaluma katika vyuo vikuu. Na vyuo vikuu vimeanzisha vyombo vyao vya kujiendesha na kujitawala. Kwa hiyo kazi kubwa ya Serikali imekuwa ni kutoa sera na muelekeo na kutoa rasilimali lakini uendeshaji wa vyuo vikuu unakuwa ndani ya vyuo vikuu vyenyewe. Kwa hiyo kuna vyombo viwili vikubwa; Kuna Baraza la Chuo Kikuu na kuna *Senate, Senate* ni kama Bunge hili. Hili ni jambo la msingi sana ambalo lazima tulielewe, na hivyo hivyo duniani. Sasa hizi nyenzo zimewekwa ili vyuo vikuu vijiendeshe na vilinde uhuru wa kitaaluma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo jambo moja la msingi sana ambalo lazima tulirekebishe ni kuepusha urasimu wa kawaida kuuingiza vyuo vikuu, *bureaucracy* ya kiserikali. Kwa mfano vyuo vikuu duniani na hapa Tanzania siku zote huwa vinaajiri watumishi wake; na ndiyo maana kwenye sheria yetu ambayo nimeisoma *function* namba 05 ya mabaraza ya vyuo vikuu *is to appoint officers of the institutions.* Maana yake waajiri wa vyuo vikuu ni mabaraza ya vyuo vikuu, na ajira za chuo kikuu ni za chuo husika. Ndivyo ilivyo duniani, ndiyo maana inaitwa *university*, yaani u*niversal from the word universal)*. Kwamba misingi ya vyuo vikuu ambayo inafanana duniani kote. Sasa nataka niulize, na mtusaidie kulirekebisha jambo hili. Katika miaka ya hivi karibuni, nadhani kuanzia Mwaka 2015, 2016, tumeamua ajira za vyuo vyuo vikuu zinaendeshwa na Serikali kupitia Sekretarieti ya Ajira. Hili jambo ni *peculiar* kwa Tanzania, halipo vyuo vikuu vyovyote duniani. Yaani huwezi; na naona mmeanza kuhamisha walimu kutoka chuo kimoja kwenda chuo kingine. Mwalimu

wa Chuo Kikuu cha *Oxford* akitaka kwenda *Cambridge* ana-*apply,* anaomba aajiriwe na *Cambridge;* lakini huwezi kukuta Serikali ina muamisha huyo mtu kutoka Chuo Kikuu cha *Cambridge* kwenda *Oxford,* hiyo Duniani haipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo hili jambo lazima mliangalie, muachie vyombo ambavyo tumeunda kisheria kufanya ajira. Hata hizi ajira za walimu ambazo tunalizungumza hapa, tunaona kama jambo la kawaida, kwamba wanaajiri Ofisi ya Rais – TAMISEMI lakini sheria haisemi hivyo. Sheria ya Ajira za Walimu ipo katika Tanzania *Teacher's Service Commission,* na ipo *very clear.* Moja ya majukumu ya *Commission TSC* jukumu namba 03 *is to appoint, promote and discipline teachers.* Kwa hiyo Waziri ana jukumu la kurebisha hapa; na Mheshimiwa Rais moja ya ajenda yake nikufanya maboresho na marekebisho tumsaidie kurekebisha. Moja ya marekebisho ni kwamba Utumishi waache vyombo vya kisheria vifanye kazi zake. *(Makofi)*

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Taarifa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere taarifa.

**TAARIFA**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa maelezo ya mzungumzaji, kwamba kuna Sheria ya Kuajiri Walimu kupitia Tume ya Walimu tunaomba ajira inayoendelea sasa hivi ifutwe tufate sheria iliyopo sasa hivi. *(makofi/vicheko)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kitila Mkumbo, unapokea Taarifa?

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Nimeipokea ni muhimu Serikali ikafanya marekebisho na maboresho. Kama sheria hizi

ambazo tunatunga mnaona hazifanyi kazi leteni tufanye mabadiliko, ni jambo la msingi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ambalo linaendana na hilo, na nataka niweke msisitizo kabisa kabisa; mnaanza kuhamisha walimu kutoka vyuo vikuu kwenda chuo kikuu kingine; hili nimeisha lisema siyo sahihi. Ajira za walimu ni za chuo husika. Kitila Mkumbo akita kwenda chuo kikuu cha *UDOM* ana *apply*. Sasa nyie mmehamisha walimu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es salaam; kwa mfano *a rarely professor environmental economics* mmemtoa pale mkaenda kumtupa Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K. Nyerere cha Kilimo na Teknolojia ambacho hakina wanafunzi, yupo pale hana wanafunzi. *This is a professor* ambayo alikuwa anafanya kazi vizuri sana pale chou kikuu. Mmemuamisha mwalimu ametoka *PHD resource assessment* ana uchungu wa kufanya kazi amekaa siku mbili tatu ana hamishwa kwenye Chuo cha Maji, kufanya nini? Kwa hiyo kaka yangu Ndugu yangu Mheshimiwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Proresa Kitila Alexander Mkumbo, muda wako umeisha.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tusikilizane, huwezi kubishana na kiti, uamuzi nitakaotolewa na kiti utakuwa ndio *final,* kwa hiyo tusikilizane. Kanuni zetu zinatutaka kwamba kiti kikizungumza tunanyamaza kimya. Mheshimiwa Kitila Mkumbo, nakuongeza dakika nne ili uweze kumalizia hoja yako. *(Makofi)*

**MHE. PROF. KITILA A. MKUMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ubarikiwe sana, uko vizuri. Hilo nadhani limeeleweka;

Mheshimiwa George Simbachawene tunakuheshimu, umefanya kazi nzuri naomba hili jambo ulifanyie kazi ulirekebishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu ni ajira za mikataba kwa maprofesa wa vyuo vikuu. Tulikuwa na utaratibu mzuri sana, Profesa akisha ku–*retire* chuo kikuu, vyuo vikuu vinamfanyia tathimini. Akiwa bado ana nguvu na anafanya kazi zake kitaaluma vizuri anapewa mkataba wa miaka miwili miwili mpaka pale tutakapoona kwamba afya yake ya mwili na kiakili imechoka. Jambo hili tukaliondoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ipo hivi; profesa si kama wana michezo, ambaye kadri umri unavyokwenda anazidi kuchoka. Uprofesa ni kama *wine*. *Wine* inavyokaa muda mrefu ndivyo inavyozidi kunoga, profesa unavyozidi kukaa muda mrefu anazidi kubobea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na maprofesa wengi, wanafahamu Profesa Ndalichako, maprofesa wengi wanapata uprofesa *late 50's* na wameongezewa hadi *60's*. Sisi wengine tuliopata tukiwa na miaka 40 tulibahatisha tu, lakini Maprofesa wengi wanapata Uprofesa miaka 50 na kuendelea. Sasa amemaliza tu profesa ndiyo anaanza kubobea mnamuondoa. Kwa hiyo tunaomba utaratibu wa zamani ambapo Profesa akishakustaafu anapewa mkataba uendelee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utaratibu uliopo madhara yake ni nini? Vyuo vikuu vya umma kwa sasa vinaanza kubaki na *junior staff*. Kwa sababu Maprofesa wote ambao wana–*retire* Chuo Kikuu cha Dar es salaam wanakwenda kwenye *private universities;* tunamsaidia nani? Kwa hiyo naomba hili pia Mheshimiwa Waziri aliangalie na alirekebishe lirudishwe kwenye utaratibu ambao ulikuwepo. Kwa sababu tunasema *if it is not broken don't fixed it,* kwa sababu ni kitu kizuri

kilisaidia nchi yetu, kilisaidia vyuo vikuu vyetu. Utaratibu huu kwa nini uliondolewa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni kuwaombea. Wametufata maprofesa wa siku nyingi ambao waliajiriwa kabla ya mwaka 1978 kabla ya *PPF* kuanzishwa; hawa watu hawakuwa kwenye mfumo wa *pension,* waliwekwa katika mfumo wa bima, wanalipwa kitu kinaitwa *SSSS (Serious Staff Superannuation Scheme)*. Hawa maprofesa wameondoka chou kikuu anapata milioni 10, milioni 20. Baadhi yao wameniambia hata ukitaja majina yetu ni sawa tu. Sasa wamebaki maprofesa 180, hawana *pension,* wapo tu. Jambo hili limieshawasilishwa mara nyingi, Serikali imelipokea, hivyo tunaomba Mheshimiwa George Simbachawene kupitia kiti chako jambo hili ulimalizie ili tutunze heshima ya watu ambao wametumikia katika nchi hili miaka 30, miaka 40 katika utumishi wa vyuo vikuu, ni jambo la msingi sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti baada ya kusema hayo nimalizie tena kukushukuru na kukupongeza kwa mchango wako naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

**MWENYEKITI:** Kulikuwa na Muongozo kutoka wapi? Mheshimiwa Amar.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Kanuni ya 76 kwa kuokoa muda kuna uchangiaji ambao sasa hivi unaendelea ndani ya Bunge na hasa Bunge la jioni la leo. Kuna lugha ambazo zinatumika si za staha. Kwa mfano kuwaita watumishi ambao waliaminiwa na Serikali ambao wanaitwa maafisa utumishi, kwamba ni "mambumbu". Lakini pia kuna mchangiaji mwingine kasema "washamba", tuache

"ushamba". Lugha hizi mi nadhani siyo nzuri sisi kama Wabunge ni kioo cha jamii tukianza tabia hiyo ya kuleta matabaka kuwaita watumishi wa Serikali kwa lugha tofauti tofauti na sisi Wabunge kama mnambuka tuliwahi kuitwa tu humu kidogo kwamba tunachangia kama vile "waganga wa kienyeji" tulikasarika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba mwongozo wako lugha hiyo si nzuri. Naomba ufafanuzi na mwongozo wa jambo hilo ambalo limetokea kwa jioni ya leo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mbunge wa Nyang'hwale Mheshimiwa Hussein Amar kwa Kanuni namba 76 akiomba mwongozo na kanuni ina mpa uhuru kama jambo limetokea mapema leo kama linafaa ama halifai. Lakini pengine kabla sijatoa mwongozo, niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge pia kwamba huwezi kusimama na kuzungumza kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 67(2). Ili usimame kuzungumza inabidi upewe kibali au ruhusa na Mheshimiwa Spika.

Sasa amesimama kwa Kanuni namba 76 kama alivyoitaja, lakini nafikiri ana–*quote* Kanuni namba 71 ya mambo yasiyoruhusiwa Bungeni ambayo yanaainisha pale ndani sasa kwa kuwa ameeleza kwamba imeshatokea tutaielekeza *Hansard* tupitie tuone na kisha baadae tutamjibu kama alikuwa anaruhusiwa au la; kwa hiyo nafikiri tutaitolea muongozo hapo baadae.

Nahairisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 11.33 Jioni Bunge Liliahirishwa hadi siku ya Alhamisi, Tarehe 20 Aprili, 2023 Saa Tatu Asubuhi)*